# CHOZI LANGU

Eliud Mukungu

JAYSONS ELIMU PUBLISHERS
Mwanga wa Elimu

Kimechapishwa na Jaysons Elimu Publishers
Baruapepe: jelimupublisher@gmail.com
Simutamba: +254706392067/+254789954117
Tovuti: www.jaysonspublishers.co.ke
Distribution office: Diani Beach Road, opposite Aghakhan Hospital. Kwale, Diani- Kenya

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika na hulka za kughushi, kuiga, kunakili, kutafsiri au kuchapisha kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile, isipokuwa iwe imeidhinishwa kwa barua kutoka kwa mwandishi na mchapishaji wa kazi hii au kuambatana na masharti ya sheria ya kunakili, kusanii na kuiga (copyright, Design and Patents Act) ya 1988. Mtu yeyote anayefanya kitendo kilicho kinyume cha sheria kuhusu kitabu hiki anaweza kushtakiwa.
©Jaysons elimu publishers
©Eliud Mukungu

ISBN: 978-9914-49-3207

Mhariri: Miriam Biketi Kiwaridi.

Kimechapishwa kwa mara ya kwanza 2023.

TABARUKU

Kwa mwanangu Salma Loice

# SHUKRANI

Kwa mke wangu kipenzi Violet Nasimiyu ambaye alihakikisha nimepata kila kitu kinachohitajika ili kufanikisha uandishi huu. Pia nisingependa kumsahau mwalimu, mwelekezi na kiongozi wangu Bi. Petronillah Asega ambaye kwa sasa ni msimamizi wa idara ya fasihi katika shule ya upili ya St. Paul Emulakha

*Kwanini sikukatazi, mabinti kuwadhulumu,*
*Ukiwatoa machozi, daima kuwahujumu,*
*Walo kosa watetezi, tambua kuna hakimu,*
*Kumbuka yupo mwenyezi, kuna hisabu adhwimu.*

# SURA YA KWANZA

"Mmmh, Majuma tunafanyaje sasa?" Aliuliza mwanadada huku akimtazama mwenzake usoni kwa umakini wenye maana yaa kupata jibu.

"Rehema, hakuna cha kufanya!" Alijibu Majuma na kujiweka sawa kwenye kochi alilolikalia. Kochi lile lilikuwa limechanika chanika pengine lilikuwa la zamani sana. Macho ya Majuma yalikuwa yanazunguka kwa zamu juu ya vitu vichache sana vilivyokuwa ndani ya nyumba yake ambayo wengi waliita kibanda cha kuku kutokana na muonekano mdogo na uchakavu wake maana mlangoni palisitiriwa na bati chakavu.

Ndani ya chumba hiki palikuwa na ndoo mbili za maji, sufuria tatu na bakuli kadhaa. Kitanda kilichoshikilia godoro lake chakavu sana kilikuwa ni miti iliyopangwa vizuri juu ya matofali yaliyokuwa chini.

"Majuma utawezana? Acha utani, hilo si jambo ndogo. Angalia kwanza hali yako ya hapa unapoishi rafiki yangu.Je, utaweza?" Alihoji Rehema jambo ambalo liliupeleka mkono wa Majuma shavuni. Alishika tama huku machozi yakianza kutengeneza mifereji usoni mwake. Alitazama pembeni mithili ya mtu mwenye haya usoni. Majuma hakutaka kukutanisha macho yake na ya Rehema. Hata hivyo, kule alikoelekeza macho kulikuwa kama kitunguu kilichochochea machozi yake kutiririka bila kusimama.

"Sawa! Usilie Majuma, kwa sasa tunapaswa kujua tunafanyaje. Tufanye haraka maana mimi si mkaaji sana, nahitaji kwenda kumuona mama Esta anaumwa."

"Sawa Rehema basi nenda tu." Alijibu Majuma huku akiendelea kulia.

"Majuma rafiki yangu siwezi ondoka nikakuacha bila kufikia hata robo ya uwamzi juu ya hili. Nakuonea huruma sana maana hakuna mwengine maishani mwako."

"Ni kweli Rehema, yani hadi sasa ni wewe tu unayeonyesha

kunijali katika hili, zaidi ya hapo sina mwengine." Alijibu Majuma na kufuta machozi kisha akamgeukia Rehema. Rehema alimuonea huruma rafiki yake.

"Ndio hivyo sasa maana siwezi kuondoka bila kufikia suluhisho la..." hakumaliza kuongea ulisikika mlio. "Kweee!" Ulikuwa mlio uliowafanya wakae kimya kwa sekunde kadhaa. Wakati huo Rehema alionekana kushtuka sana na hili jambo.

"Mmmh! Nini hicho?"

"Usijali ni bati." Majuma alimtoa hofu mwenzake. Lilikuwa bati lililojisogeza pembeni kidogo kutokana na kubandikwa juu ya paa. Mabati hayakugongelewa misumari hivyo upepo ulipopita bati lilisukumwa na kutoa kelele.

"Aah! Sawa. Enhe sasa ukiangalia hali ya hapa unapoishi unadhani utaweza kweli? Maana hili si jambo la utani, unahitaji kujipanga, Majuma utawezana?"

"Sasa nitafanyaje Rehema jamani? Naona hakuna namna."

"Mimi nina wazo" alisema Rehema huku anamtazama Majuma aliyekuwa anamtazama kwa matumaini makubwa.

Majuma alimtazama Rehema kwa umakini. Alisubiri kwa hamu sana kusikia wazo hilo.

"Cha kukushauri hapa ni kwenda kuavya hiyo mimba!"

Huu ushauri ulikuwa kama sauti ya bomu iliyomsafirisha Majuma mpaka kwa mshtuko mkubwa. Alishtuka sana.

"Rehema! Eti nini? Niseme tu ukweli pasipo kuzunguka. Huo ushauri wako ni mbovu, siwezi kuavya mimba hii hata mara moja." Alitamka maneno haya kwa msisitizo uliochangizwa na hasira kali. Rehema alishangazwa na mabadiliko ya ghafla aliyoyaonyesha Majuma. Naye aliamua kupanda juu maana dawa ya moto ni moto eti.

"Nakushauri hivyo kwa ajili ya manufaa yako mwenyewe. Wewe mwenyewe maisha yako yanakutoa jasho, sasa huyo mtoto utaweza kumlea? Utaweza dada?" Alifoka. Hakutaka kumpa nafasi ya kuongea ama kujitetea. Alizidi kufoka kwa ghadhabu.

"Uko pekee yako kwa hili Majuma, huna mwingine wa kusaidiana naye. Angekuwepo baba yake labda ingewezekana…haya yuko wapi huyo baba yake? Fanya mambo kwa akili na si kukurupuka Majuma. Kama unaogopa gharama mimi nitasimamia hilo kuhakikisha unaavya huo ujauzito."

"Mimi naomba nikuambie ukweli, shida si gharama wala hofu ya kumlea mtoto akizaliwa. Niko tayari kuvumilia shida hizi kwani mvumilivu hula mbivu na ninaamini nitamzaa salama na nitamlea hata kwa ugumu ila sio kuua kiumbe kisicho na hatia. Siwezi fanya dhambi kwa makusudi kabisa." Alifoka Majuma asitake kabisa kuavya mimba ambayo ilikuwa ya miezi minne iliyomsumbua mno.

Halikuwa jambo rahisi kuamini kuwa hawa walikuwa marafiki wakubwa na ambao muda mfupi uliopita walikuwa wanaongea kwa maneno mazuri na laini mithili ya mafuta. Hali ilibadilika ghafla kila mmoja akawa mkali kama pilipili. Hali ya maelekezano na maelewano ilitoweka pale ndani, sasa kila mtu aliongea kadri alivyoweza.

"Mimi yangu macho tu, lakini chunga usije anza kutuletea letea sauti zako za vilio eti oooh nahitaji msaada….oooh mtoto kafanyaje…..mtoto hili." Alifoka Rehema huku amebana pua.

Majuma kwa wakati ule alikuwa ameona kwamba aliyekuwa naye hapa ndani ni shetani. Ikawa bora amfukuze.

"Binti, kwanza nakuomba toka nyumbani kwangu. Shetani ushanitibua zaidi. Ondoka nyumbani kwangu," alisema na kumsukuma mwenzake hadi nje. Rehema alitoka huku akiendelea kuongea kwa uchokozi zaidi.

“Halo haloo, hata banda la kuku nalo ni nyumba! Nina shaka maana hao kuku wenyewe wanaweza kugoma kuishi humo.” Rehema alisema maneno yaliyojaa kashfa na kejeli. Wapitia njia waliyasikia vizuri haya maneno. Walitazama nyumba yenyewe nao wakaangua kicheko. Majuma alitatizika moyoni.

Baada ya sinema hiyo alirudi ndani akiwa mnyonge sana huku machozi yakiendelea kumbubujika bubuji bubuji! kama kitoto kidogo akawa hajitambui wala hajifai tena. Alikaa sakafuni bila kuhofia vumbi. Angewezaje kuogopa vumbi wakati nguo zenyewe zilikuwa chafu kama beberu?

Hakujua ni hasira au ni maumivu moyoni mwake yaliyokuwa yanasababisha uso wake kuchafuliwa na machozi. Majuma alilia na kila mara alipotazama nyumba yake hayo machozi yaliongezeka maradufu. Pia alipotembeza macho juu ya tumbo lake, uso ulichafuka zaidi huku moyo ukijaribu kuyarejelea maneno ya rehema lakini hakuwa tayari kufuata ule ushauri.

“Najua hii ni kama vita lakini naamini nitashinda” alisema na kuinuka kwenda kuchota maji kwenye ndoo moja kuukuu iliyokuwa imehifadhi maji ya kunywa.

Alichota maji na kuyabugia mdomoni. Alipiga mafunda matatu na kumaliza kikombe cha kwanza. Kutokana na kiu na njaa aliamua kuongeza kikombe kingine cha maji. Alijipweteka pwetepwete tena sakafuni huku akiruhusu akili yake kutafakari hili na lile. Majuma akawa amezama moja kwa moja ndani ya bahari ya luja akitafari jana yake!

Matukio ya nyuma yalirudi haraka kichwani mwake. Hakutaka kuyakumbuka sana kwani mara nyingi akiyakumbuka huwa yanampeleka katika kilio cha kwikwi. Muda nao uliendelea kusonga na sasa ilikuwa saa tisa alasiri. Tumbo lilihitaji kupata kitu! Ila ni kitu gani angeweka tumboni mwake? Angepata wapi hicho kitu? Alimkumbuka mume wake, aliamini kuwa angekuwepo basi angeweza kutafuna hata

kipande cha muhogo muda huu. Hakuwa na namna ila aliona ni heri aende kwa mamake. Chambilecho mtoto hufuata kisogo cha nina yake.

"Anikatae asinikatea mimi naenda, huko nitapata chochote cha kutia tumboni kuliko kubaki hapa. Mbona nikae na kumtesa mwanangu aliye tumboni."

Taratibu alijivuta hadi kwa mama yake. Hapakuwa mbali sana ndio maana ndani ya dakika kumi na tano alifika.

" Wewe mwanaharamu umefuata nini hapa? Ondoka sitaki nikuone, ondokaaaa!" Alikaribishwa kwa namna hii.

"Aah, lakini mama...!"

"...hakuna cha lakini hapa…ondoka la sivyo ntakufinya" alifoka mama yake.

Majuma aliona dunia yote imemkataa maana hata mzazi wake ambaye alihisi angekuwa mwokozi wake na mwanawe wakati huu wa shida pia ameungana na wanadawamu wengine kumkana na kumfukuza kama mbwa mwizi. Aligeuka na kuondoka huku michiririzi ya machozi na majonzi ikaongozana naye. Wakati huo kumbukumbu ya mambo yote yaliyotokea nyuma iliendelea kukitesa kichwa chake.

Alitembea huku analia. "Kwa nini mama hataki kunisamehe? Bado ananihesabia kosa wakati sina kosa kwa nini?" Majuma alilalamika kwa uchungu, huku nyuma mama yake naye aliendelea kupaza sauti ya hamaki.

"Na sitaki nikuone hapa ibilisi wewe. Sitaki uje kwangu muuaji mkubwa." Kila neno lililotamkwa na mama yake halikuwa tofauti na msumari wa moto uliokuwa unapekecha moyo wake. Maneno yalikuwa makali kama mshale kwa binadamu, kweli mchungu.

"Ndivyo ilivyo mitoto ya siku hizi, inajiona imekua hata kwa mama zao. Acha likome." Yalikuwa maneno ya wapita njia. Majuma aliumia zaidi. Yote hayo yaliamuru macho yake kutoa machozi yaliyokuwa na kazi moja ya kuchafua uso. Alirudi hadi nyumbani kwake na kufungua mlango wake ambao ulikuwa ni bati tupu lililozipa pale mlangoni. Aliingia ndani

na kujitupa kwenye kitanda chake ambacho wewe ungekiona ungekiita mbavu za mbwa. Kwake ilikuwa ni sawa na mtu aliyekuwa ndani ya jengo la ikulu maana hakuwa na budi ya kukikumbatia kilivyokuwa. Angefanyaje sasa? Alikubaliana na kuikubali hali yake. "Haya yote yasingetokea kama isingetokea wewe Fitina. Nakuchukia Fitina." Alisema Majuma huku anafuta machozi.

******

Mzee Saradibo ni mmoja kati ya watu maarufu waliosifika kuwa na mali nyingi sana ndani ya kijiji cha Munduma Kakamega. Mifugo na mashamba aliyokuwa nayo ilikuwa sababu tosha ya kujumuishwa kwenye tabaka la wenye navyo. Saradibo hakuwa tajiri kiasi hicho, lakini kulingana na umaskini uliyokuwa umetapakaa Munduma ilikuwa lazima kumuita tajiri. Licha ya mali zake zote kwake neno furaha liliwekwa kwenye kamusi za Kiswahili kama ajali isiyo na kinga, halikufaa. Kwani wakati wote wazo na tamaa juu ya mtoto vilimtesa sana na kumnyima raha. Hakuwa na mtoto hata mmoja ambaye pengine atarithi hata shamba moja. Alikuwa na umri wa miaka 50 na miaka 30 ndani ya ndoa bila mtoto. Alihangaika hapa na pale pasipo mafanikio yoyote yale, aliendelea kujipa tumaini kuwa ipo siku angepata hitaji lake. Bado alipata shida akilini mwake. Mawazo yalimtesa. Hakujua lini ataitwa baba.

Wahenga walisema atafutaye siku zote hachoki. Mzee Saradibo hakuchoka wala kukata tamaa. Mungu si athumani! Baada ya mahangaiko ya muda fulani, walijaliwa na mtoto wa kike baada ya kuhangaika kwa miaka na mikaka. Kwa furaha waliokuwa nayo wakamwita Majuma Binti Saradibo.

Majuma alilelewa vizuri sana. Kila alichohitaji alikipata tena kwa wakati. Kadri alivyoendelea kukua ndivyo mafundisho ya maadili mema yalivyoongezeka kwake. Wazazi wake walihakikisha wanampa maadili yaliyo bora zaidi. Upekee wake ulichochea huduma nyingi na nzuri. Zaidi ya yote, wazazi wake walijua kwamba urithi bora ni elimu basi Majuma

alipelekwa shule. Miaka iliendelea kusonga hadi wakati alipokuwa kidato cha tatu.

Majuma alitesa watu kwa juhudi zake darasani kwani alijikaza kisabuni pamoja na uzuri na urembo uliomzidi hurulaini wa peponi. Wale wanafunzi waliokuwa wanapenda mambo ya kikubwa walimsumbua sana, hata hivyo hakuwasikiliza. Alisoma kwa bidii. Alikuwa makini sana hasa katika uchaguzi wa marafiki kwani kila mara wazazi wake walimsisitiza juu ya hili. Wakati huu ndio wakati alipounga urafiki na Fitina. Fitina alikuwa msichana ambaye walikuwa darasa moja. Majuma na Fitina walikuwa marafiki walioshibana sana.

Kwa namna inayoeleweka ni kwamba walikuwa chanda na pete. Walitembea pamoja, walisoma pamoja, pengine kutowaona pamoja hawa wasichana wawili warembo ilikuwa jambo ngumu kuliko ugumu wa jambo lolote gumu. Urafiki ukizidi, wahusika huwa kama ndugu wa kuzaliwa, tena wale mapacha kwa maana tabia na mambo mengine mengi huwa sawa kabisa. Tembea yao hata ongea yao walishaathiriana. Tabia zao zilifanana mno nazo juhudi zilikuwa sana. Majuma akishika nafasi ya kwanza naye mwenzake nafasi ya pili darasani. Wavulana walipata taabu sana.

Maisha yaliendelea hadi kidato cha nne huku kila mmoja akiomba kwa dhati ya moyo wake ili kuweza kupangwa shule moja katika ngazi ya "Advance". Hivi utataka nini tena kutoka kwa muumba wako kipindi umepata maombi ya majibu yako? Ulie? Au utake gunia la misumari! La hasha! Furaha ndio hitaji na hutawala kila jambo.

Ndivyo ilivyokuwa kwa Majuma na Fitina. Mungu alijibu maombi yao kwa kuwapatia nafasi ya kuendelea kuuenzi urafiki wao wa dhati. Wote walifaulu na walipangwa kwa shule moja ambayo ilikuwa ya mchanganyiko yaani ina wavulana na wasichana mkoani Nakuru nayo ni Kijiweni. Kwa nini wasifurahi wakati wataendelea kuwa pamoja? Tena wamepata nafasi ya kubadilisha mazingira. Walitamani waende haraka ili

wakaonje hewa safi ya Nakuru kidogo kwani mara nyingi wamesoma sifa nyingi darasani kuhusu Maisha ya Nakuru ikiwemo L. Nakuru.

Wakati ulipofika, walifanikiwa kujiuga na masomo ya kidato cha tano. Maisha yaliendelea huku urafiki wao ukiendelea kupamba moto na kustawi zaidi ya mara ya kwanza. Miezi mitatu baadaye tayari walishazoea maisha ya kidato cha tano ndani ya Nakuru, haya mazoea yalikuwa bora sana kwa mwanafunzi yeyote yule. Ni vema kuzoea mazingira japo huchukua muda. Sijui ni wahenga ama ni sisi tu tuliosema kwamba hakuna jambo lenye faida likakosa kasoro, kila jambo lina faida na hasara zake eti

Licha ya faida kibao za ile hali ya kuzoea mazingira na maisha kiujumla pia kulikuwa na hasara zake hasa kwa upande wa Fitina. Nakuru ilimkaa vizuri Fitina, ukimwona utadhani ni mzaliwa wa mkoa huo. Ule upole wake na tabia njema vikaanza kuyeyuka kama barafu kwenye jua kali.

″Fitina siku hizi sikuelewi." Alisema Majuma siku moja wakiwa chumbani kwao. ″Hunielewi kivipi tena?″ Aliuliza Fitina huku akimalizia kupaka poda uso wake uliokuwa ushapodoka vilivyo.

“Mmmh! Unaeza niambia unajiandaa kwenda wapi?” aliuliza Majuma

“Oooh! Natoka kidogo, si unajua jana sikufanikiwa kupatana na Japhet kama tulivyopanga maana Kelvin alinishikilia kweli kweli pale jana” alisema huku macho yakiwa kwenye kioo. Wawili hawa walikuwa wanaishi kwenye chumba cha kupanga.

“Mwanzo haukuwa hivyo unajua. Imefikia wakati hurudi nyumbani kabisa siku nzima.” Alilalamika Majuma aliyekuwa bado amejilaza. Ilikuwa Jumamosi kwa hivyo hawakuwa na kipindi.

“Changamka Majuma. Uko Nakuru rafiki yangu na wala sio huko vichakani” alisema kisha alipomaliza kuupodoa uso wake alitazama mavazi yake. Alijizungusha hapa na pale na kumtazama Majuma.

Nimependeza eh!

Majuma hakujibu chochote zaidi, alinyanyuka pale kitandani na kusali kidogo pamoja na kumshukuru Mungu wake kumlinda salama usiku.

"Haya mama kanisa, mimi naondoka" alisema Fitina baada ya kuchukua kibegi chake…..huyooo alitoka. Majuma alisikitika sana kumuona rafiki yake amekuwa tofauti na mwanzo, wakati huo walisisitizwa sana juu ya suala hili. Wazazi waliwaambia wasisahau gharama zinazotolewa kwa ajili yao katika kuhakikisha wanasoma tena katika shule nzuri. Walishauriwa wasome kwa bidii na kuyapa kisogo mambo mengine yasiyo ya lazima. Majuma alishangaa kuona mwenzake akienda kinyume na hayo. Alisahau yote aliyoambiwa, yeye anakula raha ya mji. Fitina alikuwa hana muda na wasichana wenzake. Marafiki zake kwa sasa ni wanaume, pengine isingekuwa kuishi pamoja na Majuma hata urafiki wao ungekuwa ushakufa maana tayari ulianza kudidimia. Jumamosi hiyo ilikuwa Jumamosi kubwa iliyobeba maana halisi ya wikendi kwa binti Fitina. Alikutana na mtu wake ambaye aliahidiana naye kukutana siku hii baada ya kushindikana siku ya nyuma.

Walikutana na Japhet, huyu kijana hakuwa mwanafunzi bali ni mtu wa mtaa. Walifurahi kwa kadri walivyoweza na kwa namna waliyotaka. Kwa mziki, pombe na mengine mengi ndani ya baa moja iliyopo maeneo ya Vegas. Mida ya usiku sana ndipo aliporudi nyumbani akiwa amelewa mno. Ilikuwa kazi kwa Majuma kuanza kushughulika na mlango kumfungulia mwenzake. Kabla Fitina hajaingia harufu ya pombe iliingia ndani na kulipapasa pua la Majuma. Hakika Majuma alichefuka na kushtuka kuona kumbe hata pombe mwenzake anatumia. Ilikuwa ngumu kuamini moja kwa moja lakini ushahidi ulikuwa mbele yake.

"Majuma rafiki yangu! Binti mlokole." Fitina aliongea kilevilevi wakati huo ameegemea mlango.

“Ingia basi utabomoa mlango” alisema Majuma na kuziba pua akitamani Fitina asiingie tu. Hata kile kitendo cha kumwambia aingie ni basi tu kwa kuwa hakuwa na namna.

“Acha uharibike mimi nitalipa, kwani pesa ndo nini!” aliongea huku anafungua kibegi na kutoa noti nyingi za elfu moja moja. Majuma alitokwa na macho utadhani mjusi kabanwa na mlango. Kwa muda huo huo, macho yake yalitua juu ya simu kubwa ya iPhone aliyoitoa Fitina kutoka kwenye kibegi kile.

“Haya ndio maisha, wewe endelea kumpa Bwana sifa akupe vitu kama hivi” aliongea tena kiulevi na kucheka kwa dharau. Alitoka pale na kwenda kujitupa kitandani.

“Majuma wewe ni mwongofu, usitamani mali ya mwingine” aliishia kumumunya maneno kwani usingizi ulimbeba ghafla kutokana na uchovu wa hali ya juu. Muda wote huo macho ya Majuma yalikuwa kwa Fitina aliyelala. Yalikuwa macho yaliyojazwa na mshangao mkubwa juu ya mwenzake kulewa, kuwa na mafaranga yote yale pamoja na simu kubwa. Kavitoa wapi? Alikumbuka pale ni mjini kama alivyoambiwa. Alitikisa kichwa kwa masikitiko makubwa. Aliwaza namna ya kulala asijue, alale na mlevi? Alitandika kanga chini na kuuvuta usingizi kwa taabu.

Siku zilisonga mbele kwa kasi na sasa ilikuwa Jumapili fulani majira ya saa nne asubuhi wakati Majuma anajiandaa kwenda kumpa sifa Mungu wake. Fitina nae alikuwa anaweka mambo sawa kwenda kufurahia raha za dunia. Majuma alitangulia kutoka na kwenda kanisani kisha baadae naye Fitina alitoka.

Kutokana na ibada kuwa ndefu pia mazoezi ya kwaya Majuma alichelewa kurudi nyumbani. Alirudi majira ya saa moja usiku. Alishtuka sana baada ya kufika nyumbani na kukuta kufuli linaning’inia mlangoni.

“Mmh! Bado hajarudi” alisema na kwenda kuangalia mahali wanapoweka funguo siku zote. Funguo hazikuwepo. Ulikuwa mtihani

mzito kwake, hakujua atafanyaje na kama anazo mwenzake atazipataje wakati hajui yuko wapi. Funda la hasira lilimkaba kooni. Alitamani kulia. Akiwa katika hali hiyo, alishtuliwa na sauti ya mpangaji mmoja wa kiume.

"Chukua simu, ongea na mwenzako." Majuma alipokea simu na kusikiliza upande wa pili.

"Majuma samahani, nilijisahau nikatoka na funguo….kuja hapa Bahati kwa baa inaitwa Tushikamane. Chukua bodaboda nitalipa" alieleza Fitina. Majuma alifika na kuchukua funguo huku hasira zikipungua sasa.

"Chukua na hizi pesa, ni zako," alisema Fitina na kumpatia mwenzake.

"Zimetoka wapi?"

"Wewe chukua bana, acha ushamba." Fitina aliongea kwa ukali kidogo, ilibidi Majuma apokee japo kwa kusita.

"Haya nenda nyumbani lakini usiogope, sawa Majuma? Usiogope," alisema maneno yaliyompa maswali na wasiwasi Majuma. Alipanda tena bodaboda na kurudi nyumbani. Ilichukua dakika tano tu kufika. Bado akili yake haikukaa sawa kabisa, iliwaza hizo pesa ambazo ni shilingi za Kenya elfu kumi. Zimetoka wapi? Ni zake! kwa kazi gani? Na mbona asiogope? Alifungua mlango haraka ili apike maana hata njaa ilikuwa inamkeketa maini. Aliingia ndani na kufunga mlango kisha alibonyeza swichi, taa ilitoa mwangaza ulioenea chumba kizima.

"Mamaaaaaaaa!" Majuma alipiga kelele.

"Wewe msichana mzuri acha kuogopa" ilikuwa sauti ya kidume kilichokuwa kimejilaza kitandani. Kilikuwa katika vazi la bukta na tisheti nyepesi. Kwa haraka haraka ukimtazama hakuwa anavuka miaka 25, alikuwa na mwili umejazia jazia. Alitoka pale kitandani na kuanza kupiga hatua kuelekea mahali alipokuwa Majuma aliyebaki anatetemeka kwa uoga. Majuma aliziba macho asimtazame maana alihisi kama simba anamsogelea. Mkono wenye nguvu ulianza kutembea mwilini mwake na kabla hajakaa sawa alibebwa msobe msobe hadi kitandani.

“Jamani nafaaa,” alitoa sauti ya kulalamika kwa uchungu lakini sauti hii iliishia mle chumbani maana kile kichumba kilikuwa hakiruhusu sauti yeyote kutoka nje endapo mlango umefungwa.

# SURA YA PILI

"Fitina mbona unaniangusha bana?"

"Sio kama nakuangusha Joshua ila kama unavyomjua huyo msichana, ana ulokole mwingi sana jambo ambalo linanipa ugumu kuanza kumshawishi."

"Ah!! Lakini pesa zangu ushakula, tena mara mingi tu…..ni wiki sasa imepita sijampata huyo msichana," Joshua alilalamika na kuonyesha wazi kuwa alichukia.

"Nivumilie kidogo basi, leo akirudi kutoka kanisani nitamwambia"

"Hapana! Hizo ndio ahadi zako za kila siku sasa nimechoka, kama ni ngumu nirudishie pesa zangu" alisema kwa hasira. Fitina alishtuka na kujiweka sawa pale kitandani. Pesa zenyewe ashatumia angerudisha vipi? Hata kama angekuwa nazo hivi kabisa kabisa akubali kurudisha?

"Basi Joshua unaonaje unitumie mimi tu…jilipe na mwili wangu" alisema na kwenda kufunga mlango.

"Hapana! Mimi namtaka yule mwenzako na si wewe maana tushakuzoea" mambo yaligonga mwamba. Fitina alikosa cha kusema sembuse cha kufanya?

"Nimepata wazo, kwa sababu mimi natoka leo basi nikufungie humu ndani alafu yeye atakaporudi kutoka kanisani unamalizana naye." Alisema Fitina. Joshua alifikiria kidogo kisha akasema

"Ni wazo nzuri lakini akipiga kelele je?"

"Hiki chumba hakina shida, cha msingi na muhimu mlango na dirisha vifungwe, hakutakuwa na tatizo lolote lile." Fitina alisema kwa kujiamini.

"Una uhakika?"

“Yes, this is a sure deal, ushindwe tu mwenyewe.”

Joshua alifungiwa ndani wakati Fitina anaondoka kwenda kwa baa kule Bahati.

“Hata hizi ufunguo acha niende nazo” alijisemea na kuchukua bodaboda hadi Bahati wakati huo huku ndani Joshua alikaa akiwa na hamu zake nyingi. Alishajipanga kwa tukio na ndio maana hata suruali yake aina ya jinsi alivua na kubaki na bukta. Muda uliendelea kuyoyoma bila mtu anayemsubiri kufika. Mlango ungekuwa wazi, angekata tamaa na kuondoka. Njaa nayo ilianza kumkejeli. Alichungulia ndani ya sufuria tatu zilizokuwa hapo ndani, hazikuwa na chochote.

“Hyaaaam!!” alipiga muayo. Kila muda aliangalia saa yake ya mkononi na ubaya zaidi simu yake aliiacha nyumbani kwenye chaji. Angekuwa nayo hapo angempigia Fitina arudi kumfungulia ili aondoke atafute chakula. Mida ya saa moja usiku ndipo anashtuka kusikia mlango unafunguliwa na kumuona mwanamwali aliyemsubiri kwa muda mrefu. Alikuwa na hasira naye kwa hivyo alimbeba msobe msobe hadi kitandani. Baada ya kutimiza hitaji lake alivaa nguo na kuondoka huku akijisifu

“Elfu ishirini zangu zimeenda kwa haki, mtoto alikuwa mbichi kabisa, mimi ndio mfunguzi”

Huku nyuma Majuma alikuwa kwa hali mbaya sana. Tunda lake lilikuwa limetundwa bila kibali chake. Mtoto wa watu alilia kwa kunyimwa haki ya kutenda atakalo yeye. Maumivu nayo hayakumpa nafasi ya kufikiria. Yalimtafuna kisawasawa hata kutembea hakuweza. Alijaribu kuinuka ili akausafishe mwili wake kuondoa damu zilizotapakaa lakini hakuweza kupiga hata hatua moja, alichechemea kidogo na kuanguka chini.

******

Muda wa saa sita usiku Fitina alirudi. Muda huo hali ya Majuma haikuwa nzuri bado. Alijikalia chini kama kiwete asiye na uwezo wa kuinuka. Uso wake ulijawa na machozi. Hakutaka hata kumtazama

mwenzake. Alimuona kama jambazi sugu mwenye roho ya kikatili ambaye anaweza kukuua kwa sekunde chache. Majuma alitazama upande mwingine huku akijaribu kuzishinda hasira kali zilizokuwa zinampanda kwa kasi dhidi ya Fitina aliyekuwa ameingia huku anayumbayumba baada ya kupiga mtindi.

"Wewe binti mlokole, binti wa bwana, unalia nini?" Namna alivyoongea alidhihirisha wazi kuwa anaelewa kinachoendelea. Majuma alizidi kupata hasira zilizokuwa zinampa nguvu ya kunyanyuka na kumrarua rarua Fitina. Uwezo wake kuzishinda ulikuwa mkubwa kuliko nguvu ya hasira.

"Alafu umeanza uchafu, unachafua ndani na hata usafi hufanyi wala huogi, mama kanisa mchafu." Alisema huku akiyumba, alimpiga kofi mwenzake kisha yeye alianguka kitandani na kupitiwa na usingizi mzito uliochangiwa na uchovu mwingi. Majuma alilia sana kila alipokumbuka yote aliyofanyiwa siku hiyo.

"Nimekukosea nini Mungu? Mbona hukuniepusha na huu ubaya? Kwa nini umeruhusu hili litokee? Naumia jamani..." alilia mno kila alipokumbuka kuwa usichana wake haupo tena. Usichana kwa msichana ni kama dhahabu ama mali yoyote yenye thamani ghali sana na ndio maana wengi huumia sana wanapopoteza usichana wao hata kama waliupoteza kwa ridhaa na matakwa yao wenyewe hulia na kujilaumu sembuse kuipoteza kwa njia ya ukatili? Alilia alipokumbuka kuwa usichana wake umepotea tena na mtu asiyemjua zaidi ya kuambulia kuiona sura ambayo yenyewe inaweza kupotea katika kumbukumbu. Katika kipindi chote cha maisha yake hadi hapo alipofikia kidato cha sita, hakuwai kukutana kimwili na mwanaume yeyote. Alijichunga sana kufuatia kauli ya kila mara kutoka kwa mama yake iliyokuwa inamsisitiza kujitunza na kuutunza usichana wake kwa ajili ya mume wake wakati atakapoolewa. Leo usichana huo haupo.

"Jitunze mwanangu, tunza usichana wako maana hata wanaume wanapenda wanawake waliojitunza" hii ilikuwa kauli ya mama yake.

“Nani atanioa sasa? Nitamwambia nini mama? Kwani nimekosea nini mimi?” Alilia kama mtoto mdogo. Aliona dunia imekuwa mzigo mzito, tena uzito huo ambao binti wa hirimu yake hangeweza kujitwika wakati huo. Usiku huu hakulala wala hakufanya chochote hata kwenda kujisafisha alishindwa. Mawazo yalikuwa mengi sana. Yalimtesa kichwani na kumzawadia kilio kisichoisha, kilio kilichofanya akose usingizi. Alilia mpaka macho yake yaliyokuwa meupe pepepe yakavuja damu na kuwa mekundu. Saa nayo bila huruma iliendelea kusonga mbele japo binti huyu alikuwa amekesha kutwa kucha akiwaza na kuwazua asipate jibu. Ilikuwa saa nane, nazo sekunde ziliendelea kukimbizana kwa madaha. Wakati huo hata chembe dogo ya usingizi haikuwepo machoni wala kichwani mwa Majuma. Fitina alikuwa anakoroma kama fahali zizini miguu kaitupa huko na huko. Baada ya kuwaza sana ndipo akatambua kuhusu zile pesa elfu kumi alizopewa na mwenzake alipofata ufunguo.

“Nimeuzwa mimi” aliendelea kulia. Majira ya saa kumi na moja, usingizi ulimuonea huruma, alijilaza pale chini bila kujua.

Ni Jumatatu sasa, pengine ni kutokana na kuchelewa kulala ndio maana aliamka mida ya saa tatu asubuhi.

“Mungu wangu, nimechelewa shule.” Alitazama huku na huku hakumuona mwenzake kwani alikuwa pekee yake. Alisimama haraka ili ajiandae. Halwoho! Majuma alikuwa amesahau yote. Maumivu aliyoyapata baada ya kuinuka haraka yalimkumbusha kilichotokea usiku huo. Isingekuwa kushikilia kitanda angeanguka. Bado hali ilikuwa mbaya. Hii siku ilipita Majuma akiwa akilia kwa kutendewa unyama kwa njama za rafikiye wa karibu. Chambilecho umdhaniaye siye kumbe ndiye. Majuma hakwenda shule kwani moyoni alikuwa na kinyongo, kula hakula, kilio na machozi vilikuwa chakula chake. Jumanne nayo ilipita hata Jumatano pia ikapita. Mwili ulikosa nguvu kwa kutokula. Macho yalivimba na yalikuwa mekundu kwa kulia.

Alhamisi alijiandaa uji na baada ya kula alijitahidi kufika shule. Huku sasa ilikuwa shida, licha ya kumwambia mwalimu kuwa alikuwa anaumwa hakusikilizwa.

"Leta kibali cha daktari" alisema mwalimu Bakora ambaye alikuwa zamu. Majuma alikosa cha kusema maana hata hicho kibali hakuwa nacho. Alitamani aseme ukweli wa mambo lakini aliogopa na kuaona aibu.

"Nyinyi ndio wahuni, hamtaki kuja shuleni yenu ni kutanga. Tunawasaka sana watu kama nyinyi mnaoharibu sifa za shule yetu. Sasa leo utanitambua." Mwalimu Bakora alifoka na kumvuta mkono hadi ofisini. Bakora kali zilianza kusikika zikirindima ndani ya ofisi.

"Mwalimu mimi sina hio tabia" alijitetea lakini utetezi wake haukutosha kumshawishi mwalimu Bakora asimpige. Majuma alishuhudia kofi zito likitua shavuni mwake.

"Unadhani mimi ni mtoto mdogo? Kwa hivo mimi nakudanganyia?" mwalimu Bakora alifoka na kurusha bakora bila kujali inaenda kutua mahali gani ikishafika kwenye mwili wa Majuma. Ile bakora ilitua shingoni kidogo tu itue usoni. Majuma alilia kwa uchungu wa bakora na kwa kusingiziwa. Aliogopa kujitetea kwani kujitetea ilikuwa ni sumu kwake. Mwalimu aliendelea kumpiga utadhani walikuwa na ugomvi pale nyuma.

"Hey! Mwalimu, mbona unampiga mwanafunzi kiasi hicho? Alishaa mwalimu Herman baada tu ya kuingia ndani ya ofisi ile.

"Hawa ndio ninaowatafuta siku zote, wanachafua shule yetu kwa tabia zao za umalaya." Mwalimu Bakora alitamka pasipo kujali ukali wa maneno wala uhalisia wake.

"Lakini mwalimu una uhakika kweli hiyo ndo tabia yake? Isije kuwa unamuadhibu kwa kosa lisilokuwa lake." Alisema mwalimu Herman na kutoka baada ya kuweka vitabu vyake mezani. Hali alioikuta iliendelea. Majuma alidhani labda itakuwa afueni ila wapi. Alitamani kutoka na

kukimbia ila huo uwezo alikosa. Alilia hadi machozi yaligoma kutoka tena.

"Mwalimu unanionea tu bure, mimi sina hio tabia." Aliongea huku analia. Mwalimu alichukia zaidi. Majira ya jioni alirudi nyumbani akiwa hoi bin taabani kutokana na yote yaliyomkuta siku hiyo. Yote yalimuumiza hakuwacha kulia hata kidogo. Aliamini chanzo cha hayo yote ni Fitina. Alitamani ahame hapo nyumbani aende sehemu nyingine ila angeenda wapi? Ataenda kukaa bure? Hakuwa na uwezo wa kupanga chumba kingine.

Hata angewaambia wazazi wake wangemshangaa na kumhoji sana. Kwa nini anataka kuhama? Angewajibu nini wakati hakuwa tayari kueleza ukweli? Hakujua ni kwa nini alificha ukweli juu ya yote aliyofanyiwa na Fitina. Hakujua kwamba ni kwa sababu anampenda ama ni woga tu katika kusema ukweli. Hata sasa kama ingetokea akaulizwa ni nini kilimkuta bado hakuwa na uwezo wa kuweka bayana. Ndani ya nyumba walikuwa kama mabubu. Hamna yeyote aliyejaribu kuzungumza chochote kwa mwenzake. Majuma hakutaka kabisa, alimuona Fitina kama shetani mwenye roho ya usaliti. Muda wote alijiinamia, nayo machozi yakamtoka hasa alipokumbuka kuwa alikuwa ameupoteza usichana wake. Alilia sana.

Siku ya Ijumaa, baada ya Majuma kujiandaa vizuri alitoka na kuelekea shuleni. Mawazo mengi yalikisumbua kichwa chake kila alipojaribu kuwaza juu ya kitakachotokea leo. Hakutaka kuwa na hofu sana kwani aliamini ya jana ni ya jana tu. Majira ya saa nne asubuhi, alishtuka kusikia anaitwa ofisini kwa mwalimu mkuu wa shule. Mapigo ya moyo yalienda kasi. Hakujua anaitiwa nini. Alitembea kwa haraka huku hofu ikiwa imeanza kumvaa. Majuma alifika ofisini. Kabla hajaingia, macho yake yalitua juu ya walimu sita kwa idadi waliokuwepo mle ndani. Mwalimu Bakora alikuwa miongoni mwao. Majuma aliogopa.

Majuma alitoa salamu ambayo ilimfanya ajilaumu kwani hakuna mwalimu aliyeitikia. Mwalimu mkuu hakutaka kupoteza muda.

“Nyinyi kidato cha sita mnakaribia kufanya mtihani yani mmebakisha miezi mine tu. Tunawategemea ila mwenendo wenu hautupi matumaini kabisa. Mna tabia mbaya hivyo tunaanza na wewe.”

Majuma alitetemeka na kugundua kumbe yale mambo hayakuisha kwani mwalimu Bakora aliyafikisha kwa mkuu wa shule. Kama kawaida, Majuma alijitetea vya kutosha ila aliambulia kipigo cha mbwa mwizi. Alipigwa hadi baadhi ya walimu wakamuonea rehema

“Jamani mimi si muhuni, kama hamuamini basi muulizeni Fitina.” Alilia Majuma.

“Fitina ndio nani?” aliuliza mwalimu mkuu.

“Mwenzangu ninayekaa naye, naye pia ni form six”

Muda si mrefu Fitina aliitwa kuulizwa haya mambo juu ya mwenzake. Kwanza alishangaa kuona namna mwenzake alivyopigwa hadi kuvimba

“Wewe msichana unamjua huyu?” lilikuwa swali la mwalimu mkuu.

“Ndio. Ninakaa naye.” Fitina alijibu akijifanya ana ujasiri lakini alikuwa anatetemeka kwa uwoga.

“Sawa. Hatutaki kuzunguka na ninaomba uwe mkweli. Rafiki yako hatulii, anahangaika na wanaume, ni kweli au si kweli?” aliuliza mwalimu Bakora kwa wakati huu. Fitina alijing’atang’ata bila kujua ajibu nini.

“Wewe tunakuuliza” alifoka mwalimu Bakora na kurusha fimbo na kumpiga Fitina.

“Ndio mwalimu, ni ukweli.” Fitina alijibu.

Moyo wa Majuma ulishikwa na ganzi iliyosababisha ubaridi wa kipekee kama umemwagiwa maji. Alihisi alichokisikia hakikuwa sahihi, labda maskio yamepokea taarifa tofauti na ile iliyotolewa. Alichokisikia ndicho kilichotamkwa tena kilisisitizwa zaidi.

“Ndio ni kweli Majuma hatulii nyumbani, anahangaika na wanaume hata muda wa kujisomea hana.”

Kama Majuma angekuwa na tatizo la presha, kwa kweli angeanguka na kuzimia papo hapo.

“Paaaaaah!!!” Ilisikika kofi iliyotambaa kwenye shavu la kushoto la binti huyu. Akupigaye shavu la kushoto mgeuzie na la kulia. Majuma hakugeuza lakini alishtuka akipigwa kofi nyingine zito kwani ilisababisha kizunguzungu kilichombwaga chini kama mzigo. Kilio hakikuisha, kilisikika bila kukoma. Angejiteteaje wakati shahidi ameshathibitisha hilo? Majuma ugumu ulikuwa wapi kusema ukweli?? Aaah!!

“Huyu Fitina ndio...” Aliongea kwa upole akiwa chini palepale ila hakumalizia kusema, mwalimu mkuu alidakia na kwa hasira alifoka.

“Acha kutupigia kelele na uongo wako pumbavu!”

“Yani muda wote unatusumbua tu na kutudanganya, unatuona sisi wapumbavu eeh? Unatuchukulia sisi ni watani wako?” mwalimu Bakora alifoka na kurusha fimbo iliyotua mgongoni mwa Majuma.

“Aaaaiih!!” aliishia kutoa mlio wa maumivu. Kuinuka alishindwa kwani kizunguzungu kilimbana chini. Alipigwa fimbo zingine mbili za mgongoni, aliamua asimame la sivyo kifo kitamkuta pale chini. Alivyosimama tu alipepesuka na kushika kichwa kwani bado kizunguzungu kilimshika. Alipepesuka na kuanguka. Aliangukia mezani kwa mkuu na kufanya vitu vilivyokuwa vimewekwa katika mpangilio mzuri vitawanyike. Alizawadiwa kofi na kusukumwa kwenda chini kidogo tu ajipigize kisogo kwenye sakafu.

Pembeni alikuwepo mwalimu Herman, alionekana akiupeleka mkono wake ulioshika kitambaa na kufuta chozi lake. Alimtazama Majuma aliyekuwa ameanguka na kubaki palepale kisha akasema.

“Jamani hata kama ana makosa lakini sio kwa adhabu ya namna hii, naye ni binadamu, anasikia maumivu.” Alisema huku walimu wote wakisikiliza, wakati huo Fitina aliruhusiwa kuondoka.

"Kwa hivyo unatetea uovu?" aliuliza mwalimu mkuu kwa hasira hadi mwalimu Herman akanyong'onyea ila alijiwekea ahadi ya kumsaidia Majuma. Majadiliano yalifanyika. Walimu wengi walitaka Majuma afukuzwe shule kabisa. Mwalimu Herman alijitahidi kwa uwezo wake kuwashawishi walimu hata kuomba msamaha kwa niaba ya Majuma ili tu asamehewe.

"Mimi ni mlezi wa chama cha YCS, mimi namfahamu Majuma vizuri….hizo tabia hana. Yeye anamtumikia Mungu kwa uwezo wake wote. Hawezi kufanya hivyo."

Mungu si athumani ile mipango ya kumfukuza shule ilifutwa. Majuma alifurahi japo alikuwa anaugulia maumivi makali sana ya fimbo. Majira ya saa moja usiku, Majuma na mwenzake walikuwa nyumbani. Kama kawaida hakukuwa na mazungumzo yoyote yale. Alivumilia na kushindwa hivyo aliamua kumvaa Fitina na maswali.

"Fitina nimekukosea nini? Umefanya nimeharibiwa usichana wangu bado hujaridhika umeamua kunizushia uongo shuleni….nimekukosea nini mimi?" aliuliza huku analia. Fitina hakujibu chochote.

"Nijibu, ubaya wangu kwako uko wapi kwako?"

"Majuma wewe ulitaka nipigwe, ulitaka nikatae ili nipigwe na walimu?" walizozana ilibakia kidogo kupigana. Miezi miwili ilipita huku amani ikitoweka kati ya Majuma na Fitina pale nyumbani. Kila mmoja alijua lake ikiwemo kujiandaa alivyojua mwenyewe dhidi ya mtihani wa kidato cha sita…maana ni miwili imebakia.

Siku moja wakiwa shuleni, ghafla kengele iligongwa. Ilikuwa saa tano asubuhi. Wanafunzi wote walikusanyika. Wavulana waliambiwa waendelee na majukumu mengine. Kidato cha tano nao waliambiwa vivyo hivyo wakati wasichana wa kidato cha sita walitakiwa kuingia kwenye chumba fulani. Hii ni siku ambayo haitawai sahulika na Majuma. Kule

ndani ya chumba walikuwa wanapimwa ujauzito. Majuma alikuwa na ujauzito wa miezi miwili.

Wale walimu waliokuwa wanataka Majuma afukuzwe walipata cha kusema. Minong'ono ilitambaa chini kwa chini mwisho shule nzima ikawa na hizi taarifa kwamba Majuma ni mjamzito. Licha ya Majuma kufahamu kuwa kuna siku alifanyiwa ukatili hakutegemea kama itakuwa hivyo. Alidhani ujauzito hauwezi kuingia ndani ya siku moja tena siku ya kwanza kushiriki tendo. Alipatwa na mshtuko mkubwa mno siku hii. Pale alipokaa alihisi anakuwa mwepesi kiasi cha kuweza kuruka. Alijiona anaelea hewani, mara kadhaa alijishtukia na kujitikisa ili akili ikae sawa. Maskini Majuma akili ilivurugika kabisa. Hakuwa na uhakika juu ya uhalisia wa haya aliyoambiwa. Alihisi ni ndoto na pengine baada ya muda ataamka kutoka usingizini.

"Majuma binti Saradibe anahitajika ofisini kwa mwalimu mkuu" alisema msichana mmoja wa kidato cha tano. Majuma alikuwa darasani kwani baada ya kupimwa waliingia darasani. Alisimama akiwa na hofu, miguu ilitetemeka kidogo amwangukie Hillary aliyekuwa amekaa meza iliyokuweko mbele yake.

"Kuwa makini bwege wewe. Fanya hivo uniangukie nikufinye."

Majuma hata hakusikia, alizama katika mawazo yaliyompeleka mbali sana. Alihisi kuchanganyikiwa maana hata ofisi yenyewe aliisahau. Aliingia kwenye staff office na kuwakuta baadhi ya walimu. Aliwasalimia lakini hawakumjibu chochote. Alitulia kwa sekunde kadhaa kisha akasema…

"Nimeambiwa mwalimu mkuu ameniita." Walimu walimshangaa.

"Umeanza kuchanganyikiwa wewe. Kwa hivyo ofisi ya mwalimu mkuu ni hii?" alisema mwalimu fulani wa kike. Jambo hili liliwafanya wote wacheke. Majuma alipatwa na aibu isiyoelezeka…kugeuka aondoke alishindwa, kusimama hapo hapo alishindwa…alibaki tu anahisi kama mahali alipokanyaga ardhi inanyanyuka, inashuka.

"Hebu toka! Pumbavu unachafua hali ya hewa." Ilikuwa ni kauli ya kuumiza lakini kwa Majuma ilimsaidia maana bila hiyo asingeweza kutoka pale. Alikutana na mwalimu Herman pale mlangoni.

"Majuma!!!" aliita kwa namna ya kushtuka hivi.

"Yes sir" alijibu akiwa kama hajiamini. Aibu ilitawala uso wake aliinamia chini.

"Unaelekea darasani?"

"Hapana mwalimu, naenda kwa mwalimu mkuu"

"Hebu ukitoka huko njoo unione" alisema mwalimu Herman na kuingia ofisini. Majuma alihisi kuchanganyikiwa Zaidi. Aliona mambo yanaanza kumlemea na kumzonga. Alijaribu kutuliza akili kidogo, ilipotulia alielekea ofisini kwa mkuu. Kufika tu alianza kushambuliwa kwa maneno kutoka kwa mkuu.

"Wewe ni msichana mjinga sana. Mnafanya tabia chafu huko, mambo ya kikubwa…mnajiona mmekuwa kupita sisi walimu wenu. Nimekuita muda mrefu tu ila unaanza kujivuta vuta kama mzee."Alifoka.

"Mkuu hata usiumize kichwa sana ngoja kwanza tumfundishe heshima kidogo" alisema mwalimu Rashid na kuchukua fimbo mbili zilizokuwa kwenye kona ya jengo la ofisi.

"Lala hapo!! Lala chini hapo." Alitoa amri mwalimu Rashid. Majuma alishangaa kusikia alichoambiwa maana kwa kawaida wasichana huwa wanapigwa mikononi na sio kwenye makalio kama wavulana.

"Usinipotezee muda lala hapo" alisema kwa hasira. Alimshika kisogo na kumuinamisha, bakora sita za nguvu zilitua mwilini mwa Majuma. Alilia mno, alitamani hata angekuwepo wa kumtetea lakini hakuwepo.

"Ndio muache kiburi, wapumbavu nyinyi. Mnaifanya shule ionekane danguro la makahaba na watu wasio na nidhamu.

Mnatudhalilisha. Haya inuka hapo" alisema mkuu aliyekuwa amechukia sana.

"Miezi miwili iliyopita tulikuuliza sana na uligoma kwelikweli haya huyo ujauzito umeshushiwa?" aliuliza mwalimu Bakora. Majuma hakuweza hata kuongea kwa sababu ya kilio.

"Unaulizwa huo ujauzito umeshushiwa? Haya mmeona walimu, niliwaambia huyu amekomaa katika mambo haya. Tunamuuliza hatujibu chochote ametulia na tumbo lake." Alisema madam Ruth. Walipoona Majuma hajibu chochote walimpiga sana kwa madai ana kiburi.

"Mimi sioni hata haja ya kuendelea kuongea kuhusu yeye, huyu ni wa kufukuzwa tu. Unafikiria atakaa darasani atulie na hio mimba? Hapa hakuna namna nyingine hata wakimtetea tena maana walimu wengine wapuuzi tu wanatetea ujinga na ushenzi." Alifoka mwalimu Bakora. Mwalimu mkuu alirudi mezani na kuanza kuandika barua.

"Nenda darasani tutakuita tukiwa tayari muda si mrefu"

Majuma alitoka huku analia. Alipiga hatua kadhaa baada ya kutoka ofisini ghafla alisikia sauti kali.

"Wewe si nilikuambia unione ukitoka huko?" Alikuwa mwalimu Herman. Ulikuwa mshtuko wa kipekee uliotambaa ndani ya mwili wa Majuma baada ya kusikia sauti ya mwalimu Herman. Alijitenga mahali fulani peke yake.

"Fanya haraka" Alionekana kuwa tofauti na kawaida yake. Alikuwa na hasira za mkisi, achilia mbali ule ukali aliokuwa anauonyesha. Hakika Majuma alishangaa na kuogopa sana leo hii. Alipiga hatua za haraka kufatia wito huku mkono wake wa kulia ukienda hadi usoni kufuta machozi yaliyokuwa yametapakaa.

"Twende ofisini" Mwalimu Herman aliamuru kisha aliongoza njia wakati huo Majuma akiwa nyuma yake. Wasiwasi mkubwa ulitanda utadhani ng'ombe anayepelekwa kichinjioni. Walifika ofisini, mwalimu alivuta kiti na kujituliza akiruhusu sekunde kama ishirini kupita pasipo

kusema chochote, Zaidi ya kujiinamia na kugonga gonga meza mithili ya mtu mwenye mawazo mengi….alikuwa anajaribu kuzichukua hasira zake na kuzipunguza. Ukimya ulitawala, baadae kidogo mwalimu aling'amua kinywa.

"Majuma!!"

"Yes sir!" aliitika huku anatetemeka

"Hivi unajua ni kiasi gani nilikuwa nakuamini wewe?" aliuliza lakini Majuma alibaki kimya maana aliulizwa swali rahisi lenye jibu ngumu. Hakujibu chochote.

"Majuma nilikuwa nakuamini sana. Nilikuona wewe ni msichana mwenye maadili ya kiungu, usiyependa mambo ya dunia. Hata hivyo kila ambaye alikuona sina shaka alipata kuiona hiyo picha nzuri" Alitulia kidogo na kutafakari kisha aliendelea.

"Niliiona hiyo picha tangu nilipohamia hapa, yani kila kitu chako kilidhihirisha uzuri. Ile siku wangeniuliza niwape sababu ya kukutetea nisingewapa ushahidi zaidi ya maneno ambayo mtu angehisi nadanganya lakini sikujali hilo" aliongea kwa msisitizo.

Majuma hakuwa na la kujibu, alibaki tu anasikiliza mambo anayosimuliwa na mwalimu. Mambo ambayo si mageni kwake kwani yalimuhusu yeye mwenyewe.

"Japokuwa walimu wenzangu walinipinga sana na kuona natetea uovu lakini sikujali kwa sababu nilikuwa na uhakika na ninachokisema. Nilikuwa na uhakika na utetezi wangu. Tazama sasa ulivyoingiza mchanga kwenye kitumbua. Kumbe yaliyokuwa yanaongelelewa ni kweli? Nilidhani najitutumua kukutetea kumbe najitutumua kujipaka matope! Hata sijui nitaificha wapi sura yangu. Walimu pia wataanza kuniona kama muhuni, wananitenga, kwa nini umefanya hivi Majuma!"

Ama kweli uchungu na maumivu hayachagui. Hukaa popote yanapopenda. Maumivu yalimshika mwalimu hadi akadondosha chozi mbele ya mwanafunzi wake tena wa kike.

"Wema wangu umeniponza, nilijitoa kukusaidia lakini kumbe nilikuwa namsaidia mchafu kunichafua, kwa kweli nimechafuka" alisema kwa uchungu na kuinamisha uso wake chini. Aliona haya kutoa machozi mbele ya mwanafunzi wake. Maneno ya mwalimu yalikuwa mithili ya msumari wa moto uliokuwa unachokonoa chokonoa kuta za moyo wa Majuma…aliumia zaidi. Aliona ni heri aseme ukweli ili ufahamike japo haungesaidia chochote kwa sasa.

"Mwalimu naomba unisamehe kwanza, pia naomba unisikilize. Haya yote amesababisha rafiki yangu Fitina…" alipotaka kuendelea alikatishwa na sauti ya mwalimu.

"Nenda darasani, nikikuhitaji au niwe na shida na wewe nitakuita" alisema akiwa amejiinamia vile vile. Majuma alidhani amepata nafasi ya kueleza ukweli wake aliouficha siku zote lakini nafasi nayo ilikimbia. Aliganda, hajui aondoke au ajaribu kumuomba aongee naye ili amueleze.

"Mwal…mwalimu..., Tafa..." aliita.

"Nimesema nenda darasani" alisema na kuinua uso wake uliojaa hasira, macho yalikuwa mekundu mno hadi Majuma aliogopa. Alitoka haraka na kwenda darasani. Minong'ono ya hapa na pale ilisikika mle darasani, alipoingia tu minong'ono yote ilipotea. Alitambua hiyo minong'ono ilimuhusu yeye lakini hakujali sana alielekea hadi kwenye meza yake na kujiinamia huku kizunguzungu kikipigana vita vikali na ubongo wake. Hata hakupata muda wa kupumzika ghafla alisikia kengele ikigongwa. Ilikuwa kengele ya dharura. Maneno ya mwanafunzi mwenzake yalisikika waziwazi. Maneno ambayo mwanzo yalikuwa minong'ono

"Ohooo mambo ishakuwa tayari huko. Ni wakati wa mtu kufinywa, hatunaye tenaa"

"Shule ilimpenda lakini dunia imempenda zaidi" alitamka hayo mwanafunzi mwingine wa kiume, alipita haraka karibu na Majuma na kumpiga kikumbo. Majuma alipepesuka karibu aanguke. Wanafunzi wote

walikuwa katika mstari ulionyooka. Walimu walianza kutoka ofisini na kujaa pale kwenye uwanja wa kukusanyikia. Walikuwepo walimu wote ndani ya eneo hilo isipokuwa mwalimu Herman ambaye alijitenga mbali. Mkuu hakutaka kuzunguka wala kuzungumza sana.

"Wanafunzi tumewaita hapa kwa lengoo moja tu. Tunataka mjifunze kuwa hata ukibakisha wiki moja tu kufanya mtihani tutakutimua ukileta ujinga. Kuna mpumbavu mmoja amekutwa na kesi ya kinidhamu. Sasa hili haliitaji kuita wazazi wala kuhojiana chochote na mtu yeyote yule. Huyu Majuma binti Saradibe tunamfukuza shule moja kwa moja maana hata ushahidi wa ujauzito anao hivyo kuanzia leo si mwanafunzi wa Kijiweni tena"

Majuma nguvu zilimuisha, hakuamini alichokisikia. Hapo hapo aliitwa kuchukua barua kwenda kuwapa wazazi wake ili pia nao wajue.

"Haya funga virago vyako ondoka. Wasalimie huko Kakamega. Ukifika waambie wakupe ugali na *ingokho"* alikuwa mwalimu Bakora.

Alirudi pale wanapoishi na mwenzake Fitina. Muda wote alijilia na kuhisi kwamba ulikuwa mwiba wa kujidunga kwani aliuchagua yeye. Hakuamini kama yaliyomkuta ni ya kweli au ni ndoto maana upo wakati alielea katika bahari ya kusahau yaliyokuwa yakiendelea alifikiria safari ya Nakuru kwenda Kakamega. Alikosa Amani kabisa na kila alipojiuliza swali kuwa ataenda kuwaambia nini wazazi wake? Nguvu zilimuisha. Atawaambia nini wazazi wake waliojitoa kwa hali na mali kuhakikisha wanampa mtoto wao wa pekee kila alichohitaji ili tu asome kwa bidii? Ataenda kumwambia nini mama yake ambaye kila mara amekuwa akimsisitiza kujitunza?

"Mungu kwa nini umeruhusu hili litokee kwangu?" Majuma alilia sana

Hadi kufikia sasa Majuma aliona dunia ni nzito na imemlemea mno. Hakujua kwa nini haya yanamtokea wakati aliishi kunitunza kama mboni ya jicho lake. Aliona dunia ikimkana na kutaka kummeza mzima mzima.

Alihisi meno ya dunia yalikuwa wazi kama ya ngiri na tayari kumng'ata na kumwadhibu kwa kucha zake. Alishangaa mbona dunia ilikuwa imebadilika kiasi Kile kwani yule mtu mwenye kufanya mabaya siku zote yuko salama na hapatwi na masaibu kama haya, lakini yeye ambaye daima huenda katika njia za kumpendeza Mungu amekutana na mabaya.

Uchovu kutokana na kulia uliingia mwilini mwake. Aliamua kutulia ili apumzike kwanza. Haikuwa kazi rahisi kujituliza kutoka kwenye ile hali ya kusalitiwa na kukataliwa na ulimwengu wote, kwa jitihada zake za kujisahulisha hatimaye kilio kilikatika kabisa, alikuwa amekaa chini huku mgongo wake ukiwa umeegemea kwenye kitanda. Alitembeza macho huku na huku lengo tu kuepusha macho yake kuganda sehemu moja hatimaye akaanza kupata mawazo tena. Akili ya kuimba nyimbo fulani fulani ilimjia, alihitaji kuimba ili ajichangamshe lakini ukweli huo uwezo wa kuimba hakuwa nao. Hata alipojaribu kukumbuka nyimbo za kuimba, zilimjia nyimbo zilizobeba huzuni isiyo kifani. Aliamua kuacha na kusimama labda akatembee tembee nje kupoteza mawazo. Aliposimama alihisi maumivu makali mwilini nalo tumbo kuvuta. Alilishika na kulitazama, alipolitazama tu akili ilimwambia.

“Hili ndilo tumbo lililobeba mimba.”

Alishtuka ungedhani ilikuwa sauti ya mtu iliyomwambia haya. Maskini Majuma, alirudi katika huzuni na kilio ambacho kilitulia kwa muda. Alilia sana, yani hakuamini kama amebeba ujauzito, ujauzito uliomuondoa katika maisha ya shule.

“Ina maana mimi sio mwanafunzi tena!! Aaah!!” Hakuamini kama yupo katika maandalizi ya kuitwa mama wa mtoto. Vipi kuhusu baba wa mtoto?? Hamjui labda kwa sura tena kwa mbali. Hii siku ya Ijumaa ilipita akiwa hajui aanzie wapi kwa kutoka na kwenda nyumbani Kakamega. Jumamosi nayo ilipita. Kiukweli pale ndani walikuwa wanaishi kama maadui, chuki ilitawala kati ya Majuma na Fitina. Jambo kidogo tu walizozana.

"Ni heri tu uondoke, unanijazia nyumba bure. Unasubiri nini?" hii ilikuwa kauli ya kila mara kutoka kwa Fitina.

"huwezi kuniamuru hivo kirahisi rahisi shetani wewe"

"mimi shetani?"

"Yeah, tena wa mguu mmoja"

Fitina alimrarua mwenzake kofi zito.

"Na bado hautaamini nitakachokufanyia! Wewe ngoja uone." Fitina alisema tena kwa hasira.

Majuma alikuwa anaumia kila sekunde kila dakika, alikosa roho kwa kweli. Siku ya Jumapili ilifika na ilipita hata kanisani hakuenda maana alihisi nguvu ya kwenda huko haipo. Kila alipokumbuka yaliyomtokea aliona kama Mungu amemuonea, hakwenda kanisani. Kuhusu kula alikula kidogo sana jambo ambalo lilifanya afya yake kudhoofika mno ndani ya hizo siku tatu. Ilikuwa Jumatatu sasa, aliamka hajui afanye nini na aende wapi. Pa kwenda ni Kakamega ila angeanzaje???

Majira ya saa tano asubuhi akiwa hapo nyumbani ghafla alisikia mlango unagongwa. Hakujua ni nani ndio maana hakutaka kujibu haraka. "Ngo ngo ngo!" Yule mtu aligonga kwa mara nyingine tena, hakutaka kutoa sauti yake alikuwa anagonga tu. Aliamua kunyanyuka na kwenda kufungua mlango. Alikutana uso kwa uso na Fitina aliyekuwa pamoja na walimu wawili.

"Yani wewe msichana tumekufukuza uende kwenu lakini bado umeng'ang'ania hapa. Unamsumbua mwenzako hapati muda na raha ya kujisomea maana anasema muda wote wewe ni kuingiza tu wanaume."

"Ndio ukweli huo mwalimu nashindwa hata kusoma maana mwenzangu hajali wala haogopi kuleta watu wake. Mbaya zaidi anataka mimi nifanye upuuzi anaofanya" alisema huku anatoa chozi. Walimu waliamini.

"Kweli mtu aliyezoea mambo yake huwezi kumbadilisha, yani licha ya ujauzito bado huachi wanaume. Ama kweli umeshindikana," huyu alikuwa yule yule mwalimu Bakora.

"Tena usitake kumharibu mwanafunzi wetu. Andaa virago vyako uende."

Sasa Fitina alihitajika kuingia ndani kuchukua kila kilicho cha Majuma akitoe nje. Alifanya hivyo kisha mlango ulifungwa.

"Kwa usalama wako ondoka tu." Alisema mwalimu Bakora kisha wao waliondoka na kumuacha Majuma peke yake pale. Hata nauli hakuwa nayo hivyo hakujua anaondokaje. Akiwa hapo ghafla alikumbuka kitu. Alikumbuka ile siku alipewa elfu kumi na Fitina. Alitafuta sana kwenye begi lake mwisho aliipata. Alisimama na kuanza kutembea pole pole.

"Nyumbani siendi, bora nipotee. Naenda kokote ninakokujua mimi," alijisemea huku analia, wakati huo begi lake lipo kichwani.

"Nyumbani siendi" hii ilikuwa kauli aliyoitamka mara kwa mara. Nayo haikuacha kuzunguka ndani ya akili yake. Alishajiamulia kutokwenda nyumbani yani ni heri akafie tu kusikojulikana kuliko kwenda nyumbani maana alijua ni balaa gani litatokea. Hisia zake zilijinjenga juu ya namna mambo yatakavyokuwa mazito akirudi nyumbani. Alitembea akiwa na begi lake hajui ni wapi anaenda cha msingi alitembea ili apotee hapo. Alizunguka huku jua nalo likiendelea kumhukumu. Mwili ulilowa jasho kutokana na joto lile lililomsumbua mno. Aliamua kujituliza mahali fulani penye kivuli. Pembeni alikuwepo jamaa moja muuza juisi na *ice cream* bila shaka maji yalikuwa miongoni mwa zile bidhaa zake.

"Oya bro! Nisaidie juisi ya maembe na iwe baradi tafadhali."

"Poa siste, haina noma, unataka ya *mbaula* au ya *chwani*?" alisema huku akisimama kumhudumia mteja wake.

"Hebu nipe hiyo ya hamsini" alijibu kisha akapewa.

Majuma alichukua pesa na kumpa muuzaji kisha akarudishiwa salio. Chenji ilikuwa shilingi mia tisa hamsini.

"Hii itanisaidia" alisema na kuiweka ndani ya braa yake kifuani. Hakutaka kuweka kwenye begi. Baada ya kunywa juisi yake tupu alijihisi afueni hata mwili uliacha kuchemka. Alipumzika kidogo kisha alinyanyuka kwa mara nyingine akitembea hapa na pale huku akitafakari juu ya mahali pa kwenda. Alitembea kwa mguu kutoka maeneo ya karibu na mahali ilipokuwa shule ya kijiweni akapita maeneo yote hadi kwa stendi ya magari yaendayo masafa mafupi. Alifika hapa ikiwa ni saa tisa alasiri maana alitembea kwa mguu umbali mrefu. Hapo stendi aliumiza kichwa asijue apande gari za wapi maana kituo hiki gari zake huzunguka hapo hapo Nakuru…hazitoki nje. Alifikiria ila mwishoe aliona hapa hapamfai. Aliamua kutembea tena kutoka kituo hicho kuelekea kwa kituo cha mabasi yaendayo mikoani. Hiki kituo kinaitwa *Travellers.* Bado hakuwa tayari kupanda gari, aliamua kutembea hadi *Travellers.* Saa tisa na nusu alifika akiwa hoi bin taabani. Alichoka kweli kweli.

"Siste radah! Unaenda *Nairobary*?" aliuliza mpiga debe

"Hapana"

"Unaenda wapi rembo, kama unaenda Nai gari ni hii tu."

"Nimesema siendi Nairobi" Majuma alikuwa mkali. Aliingia ndani ya stendi na kukaa kwenye benchi pale. Bado akili yake haikumueleza mahali pa kuenda.

"Msupa Kakamega *direct* hapa, au unaenda Bungoma??" alikuwa mpiga debe mwingine. Majuma hakujibu chochote. Aliamua kujiinamia nayo machozi yalikosa adabu…yalianza kuuchafua uso wake. Yani hadi hapo bado hakuamini kama kweli yaliyomtokea ni halisi ama ni maigizo au ndoto. Aliumia sana na hakujua ni ipi hatima ya maisha yake. Alikiona kifo kikiwa karibu naye hasa akirudi nyumbani Kakamega.

"Naenda Nairobi" alitoa uamuzi na kujifuta machozi, alimgeukia msichana aliyekuwa amekaa kushoto kwake kwenye benchi lile. "Dada

naomba nikuulize kidogo, kutoka hapa hadi Nairobi ni shilingi ngapi?"

"Ni masaa mangapi kufika?" aliuliza tena.

"Inategemea na gari lenyewe gari litatembea bila shida yoyote ni masaa manee au matatu hivi."

" Asante, nimeshukuru sana"

"Kwani unaenda Nairobi?" yule mwanadada aliuliza

"Hapana, nimekuuliza tu" Majuma alificha.

Aliangalia saa yake, ilikuwa saa kumi kasoro. Safari ya masaa matatu kwa makadirio atafika majira ya saa moja usiku Nai. Kwenda ugenini na kufika usiku!!!! Utapokelewa na nani? Majuma alitafakari sana mwisho aliona ni lazima aende Nairobi lakini sio siku hiyo kwani angefika usiku halafu ingekuwa shida nyingine. Alichoona ni cha muhimu ni kulala Nakuru siku hiyo kisha kesho yake mapema akate tikiti ya gari za asubuhi aondoke. Kuhusu mahali pa kulala hakuona shida wala hakuwaza. Aliamini popote ni kambi hata palepale stendi.

Majira ya saa tano usiku alijitaftia kakona na kujichomeka ili kuuchapa usingizi uliokuwa umeanza kumnyemelea kutokana na uchovu wa siku hiyo. Begi lake lililokuwa na nguo nyingi alilitupia kichwani kama mto kisha muda mfupi usingizi ulimpitia licha ya baridi lililomsakama na mbu waliokuwa wanajitahidi kunyonya damu yake. Mida ya asubuhi alishtuka kutokana na sauti ya kiume iliyokuwa inamuamsha. Alichukia sana kile kitendo, kwani alitaka aendelee kuufaidi usingizi ule. Alipoamuka alishangaa kuona kumekucha na kweupee kabisa. Kuangalia saa yake ni saa mbili asubuhi.

"Heee!" Alishtuka na kuinuka haraka ili aende akate tiketi mapema. Pengine kutokana na wenge la usingizi alitaka kuondoka na kuacha mzigo wake. Alipiga hatua mbili ndipo alipokumbuka….

"Oooh!! Nimeacha begi" alirudi nyuma kuchukua lakini cha ajabu begi halikuwepo hata ushahidi wa begi haukuwepo.

"Mama yangu, begi langu limeibwa" aliongea kwa presha na kupumua kwa hofu huku mapigo ya moyo yakidunda kwa kasi kubwa. Mikono yake ilishika kichwa, haamini anachokiona. Kilio juu ya kilio.

Hili halijaisha limezaliwa lingine lenye uzito unaokaribiana na la mwanzo. Furaha iliyeyuka kama barafu juani, huzuni ukatanda na kuufunika moyo wa Majuma aliyekuwa amepoteza nguvu ya kukishinda kilio. Alilia kweli kweli bila kujali watu waliokuwepo eneo lile. Hata watu wenyewe hawakuwa na muda naye, ni wachache tu ndio waliojaribu kusongea na kutaka kujua ni kipi kimemkuta mtoto wa watu. Walimzunguka kama wafanyavyo waandishi wa habari, kila mmoja akihoji kwa namna aliyoijua yeye mwenyewe.

"Siste, kuna nini, mbona unalia?" aliuliza kijana mmoja.

"Twambie bana, tunaeza kukusaidia" alikuwa kijana wa pili.

"Una ndugu yako au mtu wa familia amekufa?" aliuliza mwingine. Wote walikuwa wanaume, hakuwepo mwanamke hata mmoja. Majuma aliona aibu kuelezea kilichomkuta ila ushawishi wa hawa watu ulimwaminisha kuwa anaweza pata msaada.

"Nimeibiwa" alisema huku analia.

"Umeibiwa nini?"

"Nimeibiwa begi langu, lilikuwa na nguo na vitu vyangu vyote. Hata pesa zilikuwa ndani" alieleza huku akionekana kuchanganyikiwa sana maana hadi alisahau kuwa kuna pesa aliweka kwa bra…mia tisa hamsini.

"Mmmsyuuu!!" alisonya mmoja na kuondoka baada ya kusikia hayo. Mwingine alicheka na kumkejeli.

"Dada acha ushamba, hapa sio *Shimalabantu* kijijini, hapa ni Naks bana." Alisema na kuondoka zake. Huku nyuma kilio kiliongezeka kwa Majuma. Yani amepatwa na masahibu lakini mtu wa kumfariji hakuna. Watu walimpita kama hawamuoni, na waliomsogelea ndo hao

wanamcheka na kumdhihaki. Alibaki mpweke na mkiwa asiye na namna ya kufanya Zaidi ya kujiinamia chini na kuanza kupoza machungu ya moyo kwa kilio Zaidi.

Aliona dunia imemtenga, tena ghafla. Hakujua ni kwa nini dunia imemtenga kiasi hicho, hakujua ni wapi amekosea. Pengine angejua angetubu kwa nguvu zake zote. Akiwa pale chini muda mwingine alipitapita kijana fulani aliyeonekana mpiga debe, kwa sababu mara nyingi alionekana akiwakimbilia abiria na kuwauliza.

"Bro unaenda Kisumu? Vipi, unaenda Kakamega?" hii ilikuwa kauli aliyokuwa anaitamka kila mara alipomuona msafiri. Huyu kijana alipomuona msichana aliyejiinamia analia alishtuka sana, alimsongelea na kuanza kumhoji.

"Mrembo, una shida gani, mbona unalia?" aliuliza lakini Majuma hakujibu akiogopa kufanya makosa ya mara ya kwanza na kuchekwa tena.

"Naomba niambie, huenda nikawa wa msaada kwako. Sisi wote ni binadamu, niambie." Alimshawishi sana na mwisho Majuma alimweleza yote yaliyomkuta siku hiyo. Yule kijana aliumia.

"Kwani nyumbani ni wapi?"

"Kakamega" Majuma alijibu

"Si unaenda huko"

"Ndio" alijibu na kusahau kabisa kama alipanga kwenda Nairobi. Alichanganyikiwa.

"Ok basi njoo huku, usijali utafika nyumbani, ngoja nikakufanyie mpango. Nifuate huku" alisema yule *manamba*. Majuma alikuwa nyuma anamfuata hata hivyo alikumbuka kuwa alipanga kwenda Nairobi, ameshasema kuwa anaenda Kakamega, alishinda kubadilisha kauli, hakuwa na namna. Alifanyiwa mpango ya usafiri kisha akatakiwa kila la kheri.

"Safari njema mamangu"

"Nashukuru sana, umenisaidia sana hata sijui nikushukuru vipi"

"Usijali, kama nilivyosema mwanzo, sisi ni binadamu, kwa hivyo tunapaswa kusaidiana."

"Labda kama sijaenda naomba nijue jina lako" Majuma alidadizi.

"Mi naitwa Abdul, ni mzaliwa wa Kakamega pia sehemu inaitwa *Samitsi."* Alijieleza yule mpiga debe.

"Aah, kwa hivyo wewe ni *Mkabaras*?"

"Yes, huku nipo tu kujiitaftia. Na wewe? Pia ni vizuri nikujue." Abdul aliuliza.

"Mimi naitwa Majuma, nyumbani ni Kakamega kama nilivyokwambia mwanzo, sehemu panaitwa *Munduma*, sijui kama unapajua?" hapo gari lilikuwa tayari kuondoka, kwa hivyo alitakiwa kupanda ili aende.

"Ingia kwa gari, lisije likakuacha"

Alipanda basi la kampuni ya *Eldoret Express* lililokuwa linatoka hapo Nakuru mida ya asubuhi kuelekea Kakamega. Ndani ya safari alikuwa na mawazo sana, hakujua ataenda kusema nini nyumbani na ni nini kitatokea. Hakujua nani atamuelewa pindi atakapoanza kujitetea akijaribu kueleza ukweli. Alilitazama tumbo lake na kuanza kulia. Kwa kawaida safari ya Nakuru hadi Kakamega hutumia masaa manee au hadi tano kwa hivyo mida ya saa nane alishuka kituo kiitwacho *Total* na kilichobaki ilikuwa ni kuchukua boda boda wa pikipiki aelekee nyumbani ambapo ni umbali wa kilomita tatu kufika kijijini kwao Munduma. Ilikuwa ngumu kufikia uamuzi wa kwenda nyumbani ila angefanyaje?? Aliona ni heri arudi nyumbani, chochote kitakachotokea na kitokee. Alipata mshtuko alipokumbuka kuwa hata hiyo nauli ya kumfikisha kwao hakuwa nayo. Hakujua ataendaje ila alipotulia kwa sekunde akili ilimtuma kujichunguza kwenye bra. Alishangaa kukutana na shilingi mia tisa hamsini. Alimshukuru Mungu kwa hili na hakutaka kupoteza muda sana, alipanda boda boda na kuelekea nyumbani Munduma.

# SURA YA TATU

Majuma aliwasili nyumbani Munduma saa tisa kamili. Alitembea kwa masafa machache kutoka kituo cha pikipiki ambapo teksi ilimfikisha. Alipatwa na hofu njisi ya kukabiliana na wavyele wake ambao walijituma ili mwanao wa pekee apate elimu ambayo ni msingi wa maisha bora. Wakati mwingine, alitetemeka kama kifaranga nao mwili ukapatwa na kibibi.

Baada ya kufika karibu na lango lao kwa wasiwasi na hofu, alijibana mahali fulani na kuchungulia nyumbani. Hata hivyo, alishangaa kuona harakati zikiwa nyingi pale nyumbani kwani chumba kilikuwa kimejaa pomoni na kutapika baadhi ya watu nje ya nyumba. Majuma hakujua ni nini kilichokuwa kinaendelea kwani jambo usilolijua ni usiku wa giza totoro!

Hali ilivyokuwa pale nyumbani ilionyesha kulikuwepo na jambo. Kisha mkusanyiko wa watu kwa vikundi vikundi ikawa si jambo tu bali mambo makubwa makubwa. Wengi wa watu walikuwa wazee. Ni nani asiyejua kuwa palipo wazee hapakosi jambo? Kwake aliona kama ya mgambo ilikuwa imelia. Ujio wa watu pale nyumbani kwao ulimtisha na kumpa wasiwasi mkubwa. Hakujua ni nini kinaendelea pale. Hakutamani iwe kama hisia zake zilivyomuelekeza. Alitamani ampate mtu wa kumuuliza ili apate uhakika zaidi kuliko kuendelea kuaminianachokisihisia. Huyo mtu wa kumuuliza hakupatikana kwa hivyo njia pekee iliyobaki ni kwenda tu nyumbani. Angeanzia wapi? Alishindwa kujua ni kwa namna gani atanyanyua mguu wake na kuutua kwenye uwanja wa kwao.

Akiwa amejificha mbali na pale kwao, ghafla alipita mtoto mmoja, alikuwa anaenda kulekule.

"Wewe, njoo kwanza, wewe!!" Majuma aliita, yule kijana mdogo hakujibu chochote, aligeuka na kumtazama Majuma.

"Njoo kwanza" aliita tena.

"Unaelekea wapi mdogo wangu?" aliuliza bila maneno mengi.

"Naenda pale" alijibu kwa kunyoosha kidole kuelekea anakoenda. Ni nyumbani kwa akina Majuma.

"Ahaa, kwani watu wanafanya nini pale?"

"Wale walimbeba mzee anayeishi pale, alianguka alipoenda shambani" yule kijana mdogo alisema.

Majuma hakutaka kuuliza maswali zaidi, angalau ameshaelewa japo undani wa hili suala bado hakuufahamu. Hata hivyo alipata afueni kidogo kwani yeye alihisi kuna jambo mbaya zaidi. Alimruhusu yule mtoto kuondoka, naye alijtoa mhanga, liwalo na liwe. Aliamua kupiga hatua kufika nyumbani. Hofu ilikuwa kubwa, alitetemeka mwili hadi moyo.

Macho ya wachache yalishamuona na katika hao hakuna hata mmoja ambaye hakushangaa kumuona. Kila mmoja alimshangaa kwa jambo lake. Wapo walioshangaa kumuona kipindi ambacho si cha likizo.

"Je, amerudi kwa sababu ya ugonjwa wa baba yake? Na kama ni hivo, ndio arudi bila chochote? Hata begi!!?"

Wengine walimshangaa alivyobadilika rangi ya ngozi na kuwa mweupe kutokana na mazingira ya Nakuru. Aliwasalimia huku akishuhudia wazi wazi dukuduku lililotawala usoni mwao. Hakushughulika nao sana, alipiga hatua kuelekea ndani. Haukuwa mshtuko wa kawaida kwa mama yake baada ya kumuona Majuma hapo. Hakuwa na hakika kama waliwasiliana hapo nyuma na kupeana ahadi za kurudi. Hakuwa na uhakika.

"Hee, Majuma kuna nini tena!!? Mama alishangaa, aliuliza kwa pupa hata bila ya salamu wala kujali watu waliokuwepo hapo nyumbani. Majuma hakujibu chochote kwa sababu majibu yalikosekana kabisa

ukichanganya na mhemuko aliounyesha mama yake. Kumbe hata mzee Saradibe alisikia. Alisikia habari za uwepo wa Majuma hapo nyumbani.

“Niitie mama Majuma” aliongea kiugumu ugumu maana alikuwa amedhohofika sana. Mkewe aliitwa na muda si mrefu aliingia chumbani.

“Nimesikia unaongea na mwanao” alisema mzee Saradibe na kukohoa kwa nguvu.

“Tena nashangaa kumuona amerudi, sijui nini kimemkuta huko maana hata begi lenyewe hana” alisema mama Majuma mwenye mazoea ya kuongea kwa sauti kubwa, usiombe kugombana naye.

“Labda amesikia unavyoumwa." Alisema Shaban. Kijana ambaye alishughulika katika kumbeba mzee Saradibe.

“Ah! Sidhani na hata kama ndo hivyo sasa ndio arudi bila begi? Arudi bila kutoa taarifa? Na kwanza kuhusu kuumwa yeye amefahamu lini? Yani mzee aumwe leo naye arudi leo? Hapana!” Mama Majuma alihoji maswali ya msingi.

Wote waliguna na kuumiza vichwa kwa maswali haya. Kwa kuwa mhusika yupo, basi walionelea hakuna haja ya kuandikia mate ilhali wino upo, waliamua kumuuliza yeye mwenyewe.

“Mama naona umerudi ghafla hata bila taarifa, kuna nini? Au umerudi likizo?” aliuliza mama Majuma na kukaa kitandani alimolala mzee. Majuma alikosa cha kujibu. Alifikiria kidogo kisha alisema.

“Ndio nimerudi likizo” alijibu bila kujua kwamba ameharibu kabisa kusema hivyo.

“Mwezi wa tatu, likizo gani hasa kwenu nyinyi, kidato cha mtihani?” alihoji mjomba wake aliyeitwa Lumasayi. Majuma alibaki kung’ata vidole.

“Yani hata kudanganya huwezi Majuma, jibu lako ni la uongo pia hata muonekano wako unakusaliti tu. Hebu tuambie ni nini kimekukuta hadi ukarudi tena bila begi” mjomba alifoka.

“Enhee, begi liko wapi?” alidakia mama mtu

"Nim…nimei…biw..a"

"Umeibiwa wakati gani?" aliuliza mjomba Lumasayi

"Wakati nakuja"

"Haya mmeona? Ina maana alijiandaa kabisa kwa safari. Na tukumbuke hii sio likizo, ni lazima kuna jambo si bure, naomba atuambie kuna nini"

Sasa hata mgonjwa alisahulika, maswali yalikuwa mengi kwa Majuma. Majuma alishindwa hata kunyanyua kichwa kwa wakati huu. Haikuwa rahisi kusema ukweli ambao hata hivyo ulianza kuhisiwa. Hisia za ukweli huo zilisindikizwa na macho ya uchunguzi wa kitaalamu uliojaa uzoefu. Macho ya mama yake yalishagundua mabadiliko katika mwili wa mwanae.

"Majuma wewe ni mjamzito. L" Majuma alishtuka asijue mama yake amejuaje. Hakufahamu kama mama yake ni mzoefu na ana maarifa makubwa katika mambo haya. Lilikuwa jambo la kushtukiza kwa wote. Haikuwa rahisi kuamini ila kilio cha Majuma kilianza kuwapa nguvu ya kuamini kuwa ni kweli.

Baada ya kubanwa sana Majuma alifunguka na kueleza ukweli uliopo.

"Nimefukuzwa shule kwa sababu ya uja-zi-to" alisema huku akilia. Mshtuko mkubwa ulijaa mle ndani. Mama yake kidogo aanguke kutokana na taarifa hii, wakati huo mzee Saradibe ambaye alikuwa kitandani kwa sababu ya presha iliyomvamia tangu siku chache za nyuma, yeye hali ikawa mbaya zaidi. Pumzi iligoma kutoka kwa dakika kadhaa. Alishindwa kupata afueni na itoshe kusema mzee hakuwa na nafasi tena ya kuishi. Alikata roho palepale. Tatizo la presha na kifafa ndio lilikuwa limemwangusha akiwa shambani, sasa wakati huu si kumwangusha tena bali tatizo limechukua uhai wake.

"Majuma Majumaaa!!, kwa upumbavu wako umemuua baba yako. Umeniulia mume wangu!" alilia kwa uchungu mama Majuma.

Unyende wa mama Majuma ulizua gumzo kwa watu wa kijiji cha Munduma hasa wale waliokuwa karibu na pale nyumbani. Muda mchache tu watu wengi walifika na kujumuika na wale waliokuwepo mahali hapo tangu awali.

“Kuna nini tena, mbona makelele? " Alihoji mama mmoja aliyekuwa anakuja mbio mbio huku anafunga vizuri kanga yake kiunoni.

“Labda mzee ametuacha”

“Ngoja tukaone huko huko”

Watu walikuwa wengi na kila mmoja alikuwa anahoji lake.

“Oooh!!! Nitafanyaje sasa mimi. Majuma unaona sasa upumbavu wako, unaona sasa?” alifoka na kumfuata Majuma kwa hasira. “paaaaah!” Majuma alipigwa kofi hadi alipata kizunguzungu. Hakukaa sawa aliongezewa lingine hadi akaanguka. Ilibidi Lumasayi mjomba wa Majuma kuja kuingilia kati la sivyo Majuma angeumizwa.

Wakati huo kule nje baada ya kuulizana ulizana watu wale walielewa ni nini kinaendelea pale.

“Hivi ndivyo ilivyo mitoto ya siku hizi yani mambo ya ajabu, ona sasa amesababisha kifo cha mzee.

“Alafu ukiwaambia ni wabishi wanajifanya wanaelewa kila kitu kuliko wakubwa wao. Madhara yake ndio haya sasa” walinong’ona akina mama fulani waliokuwepo hapo, pembeni kidogo.

“Na amepata hasara kubwa kweli, ana ujauzito, kafukuzwa shule, na pia amempoteza baba yake. Ndio wajifunze wapuuzi hawa. Amemuua mzee wa watu” minong’ono iliendelea kusikika.

“Kusema ya kwamba huyu msichana amemuua mzee mimi hapo kidogo napinga kwa sababu mama yake ndio wa makosa. Alijua fika hali ya mzee ilivyo alafu anapayuka payuka taarifa za kushtua, alitarajia nini?” alihoji bwana Kombo.

“Ni kweli lakini chanzo cha yote haya ni nini?”

"Chanzo ni Majuma sikatai, lakini mama yake ndo ana tatizo. Amekosa nguvu za kutawala mihemko yake na kutatua tatizo"

Hakika minong'ono ilikuwa mingi sana. Kila mmoja akijaribu kuelezea hali halisi.

Ni siku nyingine tena, siku hii ilipangwa kuwa ya mazishi ya marehemu mzee Saradibe. Watu walikuwa wengi msibani. Walikuwa wengi kutokana na umaarufu aliokuwa nao. Ilikuwa ngumu kuamini kama kweli mzee Saradibe amefariki. Wale wenye tabia ya kulaumu bila kujua ukweli wa tukio walilaumu mno. Lawama kubwa zilienda kwa Majuma.

Majuma alitamani akimbie aondoke na aende mbali ila kibinadamu na kiustaarabu aliona si vyema kutomzika baba yake. Hivyo aliamua kuhudhuria msibani. Muda wote macho ya watu wengi yalikuwa juu yake hadi akaona aibu. Watu walimuona kama jasusi aliyemuua baba yake. Mama Majuma hakufanikiwa kumuona tangu jana alipompiga, sasa balaa lilikuwa pale mama yake alipomuona.

"Wewe shetani sitaki nikuoneee, umemuua sasa unataka nini? Unataka kumla nyama? Sihitaji kukuona mwana haramu wewe" mama alifoka sana. Majuma aliona aibu mno. Hakuamini anayoyasikia kutoka kwa mama yake.

Kwa woga aliamua kusogea pembeni huku analia.

"Mungu wangu kwani ni wapi nilikukosea? Ni kipi nimekifanya hujakipenda? Je, ni kuishi maisha yanayokupendeza? Au ni kwenda kanisani kila mara? Kama si hivyo kwa nini umeamua kuniadhibu kiasi hiki baba? Kosa langu ni lipi, Mungu mbona umeniacha mimi" Majuma alilia machozi.

"Mnafiki huyo anajifanya analia wakati yeye ndiye kamuua baba yake" yalikuwa maneno ya watu. Watu wote walimsema. Aliona dunia inamzonga zonga na kuegemea upande wake. Hakuwa na namna ya

kufanya, ilibidi aondoke na kuenda mbali na hapo maana kubaki hapo isingewezekana.

Mzee alizikwa na ilipofika jioni watu walitawanyika. Majuma alikuwa mtaani anazungukazunguka kama mbwakoko asijue ni wapi pa kuenda. Muda nao si rafiki kabisa, majira yalisonga na hatimaye usiku uliingia. Mawazo mawili yaliingia akilini mwa Majuma, arudi nyumbani japo alijua fika kwamba kuna changamoto. Wazo la pili ni kununua sumu anywe maana uhai wake ushakuwa mzigo kwake. Hata hivyo alipojipapasa mahali alipokuwa amehifadhi pesa zake hakuziona. Si haba alichanganyikiwa mara baada ya kugundua hela zake hazipo. Alijipapasa sehemu mbali mbali hata sehemu ambazo hakuweka alijipapasa huku akiamini pengine atazipata.

Kilio na machozi ndivyo vitu pekee vilivyodhihirisha uchungu uliogubika moyo wake kwake vilikuwepo na havikumsaliti. Alilia kwa uchungu mkubwa huku akimhoji Mungu wake mambo yale yale ya kila siku kwa kuruhusu shida zote hizo kumng'ang'ania yeye tu. Kila kitu alikiona kinaenda mrama na kuacha njia sahihi ili mambo yawe sawa. Majuma aliona kama sauti ya kilio chake haisikiki kwenye masikio ya muumba wake na pengine hata machozi yake ya kila uchao hayakumfikia Mungu wake. Alihisi Mungu amemgeuzia kisogo.

Miguu ilikosa nguvu, alishuka hadi chini huku machozi yakiendelea kuuchafua uso wake. Kila lililoingia katika kumbukumbu yake lilimtesa na kumfanya aongeze kasi ya kulia. Alikumbuka yote hadi yaliyotokea hivi karibuni; Si kusingiziwa kuua babake, si kufukuzwa na mamaye nyumbani, si kuibiwa begi mjini Nakuru, si kufukuzwa na walimu shuleni, si kusalitiwa na rafikiye wa karibu Fitina, si kubakwa na janadume lile. Si kupoteza pesa na hapo alipo ni mtaani. Majuma alichanganyikiwa maana hakujua angekuwa mgeni wa nani wakati ule wa dhiki. Ama kweli akufaaye kwenye dhiki ndiye rafiki.

"Eee Mungu umenileta duniani ili niteseke, nikose furaha kila siku. Kwa nini hutaki kujibu maombi yangu? Mbona wengine unawajibu? Kwa

nini ni mimi tu sijibiwi?" Alisema Majuma ndani ya midondoko ya machozi.

Watu waliopita mahali hapo hawakumjali, kila mmoja aliendelea na mambo yake usiku huo. Muda ulisonga kwa kasi bila hata chembe ya usingizi kwa binti huyu kwani mambo yalikuwa mengi kichwani kando na baridi pamoja na mbu waliokuwa wanamtesa kwa usongo.

*******

Kulipokucha Majuma hakutaka kufikiria mara ya pili, aliona ni heri aende nyumbani kuliko kuendelea kuogopa. Aliamini pengine mama yake alimfukuza kwa hasira ya kumpoteza mumewe na labda zile hasira zitakuwa zimeshapotea. Alivyowaza sivyo ilivyokuwa maana alipofika tu nyumbani, mama yake alimtimua na hakutaka kabisa kumtia machoni pake tena. Majuma aliamini mkataba na mama yake pale nyumbani umeisha kabisa.

Alilia vya kutosha pengine ataonewa huruma lakini hakuwepo hata mmoja ambaye alijaribu kunyanyua kinywa kumtetea binti huyu. Hakuwa namna kwani lisilo budi hubidi . Ilimbidi aondoke, Majuma alitembea huku akiangalia nyuma mithili ya mtu anayeaga makaazi yake. Hakujua safari aliyokuwa nayo itakwamia wapi, aliamua kwenda asikokujua mara kadhaa macho yake yakitua kwenye tumbo lake. Alitembea muda mrefu, jua nalo lilikuwa kali la kumuadhibu huku tumbo likalalama kwa njaa kwani muda mwingi ulikuwa umepita bila kutia chochote tumboni. Hakujua cha kufanya ili angalau atulize njaa iliyoibuka ghafla maana hata thumni yenyewe hakuimiliki. Mwili ulianza kulegea na kupoteza nguvu.

Kwa hali ilivyokuwa, Majuma aliona hali ilizidi kuharibika. Pasipo kutumia akili mambo yangekuwa mabaya. Aliamua kuyasogelea mabanda ya mama ntilie akiwa na tumaini kuwa angepewa chochote kwa msaada. Aliingia na kukaa karibu na meza. Kabla hajatulia mama ntilie alifika pale.

“Nikuwekee chakula gani?”

“Mama naomba msaada wa chakula chochote hata kama ni kidogo, sina pesa. Naomba unisaidie nahisi njaa” alisema huku machozi yakimlenga lenga.

“Msyuuu!! Nilipoona umekuja kukaa nilifikiri ni mteja wa maana kumbe umekuja hapa kuniletea ngonjera zako. Hebu toka! Toka we mwanamke. Kama hauna pesa we ni mwanamke, nenda ukajiuze” Mama ntilie alisema hata bila kujali ukali wa maneno yake huku akimsukuma Majuma ili aondoke.

Majuma alitoka kichwa chini aibu imemvaa, machozi nayo bila haya yalianza kutiririka na kufanya mito usoni mwake. Watu wachache waliokuwepo ndani ya banda hilo la mama ntilie waliangua kicheko huku wakimshangaa.

“Yani watu wengine ni wa ajabu sana, yani unajua huna pesa alafu unakuja kukaa wakati unataka kuomba chakula!" Mama mmoja aliyekuwa anakula wali samaki alisema.

Majuma alisukumwa hadi nje huku akilia, hakutaka kubaki hapo maana ilikuwa aibu kubwa kwake, aliondoka huku ameshika roho mkononi. Kutoka mahali pale kwa kusemwa vibaya na kusukumwa haikuwa mwisho wa njaa kali iliyokuwa ikimsumbua na kumfanya awe mnyonge sana, njaa kali iliendelea kumsumbua na hakujua ni wapi pa kwenda akaikomeshe.

Aliumia sana kila alipowaza kuwa anapata shida mithili ya mtoto mkiwa, mtoto wa mtaani ama mtoto asiyekuwa na wazazi, wazazi waliokuwa wanamlea vizuri sasa wamefariki na labda hata makazi yamebomolewa. Haikuwa hivyo kwake kwani mama yake yupo na makazi yao yapo lakini leo nyumbani kwao ni mfano wa kituo cha polisi. Aliogopa kurudi. Alilia sana. Kuna wazo moja liloingia akilini mwake na kumpa tumaini japo kwa asilimia ndogo sana.

Kwa mara ya kwanza, Majuma alimuwazia rafikiye kwa jina Rehema. Rehema alikuwa rafikiye kwa muda mrefu. Rehema alikiwa binti mwenye roho safi na nyeupe jambo ambalo lilimchochea Majuma kuufanya uamuzi kwa kina ili akaishi naye. Licha ya Majuma kuwaogopa marafiki wake, hakuona ubaya wa kwenda kwa Rehema lilivyokuwa jina lake, alihisi angekuwa mkombozi na akaiweka imani yake kwake.

Aliendelea kupiga hatua kuelekea kwa huyo rafiki yake anayeishi kijiji kingine kinachoitwa Maraba ambacho kinapata maili chache kutoka ijiji cha Munduma. Akiwa njiani ndivyo alipokujiwa na wazo kuwa Rehema alikuwa jiko la mtu. Hofu yake nyingine ni juu ya kuwepo ama kutokuwepo kwa rafiki yake huyo kwa miaka kadhaa ilikuwa umepita tangu walipoonana.

Kutoka pale Munduma hadi Maraba anapoishi Rehema ni mwendo wa dakika 30 lakini Majuma alitumia lisali moja na nusu kwani alikuwa anatembea taratibu huku akikaa chini mara kadhaa kwa kuwa alikuwa hoi bin taabani. Majuma alivunjika moyo kwa mbali alipoona kufuli ikining'inia mlangoni. Aliamua kuketi chini, si kwamba alikuwa anamsubiri rafikiye, bali alihisi kunyong'onyea zaidi.

Baada ya dakika tano hivi alisimama huku akiyumba yumba kama mtu aliyepiga mtindi, mwili wake ulikuwa umelegea sana kwa njaa. Aligeuka kurudi alikotoka lakini ilikuwa ghafla bin vuu macho yake kumuona Rehema aliyekuwa akirejea akiwa na ndoo ya maji kichwani.

"Oooh! Majuma, karibu sana"

"Asante dadangu" Alisema lakini sauti haikusikika. Hata nguvu ya kutoa sauti ilididimia.

"Nilikuwa nimeenda kutafta maji" Rehema alisema na kufungua mlango. Waliingia ndani na kuanza kuzungumza.

"Nitakueleza yote lakini kwanza naomba unisaidie chochote nile. Kama hakipo basi naomba maji ya kunywa" Alizungumza kwa sauti yake ile ile. Aliongea huku akitia huruma, machozi yalianza kumtoka.

Machozi hayakutoka machoni pa Majuma pekee bali hata Rehema pia macho yake yalimwaga machozi akimhurumia rafikiye. Alifuta machozi lakini kila alipomtazama rafiki yake, machozi yalimwagika tena na tena

"Kama chakula hakipo naomba maji basi" Alirudia kauli ile ile.

Nyumba ya Rehema ilikuwa chumba kimoja tu hivyo kitanda kilikuwa hapo hapo na vyombo pamoja na kupika ni papo hapo. Aliinuka na kutazama kwenye sufuria iliyokuwa mahali hapo. Hii sufuria ilikuwa na chakula kidogo ambacho kilibaki. Kilikuwa kidogo mno ila Majuma aliona kama ni chakula cha mwaka mzima. Aliendelea kula wakati huo Rehema alikuwa na jukumu moja la haraka, kuandaa chakula kingine kwa ajili ya rafiki yake. Basi ndivyo mambo yalivyokuwa na baada ya yote Majuma alimsimulia kila kitu tangu akiwa Nakuru hadi hapa alipo. Ni hadithi ndefu mno yenye kutumia muda mwingi hata hivyo ilikuwa ndefu zaidi kwani mara nyingi alikuwa anasimulia na kutulia kutokana na kwikwi za vilio zilizokuwa zinamkaba koo.

"Hakika Fitina ni mbaya sana, ila wewe msamehe tu ili nawe uweze kusamehewa. Na kwa kuwa nimeshafahamu ukweli basi nitahakikisha nimeongea na mama yako ili tuyaweke mambo sambamba.

"Hata usijisumbue kwa sababu hatakuelewa. Ameshanikataa mimi na kunifukuza licha ya kujaribu kurudi kwake. Sitaki uongee naye chochote, nitajua mwenyewe pa kwenda."

Rehema alipeleka macho yake hadi kwenye tumbo la Majuma kisha aliwaza huko anakotaka kwenda itakuwaje na ujauzito ule?

"Unataka kufanya jambo la hatari. Wewe unadhani utaenda wapi na hali hii? Ni hatari kwako."

"Yani Rehema nipo tayari kwa lolote. Hata nikifa sawa tu lakini popote naenda" Majuma alieleza. Rehema aliona hapo hapakuwa pa utani. Akamhurumia rafikiye kwa kunyanyaswa na kudhalilishwa na dunia. Alitafakari kidogo kisha akasema "Basi tutakuwa tunaishi wote hapa"

# SURA YA NNE

Wiki imepita tangu wawili hawa walipoamua kuishi pamoja kama ndugu wa toka nitoke, nifae nikufae, anguka nikuinue, lia nikufute machozi. Kwake Majuma alimwona Rehema kama nyota ya kipekee. Alimfaa pakubwa kwani akufaaye kwenye dhiki ndiye rafiki. Majuma alianza kujenga furaha yake upya. Rehema hakuwa na namna ilibidi ajiandike kazi ya ziada kuhakikisha mwenzake anakuwa sawa. Hakutaka kumwacha hata kwa sekunde chache. Kila muda alikuwa naye ili asijisikie mpweke. Jitihada hii bado haikufua dafu ndipo alipoamua awe anamtembezatembeza huku na huku lengo tu kupambana na mawazo ya maswahibu yote yaliyotokea. Tembea yao ilikuwa inawafikisha hata sehemu za mbali huku simulizi zikiwa nyingi njiani.

Haikuwa kazi rahisi Majuma kusahau yaliyotokea kwani kila alipogeuka kulikuwa na alama iliyomkumbusha matukio yote ya jana; aliyeumwa na nyoka akiona ung'ong'o hushituka kwake alama zilikuwa kama kitambulisho cha jana yake. Kilichomsumbua sana Majuma ni alama iliyosimama tisti tumboni na makovu ya moyoni. Siku moja saa sita unusu mchana, wawili hawa waliamua kupunguza muda kwa kutembea hapa na pale .

“Leo tunaenda hadi Murumba”

“jamani ni mbali” Majuma alisema.

“Ni mazoezi tu mdogo mdogo hadi tufike” Rehema alisema.

Safari ilianza na ndani ya majira ya saa nane walifika Murumba. Walizunguka zunguka ila bada sekunde kadhaa, Majuma alishtuka huku

ameachama kinywa chake wazi baada ya kumtia machoni mtu fulani. Alibaki katumbua macho kwa mshangao.

"Majuma mbona unamshangaa sana huyo mtu. Unamjua?" Rehema aliuliza.

"We Majuma!" ilimpasa Rehema kuita tena na kumtikisa maana kwa mara ya kwanza hakusikia. Majuma alishtuka mithili ya mtu aliyesikia bomu.

"Mbona unanishtua Rehema" alisema na kumgeukia mwenzake.

"Naona umemzingatia sana huyo mtu. Unamfahamu?"

Baada ya hili swali Majuma aligeuza tena shingo na kumtazama yule mtu ambaye kwa sasa alikuwa anapanda kwenye gari lililokuwa linang'oa nanga.

"Ah! Mbona unatoa chozi tena? Majuma una shida gani? Nakuuliza kama unamjua yule mtu hunijibu, sasa mimi nitakusaidiaje lakini?" Rehema alihamaki, Majuma aliendelea kububujikwa na machozi mithili ya maji bombani. Alilitazama lile gari akilia kama mtu anayemuaga mtu wake wa karibu sana.

"Unanishangaza sana Majuma. Ushaharibu kila kitu yaani hata ile furaha niliyoitegemea ishapotea." Aliongea na kumshika mkono kumvuta warudi nyumbani.

"Umenisababishia matatizo. Umenifanya nipoteze thamani yangu mbele ya macho ya watu wangu" Majuma alilalamika na kumfanya Rehema apigwe na butwaa. Hakuelewa ni matatizo gani amemsababishia mwenzake. Alihisi ni kama Majuma ameanza kuchanganyikiwa. Hakumjali sana, aliendelea kumvuta na wakiiga hatua kurudi nyumbani. Njia nzima, Majuma alilalamika kwelikweli, kitendo kilicho acha maswali kwa wapita njia kwani hakujali wala kubali hali yake yake ya ujauzito.

Majira ya saa kumi jioni walifika nyumbani. Tangu wafike kilio hakikutulia hata kidogo. Majuma aliendelea kulia huku analitazama tumbo lake. Rehema alijibebesha jukumu la kuanza kumbembeleza rafiki

yake. Haikuwa kazi ndogo kumfanya atulie, mbaya zaidi alikuwa anambembeleza mtu aliyekuwa analia bila sababu iliyojulikana. Juhudi huzaa matunda. Baada ya kutumia muda mwingi kumbembeleza mwenzake hatimaye alinyamaza kulia. Rehema aliitumia nafasi hii kumuuliza yaliyomsibu mwenzake mpaka kubadilika ghafla ziarani pia hakutaka kumuuliza kwa hofu ya kumliza tena.

"Rehema naomba unisamehe kwa kilichotokea. Pili naomba unambie kama ushawahi kumuona yule mtu"

"Ndio, nimewahi kumuona tena sio mara moja"

"Anhaa, sawa!" Rehema alitika na kuzungusha kichwa kwa utaratibu, wote wakawa wamekaa kimya bila kuzungumza tena. Rehema alibaki kumshangaa. Hakutaka kuyazungumzia sana hayo mambo. Aliamua kuyapotezea akijipa tumaini kwamba akiwa tayari atamwambia.

Siku ziliposonga ndivyo hali ya Majuma ilivyozidi kusoroteka. Utenda kazi wake ulizidi kudidimia kwenye kapu la majonzi na machozi. Machozi hayakuumuisha, alilia kutwa kucha. Uso ulikosa nuru, alikonda na kukondeana akawa fremu ya binadamu. Huzuni ilioje! Hata hivyo fikra zake hazikutua kwenye kikomo cha kufikiria.

"Kama yule mtu niliyemuona siku ile sio yeye basi ni ndugu yake. Sura yake ni ile ile. Ameniharibia maisha yangu." Alilia pekee yake. Alitamani angefanya kitu siku ile. Amkamate na kumpiga lakini je, ni yeye anayemhisi? Hakuwa na uhakika.

Kuna wakati mtihani mgumu humpata binadamu yeyote yule ambapo furaha yake binafsi humsaliti kwa kumkimbia na kumuacha atawaliwe na huzuni kwa muda mrefu kiasi kwamba ahisi labda aliumbwa ili aishi kwa dunia ya huzuni na majuto, ahisi hakuumbiwa yule wa kumpenda kwa mapenzi ya dhati.

Ilikuwa siku moja ambayo Rehema alienda mbali na Majuma, alikuwa anaongea na mtu kwenye rukwama yake ndogo iliyochakaa. Alipomaliza kuongea uso wake ulijawa na huzuni kiasi kwamba Majuma

alipomuona alishangaa sana. Aliogopa kwani alijua si bure kwani dalili ya mvua ni mawingu.

"Rehema dadangu, ni taarifa gani umepewa, mbona baada ya kuongea na simu umekuwa hivyo?"

"Majuma, nakupenda sana dadangu. Nimeumia kwa yote yaliyokukuta na nilitamani kukusaidia hata kwa kile kidogo nipatacho lakini kwa hali ilivyo sasa naona sina namna." Rehema aliongea huku analia, akimuonea huruma rafiki yake.

"Kiaje? Sijakuelewa!" Alishtuka. Machozi yalimlenga lenga nazo nguvu zilimwishia. Ama kweli jambo usilolijua ni usiku wa giza.

"Nakuonea huruma sana Majuma. Nimejaribu kukutetea kwa uwezo wangu lakini imeshindikana," alisema na kufuta machozi.

"Kwani tatizo ni nini Rehema? Niweke wazi" aliuliza mara baada ya kushindwa kujua ni kipi kinaendelea. Aliuliza kwa wasiwasi mkubwa. Rehema alishindwa kujibu chochote zaidi ya kilio kilichokuwa kinaendelea kusikika. Hali hii ilizidi kumchanganya Majuma, hakujua ni taarifa ipi iliyomuumiza mwenzake na hiyo taarifa inahusiana vipi na yeye.

"Basi nambie na mimi nijue ni nini kinaendelea jamani" alilalamika lakini kupata jibu lilikuwa suala nzito. Ghafla ulisikika mlio wa simu kuashiria kuingia kwa ujumbe. Rehema alifuta machozi na kuangalia. Mshtuko uliongezeka sana baada ya kufungua na kuusoma ujumbe ule. Machozi yaliongeza kasi ya kutoka.

"jamani" Majuma alitamka kisha nae akaanza kulia.

Alipoona anashindwa kusema kinachoendelea alichukua simu na kumpa Majuma asome ujumbe ulioingia.

"Mimi narudi kesho, sitaki nimkute huyo mbwakoko, aondoke ama uondoke wewe"

Hivi ndivyo ulivyosomeka ujumbe ule ambao ulitumwa na mtu aliyeandikwa kwa jina la 'Mume wangu'. Kwanza alishangaa kuona kuwa Rehema alikuwa na mume maana tangu ahamie kwa Rehema hakuwahi sikia taarifa zozote kumhusu. Majuma alibaki njia panda, sasa kilichotawala hisia zake kwa muda huo ni ujumbe wenyewe. Anatakiwa kuondoka kwa nini? Baada ya Rehema kutulia aliamua kumhadithia vizuri yaliyojiri.

"Mume wangu kesho anarudi kwa maelezo aliyonipa. Sasa nilimwambia kwa wema kuwa nakaa na wewe lakini aliposikia hivyo, alikataa katakata kwa madai kwamba nyumba yenyewe ya chumba kimoja, tutaishije na wewe? Nimekutetea kwa uwezo wangu lakini kama ulivyoona ni mkali, hivyo sina namna japo naumia."

Kijasho chembamba kilimtiririka Majuma, angekuwa na tatizo la presha basi huenda maisha yangekatika bila habari. Nayo machozi bila heshima yaliuchafua uso wake.

"Mimi nitaenda wapi sasa, sina pa kwenda mimi. Kila mahali wananikataa. Nimemkosea nini Mungu?? Dada tafadhali usinifukuze tafadhali, nionee huruma" aliomba msaada kwa Rehema akisahau kuwa Rehema hana shida, mwenye shida ni mume wake.

Majuma alilia vya kutosha akiona ule mwanga uliobeba nuru ya asubuhi yake ghafla unapotea na kumezwa na domo kubwa la giza totoro. Furaha ilianza kuchanua na kwa kiasi fulani mifupa iliyokuwa ikionekana kutokana na kukonda kwake ilianze kupotea lakini unahisi itakuwaje? Rehema hata hakujua anaanzia wapi kumuacha rafiki yake wa dhati aondoke. Uliingia ujumbe mwingine uliosomeka hivi

"Wewe mwanamke sitaki kubishana, nimesema huyo rafiki yako aondoke. Sasa nikimkuta nitamfanyia kitu ambacho hatawai sahau" aliusoma akiwa na mshtuko mkubwa lakini hakutaka kumuonyesha Majuma ujumbe ule.

“Majuma naomba lala tu kwa leo kisha kesho mapema jitahidi uondoke ili kuokoa uhai wako. Yani nakosa namna ya kukusaidia dadangu.” Rehema alisema.

Majuma alikubali kulala hapo na mida ya usiku iliingia akiwa hatambui maana alikuwa mbali sana kimawazo. Hakujua ni wapi ataenda kuishi na hali aliyonayo.

“Na hii mimba nitaenda kuishi wapi mimi?” alijiuliza na kuanza kulia kwa uchungu. Ilikuwa karibu saa tano za usiku, Rehema alikuwa amelala lakini Majuma alikosa hata lepe la usingizi. Mida ya saa sita na robo Majuma alisikia mlango ukigongwa. Hofu ilimjaa haswa, hakujua ni nani anagonga. Alitulia bila kwenda kufungua. Mlango uliendelea kugongwa, Majuma alitamani hata amuamshe mwenzake ila kabla hajafanya hivyo ilisikika sauti.

“Fungua mlango mke wangu, nimerudi.” Majuma aliogopa alipogundua kumbe mgongaji ni mume wa Rehema.

“Si alisema atarudi kesho?” alijisemea kwa uoga huku akikihisi kinachoenda kumtokea.

******

Majuma alinyoosha mkono ili amtikise mwenzake aamke lakini alihofia. Sasa alipata hofu kuinuka kwenda kufungua mlango pia dhamira ya kumuamsha mwenzake ilizuiwa na hofu. Alibaki katikati hajui afanye nini. Mlango uliendelea kugongwa. Majuma alikosa namna ilibidi amuamshe mwenzake kwa kumtikisa na kwa sauti ya kunong’ona. Alimtikisa mara nne ndipo Rehema aliamka.

“Nini tena, mbona kuamshana usiku usiku ah!” Rehema alichukia kwa kitendo cha kukatishwa usingizi wake.

“Kuna mtu anagonga” Majuma aliongea kwa sauti ya chini.”Nani?”

“Sijui, kamfungulie” alisema lakini Rehema hakujali, bado wenge la usingizi lilimsumbua.

“Wewe mke wangu, haupo au unamficha nani humo ndani?” ilikuwa sauti kutoka nje. Rehema aliisikia vizuri sana na kugundua kuwa alikuwa mume wake. Usingizi wote ulitoweka. Aliamka na kubaki anababaika asijue cha kufanya. Ungemtazama namna alivyokuwa anapata shida hakika ungedhani labda mume wake anaenda kumfumania na mwanaume mwingine hapo ndani.

“Majuma tufanyaje sasa? Alifika kitambo?” Majuma hakujua ajibu gani kwanza. Aliinuka kwa papara, alijifunga kanga yake vizuri na kutembea kwa woga kuelekea mahali ulipo mlango. Kabla hajaufikia alimgeukia Majuma na kumpa ishara ya kuingia uvunguni lakini Majuma hakutaka kufanya hivyo. Aliona hana namna yoyote na alishajiweka tayari kwa lolote. Taratibu na kwa hofu kubwa alifungua mlango. Kukaripiwa ndio ilikuwa salamu ya kwanza kupewa, alikaripiwa kwa kuchelewa kufungua mlango. Baada ya hapo mume wake aliyeitwa Mafutu aliingia ndani huku akiendelea kufoka wakati huo yeye alibaki pale pale mlangoni.

Macho ya Mafutu yalitua juu ya binti mdogo aliyekaa kitandani, uso wake ameupakata kwenye viganja vyake vya mkono.

“We mpuuzi, unafanya nini hapa? Sitaki kukuona ndani kwangu hapa, tokaa!” ilisikika sauti ya Mafutu aliyeonekana kulewa kwa kiasi fulani.

“Nimesema tokaa, bado unang’ang’ania hapo?” alifoka na kumfuata Majuma. Rehema alipoona hivyo aliamua kuwahi na kuingia kati.

“Tafadhali mume wangu, unataka kufanya nini? Kwani amekukosea nini huyu msichana wa watu?”

“Nipishe nimfinyeee” alifoka hadi Majuma akaogopa. Aliinuka na kujibana ukutani.

"Umpige amekukosea nini? Humjui hakujui sasa kosa lake ni lipi? Kama kuondoka hapa hilo ni jambo la kuelekezana tu sio umfukuze hivyo kama mna uadui. Mbona unakuwa wa ajabu mume wangu?"

"Mimi ni wa ajabu? Natisha?" alihamaki na kurusha kofi lililosambaa usoni mwa Rehema. Hali ilibadilika, nyumba ilikuwa uwanja wa vita. Bwana Mafutu alimpiga Rehema kisha akamfuata Majuma na kumpiga mateke bila kujali yanaenda kutua mahali gani. Teke moja lilitua tumboni mwa Majuma.

"Mama yangu, nakufaaa" Majuma alilalamika na kushika tumbo, alianguka chini huku akishuhudia kofi zito likitua usoni mwake. Alijiona ana mkosi wa ajabu na balaa la kipekee yani licha ya yote yaliyomtokea nyuma leo hii anapigwa bila sababu yoyote. Kugaragara kwake chini hakukumfanya bwana Mafutu kuingiwa na huruma. Alimshika mguu na kumvuta hadi nje na kumuaga kwa teke la mgongoni. Majuma alibwagwa chini vibaya mno na hakika aliumia si kidogo. Mlango ulifungwa na kuachwa pale nje bila kuonewa huruma. Akiwa pale nje, alisikia kelele ndani.

"Unataka uende wapi? Unajifanya mama huruma sana lilivyo jina lako?" baada ya kauli hiyo ilisikika sauti ya kofi na vilio. Majuma hakuwa na jinsi, aliinuka na kujikung'uta mavumbi huku akihisi maumivu karibu sehemu zote za mwili wake. Hakujua aende wapi usiku huo lakini aliona popote aende cha msingi ajistiri pa kulala. Alijaribu kutembea, alikuwa anachechemea huku kizunguzungu kikikipiga kichwa chake kwa maumivu makali. Hali yake ilikuwa mbaya sana. Hatua tano za kinyonge zilitosha kabisa kumfikisha mahali ambapo hakuweza kuendelea zaidi. Alianguka chini na kuhisi giza likiongezeka mara dufu machoni pake.

Giza liliongezeka mara dufu machoni pake na kwa mbali kizunguzungu kilivuruga kichwa chake. Alibaki pale chini mithili ya mtu aliyechanganyikiwa kwani ilikuwa ngumu kuelewa ni nini kinaendelea na afanye nini. Dakika ziliyoyoma akiwa yupo chini hajitambui hata ile

miwasho iliyotokana na kung'atwa na mbu hakuisikia hata kidogo. Mbu nao hawakumuonea huruma, walimng'ata kwa usongo.

Baada ya masaa kusonga, Rehema alitoka akiwa na tochi mkononi. Alikuwa na shauku ya kumpata rafiki yake maana muda wote Rehema alipokuwa ndani hakufanikiwa kupata amani wala lepe la usingizi kwani mawazo juu ya rafiki yake na usalama wake yalimtesa sana. Ndipo alipofikia maamuzi ya kutoka ili akamtafute huku akimuacha mume wake ndani amelala fofofo!

Alitoka akiwa hajui anaenda kumtaftia wapi lakini Imani fulani ilimjia kwamba usiku kama huo si rahisi Majuma kwenda mbali, aliamini ni lazima atakuwa amejibana mahali akisubiri kukuche. Baada ya kutoka na kutembea hatua kama kumi na tano, mwanga wa tochi yake ulimsaidia kumuona Majuma aliyekuwa chini hajitambui. Alianza kupaparika bila kujua nini cha kufanya ili amsaidie rafiki yak

Wazo la kumpepea lilimjia, wakati huo ilikuwa saa nane za usiku. Kwa kutumia kanga yake aliyoikunja vizuri alianza kumpepea na si haba, hili zoezi lake lilizaa matunda baada ya dakika kama 25 kupita. Majuma alisimama na kurudiwa na fahamu zake. Na baada ya kuwa sawa Rehema alimpa pole.

"Majuma pole"

"Asante! Vipi kuhusu shemeji, hatokugombeza?"

"Usijali, achana naye"

"Sawa, asante. Nenda ndani basi. Niache ntalala hapa hapa nje mimi.

"Mahali utakapolala ndipo ntakapolala"

Majira ya saa tisa usiku wakiwa palepale nje pembeni kidogo ya nyumba ile, ghafla walisikia mlango ukifunguliwa kwa nguvu. Moja kwa moja walihisi mfunguaji ni mume wa Rehema, bwana Mafutu hapo ndio walijibana kwelikweli.

"Majuma hatutakiwi kuendelea kujibana hapa. Tukimbie haraka tujifiche pale mbele." Rehema alisema na bila kupoteza muda walikimbia na kujificha kwenye eneo moja lililokuwa na nyasi ndefu. Hawakujali usalama wa eneo hilo, kuna wadudu au hakuna. Macho yao waliyaelekeza huku kwenye nyumba na dakika moja tu tangu wakimbie pale walishuhudia bwana Mafutu akifika eneo walilokuwa wamejificha awali. Kwa msaada wa mwanga wa mbalamwezi waliona kitu chenye kumeta meta kilichoshikwa mkononi mwake. Ilikuwa rahisi sana kugundua kuwa lile lilikuwa panga. Bwana Mafutu alidhamiria kuua, pengine alidhani mke wake ametoka ili afanye usaliti.

Aliangaza huku na huku kisha alienda uelekeo fulani ambao ni upande wa kushoto wa ile nyumba. Alikuwa anamtafuta mke wake kwa hasira.

"Dada, umeona sasa nmekusababishia matatizo. Nilikwambia wewe rudi ndani tu" Majuma alilalamika.

"Twende huku, nifuate Majuma" Rehema alisema na kuanza kukimbia haraka mithili ya mtu anayekwepa jambo. Hakutaka kuchelewa hatimaye waonekane. Majuma alikuwa nyuma akikimbia mbio kumfuata Rehema aliyekuwa ametangulia, tochi ameizima ili wasije kugundulika. Ni mwanga wa mwezi tu ndio ulikuwa msaada kwao. Walikimbia kwelikweli, wakati huo Majuma alikuwa hajui ni wapi wanaenda.

"Tunaenda wapi sasa?" aliongea huku anatweta ungedhani alikuwa na mzigo mzito. Alichoka mapema na pumzi zilianza kumwiishia maana hali aliyokuwa nayo haikuruhusu kukimbia kimbia.

"Majuma twende tu popote kuokoa roho zetu."

Walipunguza mwendo mara baada ya kuona wako mbali na nyumbani pale. Mwendo wao wa taratibu uliwafikisha Murumba. Kitendo cha kufika hapo kilimfanya Majuma amkumbuke yule mtu aliyemfananisha siku moja. Walitulia sehemu moja kupumzika.

“Rehema, ulinambia yule mtu tuliyemuona siku ile unamfahamu?”

“Ndio namjua”

“Unamjua kivipi?”

“Jina na kazi yake tu ambayo ni ukondakta.”

“Mmmh! Hivyo tu?”

“Labda na mahali anapokaa, pia napajua”

“Hapo sawa, naomba kesho unipeleke anapokaa” Majuma alisema.

“Unasemaa?” Rehema aliuliza ungedhani hakusikia alichoambiwa.

“Kesho nipeleke kwake tafadhali”

“Kwani unamjua? Na kwa nini unahitaji kwenda kwake?”

“Dada utajua huko huko, cha msingi we nipeleke na tumkute”

“Mmmh!!! Kwani kuna ugumu gani kuniambia. Tangu siku ile hukutaka kunieleza” Rehema alilalamika japo kwa mbali alihisi jambo.

“Kwanza kumkuta itakuwa bahati, maana si unajua ile kazi yao, huwa wanatoka mapema.”

“Hata tusipomkuta haina shida, cha maana nipajue”

“Sawa mama, nimekuelewa.” Rehema alijibu na kutulia akiweka sawa suala hili na lile akilini mwake hasa lililokuwa linajaribu kumuumiza kichwa.

“Kwa hiyo tunalala wapi sasa?” Majuma aliuliza.

“Kama unavyoona namna haipo, basi tunalala hapa”

“Majambazi nao Je?"

“Mungu yupo nasi usiwe na shaka” Rehema alizungumza. Majuma aliyakaza macho yake kwa Rehema, kwa msaada wa mwanga hafifu wa mbalamwezi alimtazama huku akimuonea huruma.

"Dada, unateseka kwa ajili yangu. Najua wakati huu ungekuwa umelala nyumbani kwako." Majuma alisema akionekana kuumia katika hili.

"Nishakwambia usijali Majuma" alisema huku anaushusha mwili wake hadi chini na kujaribu kulala. Mmmh! Alijigeuza baada ya kuona ule upande ulikuwa haukidhi mahitaji ya usingizi wake. Alijilaza tena na kwa kujaribu huko alipata jawabu kuwa si haba kutakuwa na ugumu katika zoezi la kuupata usingizi. Lakini angefanyaje?

"Mbona hulali Majuma?" Rehema aliuliza na kuachia tabasamu dogo. Majuma hakuwa na hiyana, ilibidi kujilaza pale chini.

"Kaah! Rehema si una kanga!!" alilalamika baada ya kuumia.

"Ndio ninayo lakini nimeona ni vyema kujifunika kuliko kutandika chini. Si unajua baridi na mbu!"

Huu ulikuwa usiku tena wa masaa machache yaliyosalia lakini kwao ilikuwa mithili ya miaka kumi ya mateso utumwani. Hakuna marefu yasiokuwa na ncha, hatimaye asubuhi ilifika wakiamshwa na kelele za watu waliokuwa na alama za mshangao kwa kile walichokiona. Watu walishangaa sana, ilibidi wainuke haraka na kuondoka pale.

"Wana bahati sana, kulala nje na kuamka salama! Inawezekana majambazi walienda likizo." Alisikika mama mmoja.

"Dada nilisema unipeleke anapoishi yule mtu" Majuma alisema baada ya kutembea sana kuona wanakoelekea ni nyumbani kijijini Munduma.

"Ah! Nimechanganyikiwa" Rehema alisema na kuongezea

"Hata hivyo hakujaharibika kitu, hata hiyo njia Ile hapo itatufikisha" safari ya kwenda anakokaa mtu aliyehitajika na Majuma ilianza. Walitembea kwa mwendo wa kawaida na iliwachukua muda wa dakika 20 kufika mahali walipohitaji.

"Ndio hapa" Rehema alisema ila Majuma alikuwa kimya, macho yake yakichunguza namna nyumba ilivyokuwa. Ilikuwa nyumba chakavu, mbovu mbovu huku mlango ukiwa bati.

"Majuma ndio hapa sasa"

"Aaah! Sawa Rehema gonga basi" Majuma alisema baada ya kushtuka.

"Sidhani kama yupo" alisema ila kwa kutaka kumridhisha mwenzake Rehema alisogeana kugonga taratibu mlango ule wa bati. Aligonga mara mbili kisha sauti ikasikika.

"Nani? Nakuja"

Sauti hii iliposikika ilisababisha mpasuko wa hofu ndani ya moyo wa Majuma na kufanya apumue kwa nguvu. Hazikupita dakika nyingi, mlango ulifunguliwa na kutoka mwanaume mmoja. Macho yake yalisambaa kwa wageni wake akianza na Rehema. Alipofika kwa Majuma alishindwa kuzuia mshtuko mkubwa alioupata. Ukimya wa sekunde kadhaa ulitokea huku kila mmoja akionyesha mshtuko ambao si haba ulikaba nafsi yake. Macho ya Majuma yakawa kwa mtu huyu yakipeleka taarifa kwenye ubongo sehemu ya kumbukumbu. Kumbukumbu ilikuja na kutoweka hivyo alibaki katikati hajui aamini au asiamini.

"Hivi, huyu ni yeye kweli?" Majuma alijiuliza bila kupata jibu ila ule mshtuko alioonyesha mtu yule kwa kiasi fulani ulimfanya Majuma aamini pengine ni yeye. Kwa nini ashtuke?

"Samahani sana ndugu yangu, tumekuja kwako ghafla hata bila taarifa" Rehema alivunja kimya kile kifupi lakini kikajenga kimya kingine kifupi kisha baada ya sekunde kadhaa yule mtu aliuliza.

"Mnataka nini?" aliuliza kwa sauti iliyokuwa na chembe chembe za hasira ndani yake, macho yake yaliwaka. Mioyo ya Rehema na Majuma ilitetemeka kwa hofu.

"Rafiki yangu ndiye aliyehitaji ku.. kuonana naw..ewe"

Macho ya yule mtu yaligeuka kwa Majuma, Majuma akapata kihoro, akahofia kusema kilichofanya aende pale. Alitamani kukataa kuwa yeye hakuhitaji kuletwa hapo. Alijiona mjinga kuruhusu woga uharibu kila alichopanga, hivyo basi alipambana mapema na woga ule. Alivaa ujasiri na kusogea kwa umakini uliojazwa ujasiri wa kikomando.

“Unanikumbuka?” aliuliza baada ya kumsogelea karibu ungedhani alikuwa na mpango wa kumkumbatia.

“Sikukumbuki kwa chochote” alijibu

“Kwa nini ulishtuka uliponiona?” Majuma aliuliza huku amekaza macho. Muonekano wake ulishangaza hata Rehema.

“Hapa ni kwangu usisahau, kuwa na heshima bana siko polisi alaah!” alisema na kuingia ndani kisha alifunga mlango wake wa bati. Majuma alitoa chozi lakini hakutaka kutetereka wala kurudi nyuma.

“Rehema wewe nenda, mimi nipo hapa”

“Mmmh! Siwezi kuondoka na kukuacha hapa wakati hata sijui kwa nini unataka kubaki hapa, siwezi” alijenga msimamo thabiti.

“Niko salama na nitakuwa salama”

“Kwanza kwa nini hutaki nijue kinachoendelea? Wewe si ulisema tukija nitajua?”

“Sawa dada punguza hasira basi” alisema na kuguna kidogo kisha alisema

“Kiufupi huyu ndiye aliyenipa huu ujauzito”

“Nini???”

“Ndio hivyo dada na ndio maana alishtuka kuniona. Sasa kwa sababu nishafika hapa, siondoki.”

“Mmmh! Majuma una uhakika ndio huyu?”

“Ndio huyu”

“Sasa unadhani atakubali ukae hapa?”

“Akubali akatae mimi nitakaa hapa alee mimba yake. Unahisi nitaenda wapi sasa?” Majuma alihoji. Rehema alibaki kimya kisha aliguna na kuonyesha waziwazi kwamba hakuwa na jibu.

“Dada wewe ondoka uende nyumbani, najua shemeji anakutafuta huko.”

“Sawa naondoka lakini moyo wangu unahofia sana. Nina hofu na usalama wako kipenzi.”

“Usijali, mimi ni simba jike.” Alijibu kwa kujiamini kisha wakakumbatiana. Rehema alimbusu Majuma shavuni kisha alianza kuondoka huku akigeuka nyuma mara kadhaa. Baada ya kuagana kwa huzuni na machozi Majuma alisogea hadi karibu na mlango ule na kujishauri mara kadhaa kabla ya kufikia uamuzi aliokuwa nao. Baada ya kujishauri vya kutosha alijitoa mhanga kusukuma ule mlango na kuingia ndani. Alipoingia ndani macho yake yalitua juu ya vyombo vichache vilivyokuwepo, sofa lililochakaa haswa. Alitembeza tena macho yake hadi mahali kilipo kitanda. Mmh! Si kitanda bali ni matofali kadhaa yaliyopangwa vyema kushikilia vijigodoro vilivyochoka choka. Aliinua macho yake hadi juu ya kitanda hiki, alistaajabu kuona yule mtu akiwa amelala kama mtu aliyepata usingizi tangu kitambo kirefu.

“Mmmh! Sasa hivi ashalala tayari? Ananiigizia!” alijisemea na kuanza kupiga hatua za kunyata hadi kilipo kitanda kile. Alimchunguza yule bwana kwa muda fulani na kwa kuwa alikuwa karibu naye basi hata ile sauti ndogo ya kukoroma ilikuwa inasikika maskioni mwake.

“Hata kama unaniigizia mimi ndo nishafika hapa” alijisemea na kukaa chini kupumzisha mwili wake. Alikuwa na uchovu wa usiku mzima maana hata kulala alilala kwa muda mfupi mno. Tumbo nalo lilianza kumsumbua lakini haikuwa sababu ya kuukimbiza ule usingizi ulioanza kumnyemelea. Aliamua kuegemea pembeni ya kitanda kile. Ila kabla hajafanya hivyo alishuhudia yule bwana akiinuka toka kwenye kitanda.

# SURA YA TANO

Njiani Rehema alitembea huku mawazo chungu nzima yakimsumbua kichwa chake juu ya yale yatakayotokea akifika nyumbani. Alimjua vyema mume wake, bwana Mafutu. Hofu iliutanda moyo wake lakini hakuwa na namna nyingine, ilibidi arudi nyumbani. Kama ilivyo kawaida ya uhalisia wa mambo hakika ukingo wa mbio za sakafu aliyokuwa anapita ulifika. Hatimaye alikuwa mbele ya mlango wa nyumbani kwake. Ule mlango ulifungwa na hakujua mume wake yuko wapi. Alitazama kushoto na kulia bila kuona chochote. Aliamua kugeuka nyuma, moyo wake ulipiga "paaah!" mara baada ya kumuona mume wake akirudi pale nyumbani. Mkononi alikuwa ameshika panga.

Hofu ilimkumbatia, wasiwasi ulimshika huku woga ule ukilegeza miguu kidogo aanguke chini. Bwana Mafutu aliendelea kupiga hatua kali huku macho ameyatumbua kwa hasira. Rehema aliona kifo kipo karibu naye. Kwa nini? Amefanya kosa, sasa amlaumu nani? Hakutaka kujijibu. Hatua tano zilizosalia ili kumfikia Rehema ziliisha ila cha ajabu bwana Mafutu aliongoza moja kwa moja hadi ndani ya nyumba bila kusema wala kufanya chochote kile, wakati huo kijasho chembamba kilikuwa kinamtiririka mwanadada huyu.

Hakuamini kilichotokea, alihisi kama ni ndoto na kama sio ndoto basi ni muujiza uliomtembelea wakati ule. Alitumia dakika mbili pale nje akijiuliza maswali juu ya nini na kipi cha kufanya. Hakujua na hakika hakufanya chochote kile zaidi ya kuishia kurusha rusha mikono na mara kadhaa kuibeba kichwani huku machozi yakibisha hodi. Baada ya dakika

za vituko hizo kumalizika ilisikika sauti nzito iliyopewa ujazo wa ukali wa hasira. Sauti hii ilisikika kutoka ndani ya nyumba.

"We mwanamke kuja hapa!!" licha ya kusikia wito huo hakunyanyua mguu kwa lengo la kuupeleka mwili wake ndani aliko mume wake. Sekunde zilizonga

"Wewe si nimekuita, au dharau!" ilisikika kwa mara nyingine. Kwa wakati huu Rehema hakuwa na cha kusubiri, alitembea haraka yani hata ile miguu iliyokuwa mizito utadhani alibeba miguu ya tembo basi ilikuwa nyepesi mno kwa wakati huo. Aliingia ndani na kumsogelea mume wake kwa uoga.

"Unasimama huko? Songea njoo ukae hapa" bwana Mafutu aliwaka na kumuonyesha Rehema mahali alipotakiwa kukaa. Hofu ilizidi hasa alipogundua mahali alipoambiwa akae palikuwa na panga. Taratibu sana kwa uoga na hofu alisogea na kukaa chini huku akitetemeka karibu kila kiungo cha mwili wake. Baada ya kukaa ulifuata ukimya mfupi kisha baada ya dakika chache sana sauti nzito ya bwana Mafutu iliuvunja vunja ukimya ule.

"Mke wangu" aliita lakini kwa sauti yaupole hata Rehema alishangaa. Alibaki kushangaa, akasahau kuitika.

"Mbona unanifanyia hivi? Hivi unadhani ulichokifanya ni sawa? Yani mmetoka hapa usiku na sijui mmekimbilia wapi. Ikanibidi niingie mtaani kuwatafuta na hapa ndio nimerudi, vipi kama mngepata madhara? Haya, na huyo mwenzako yuko wapi?" aliuliza kwa umakini. Aliuliza maswali ambayo yaliendelea kumuacha Rehema katika mshangao mkubwa.

"Sai ndo anajifanya kuhofia usalama wetu" Rehema alijisemea.

"Mwenzako yuko wapi? Na je yuko salama?" aliuliza tena ndipo Rehema alipoamua kueleza kila kitu. Kwanza alishusha pumzi ndefu kisha alianza kumueleza yote yaliyojiri tangu awali hadi mahali alipo

mwenzake kwa wakati huu. Bwana Mafutu aliumia sana kusikia yote hayo, moyo uliumia.

“Mmh! Sikujua. Naomba unisamehe kwa yote. Mengine nimefanya si kwa akili zangu, ni pombe.”

“Usijali mume wangu, nilishakusamehe kitambo tu”

“Vipi sasa huko aliko na hali yake hiyo?”

“Hata mwenyewe sijui”

“Kwa nini sasa umekubali kumuacha huko kama uhakika wa usalama wake hauna!?”

“Mmmh! Aling’ang’ania kubaki kule hata hivyo hakuwa na sehemu nyingine ya kwenda maana kurudi huku isingewezekana kabisa”

“Oooh! Basi usiache kumtembelea rafiki yako kila wakati ili uwe unamjulia hali yake.”

“Sawa, Nashukuru sana mume wangu” Rehema alisema na kumkumbatia mume wake. Ugomvi uliisha kiwepesi.

******

Kabla Majuma hajaupumzisha mwili wake pale chini alishuhudia yule bwana akiinuka toka kwenye kitanda kile. Kwa mbali hofu ilitambaa ndani yake toka miguuni hadi utosini mwake si haba alijikaza kisabuni na kuwa tayari kwa chochote kitakachotokea.

“Wewe mwanamke ni kichaa au? Unanitakia nini mimi, au unantaftia kesi?” hii ilikuwa kauli ya kwanza kutoka kinywani mwa bwana huyu aitwaye Joshua. Aliyatumbua macho. Majuma hakushughulika kujibu chochote kile.

“Nakuomba uondoke kabla sijakufanyia jambo mbaya ama kukuua mwenyewe hapa ndani.” Kwa mara nyingine Majuma hukujibu chochote, aliinuka na kujitupa kitandani huku akipapasa tumbo lake.

“Yani naongea na wewe na unaniletea dharau? Nakwambia uondoke unajifanya kiburi, wewe ni jeuri au sio? Sasa ngoja uone.” Bwana Joshua alisema na kutoka nje kwa hasira. Kitendo cha kutoka nje akiwa na hasira kilimfanya Majuma aingiwe na wasiwasi mkubwa. Hakujua ni kitu gani ambacho Joshua alikifuata huko nje. Hakujua ni kitu gani ataingia

nacho ndani na kitakuwa na madhara gani kwake. Hofu ilimshika. Dakika chache baadaye mlio wa bati uliokuwa pale mlangoni ulisikika kisha bwana Joshua aliingia akiwa ameshika fimbo kubwa mkononi. Roho ya Majuma ilienda mbiombio hasa baada ya kuona anafuatwa mahali alipo.

Hakujua afanye nini na hata alipotaka kuishughulisha akili yake kufahamu kipi cha kufanya kwa muda huo, alishtuka ghafla bin vuu fimbo ikitua mwilini mwake. Kabla hajatoa sauti kwa maumivu makali yaliyotafuna bega lake kwa mara nyingine fimbo ilitua mwilini mwake. Hili jambo likawa mwendelezo. Majuma alipiga kelele za maumivu na kuinuka pale kitandani. Fimbo ziliendelea kurindima akipigwa sehemu mbalimbali za mwili wake na mpigaji alionekana kutokujali wala kuhofu chochote. Majuma aliona asipokuwa makini basi atapigwa sana, alidaka fimbo iliyokuwa karibu kutua kwenye uso wake ambao ulikuwa na dalili ya kuvimba hadi sasa. Aling'ang'ania fimbo ile kwa nguvu huku purukushani kali zikiendelea. Fimbo ilivunjika lakini kuvunjika kwa fimbo haikuwa mwisho wa kipigo. Makofi mazito ya kiume yalichukua nafasi yake, Majuma alipigwa sana hadi alihisi nguvu inamuisha. Alianguka chini na kuuficha uso wake kwa viganja vya mikono ili kuzuia mwendelezo wa makofi. Hata hivyo kujificha hakukuzuia mateke yaliyokuwa yanarushwa na bwana Joshua. Baada ya kumpiga na kuridhika alianza kumvuta kwa nguvu.

"Niacheee! Si umeshanipiga, niacheee!" Majuma aliongea huku akilia lakini haikutosha kumfanya Joshua asiendelee kumburura. Aliburuzwa mpaka nje na kutupwa kama mzigo. Baada ya kumfanyia yote hayo, Joshua aliingia ndani na baada ya dakika chache alitoka na kufunga mlango wake.

"Sasa nirudi nikukute hapa, utanitambua mbwa wewe. Mimba, mimba! Si ulikula pesa zangu?" Alisema na kuondoka na kwenda alikokujua yeye mwenyewe. Majuma alinyanyua kichwa na kuelekeza macho yake kwa Joshua aliyekuwa anaondoka. Alimtazama hadi alipopotea kwa macho yake ambayo yalikuwa yamevimba. Machozi hayakuacha kumtoka Majuma, kwikwi za vilio zilimkamata na kumkaba koo. Ile kauli ya bwana Joshua…"mimba, mimba! Si ulikula pesa zangu" ilimrudisha nyuma na kukumbuka mengi.

Alikumbuka namna Fitina alivyozaa matatizo yote haya yanayomkumba. Alikumbuka aliporudi nyumbani kwao kijijini Munduma, alikumbuka namna kilivyotokea kifo cha babake na vile alivyofukuzwa. Alikumbuka yote hadi hapo alipo, hakika uchungu ulizidi. Achana na uchungu na maumivu yanayotafuna moyo wake, yametokea maumivu mengine makali yaliyokuwa yanautafuna mwili wake mzima. Mgongo ulikuwa unauma, mabega, miguu, uso nao ulivimba, mikono pamoja na tumbo kulikuwa na vidonda kutokana na kuburuzwa. Mwili mzima ulifukuta kwa maumivu lakini suala la kuondoka hakutaka kulipa nafasi. Alikuwa tayari kufia pale pale.

Muda nao ulisonga akiwa palepale chini. Wakati fulani alijitazama namna alivyoumia kisha alilitazama tumbo lake na kulipapasa.

"Mungu akulinde mwanangu. Mama yako naumia sana, Napata maumivu makali lakini usijali mimi nakusubiri hapa duniani, nakusubiri uje labda utanipa furaha." Aliongea na kufuta chozi. Ilikuwa saa kumi na mbili jioni, baridi ilianza kusambaa huku na huko na kuleta madhara kwa viumbe visivyopenda hali hii. Majuma alianza kutetemeka hadi akaamua kuinuka kwa lengo la kuingia ndani hata awashe moto ili tu apate joto mwilini. Aliinuka ila kabla hajasimama vizuri miguu ilikosa nguvu, alipepesuka na kuanguka chini. Maumivu na njaa vyote kwa pamoja vilisababisha kuanguka. Angefanyaje? Anahitaji chakula. Alijikaza na kusimama tena kisha aliusogelea ule mlango wa bati ila kabla hajafanya chochote kile, alipepesuka tena na kuangukia mlango uliokuwa wa bati. Mlango uling'ooka naye akaanguka nao ndani hadi chini.

"Aaaaiih!" zilikuwa kelele kutoka kwa Majuma baada ya kufika chini na kuubamiza uso huku bati lile likipita kwenye mkono wake wa kulia na kumchana. Jeraha lenye ukubwa wa wastani lilionekana pale mkononi mwake, jeraha lililopelekea damu kutoka kwa kasi na kusambaa chini.

Maskini Majuma! Kizunguzungu kikali kilivamia kichwa chake, giza likaanza kuenea machoni pake na kuchanganyika na giza la jioni ile. Giza likatanda maradufu kiasi cha kushindwa kuona chochote kilichokuwa mbele yake. Macho yalikosa nuru. Yale maumivu hayakujali njaa ya binti huyu wala uchovu wake, maumivu hayakuwa na huruma hata kidogo, yaliendelea kumtafuna katika sehemu mbalimbali za mwili wake. Majuma alijikaza kwa mara nyingine kuinuka lakini nguvu

ilimsaliti na kama ilivyokuwa mara kadhaa hapo awali, aliishia kujipigiza chini na kuongeza maumivu. Maskini Majuma. Kumbe wanadamu wakikusaliti pia hali humsaliti mtu.

# SURA YA SITA

Muda wa saa moja jioni, bwana Joshua alikuwa anarudi nyumbani akiwa ameshika simu ndogo ya kubonyeza iliyokuwa inatoa mwanga. Mkono wake wa kulia ulishikilia mfuko ulioonekana kuhifadhi vitu vingi hasa. Sauti ya chini kabisa ilitoka kinywani mwake ikiburudisha kwa nyimbo murua hadhira isiyoonekana. Alikuwa anaimba wimbo wa mapenzi…

*Nakupenda, nakwitaji*
*Umeniacha nateseka pekee yangu,*
*Mi nadata, mi nawaza,*
*Sijui lini mpenzi ntakupata.*

*Umeondoka, umeniacha,*
*Pekee yangu nateseka duniani,*
*Mpenzi wangu, uko wapi?*
*Niambie huko ntafika.*

*Nakupenda, nakwitaji,*
*Umeniacha nateseka pekee yangu,*
*Mi nadata, mi nawaza,*
*Sijui lini mpenzi ntakupata.*

Huu ulikuwa wimbo ambao bwana Joshua alikuwa akiimba kwa hisia kali mno. Hata hivyo alifika nyumbani kwake na kuangaza huku na huku kama mtu mwenye dhamira ya kutia kitu fulani machoni. Baada ya sekunde kadhaa za kutupa jicho hapa na pale , aligeuka na kupiga hatua chache kuelekea mlango wake.

"Paaaah!" moyo wa Joshua ulishtuka. Ulishtuka baada ya kuona mlango ulikuwa wazi. Moja kwa moja akili yake ikamwambia labda wezi wamevamia nyumba yake kuiba. Loh! Sijui wangeiba nini pale! Alihisi kuchanganyikiwa, alichukua simu iliyokuwa inatoa mwanga akaitupa mfukoni mwake na kukimbilia ndani. Giza likazidi ujanja wa macho ya bwana Joshua aliyeingia ndani kwa pupa na kujikwaa kwenye lile bati lililokuwepo chini na kuanguka juu ya mwili wa Majuma.

"Aaaih!" ilikuwa sauti ya maumivu, sauti iliyomshtua bwana Joshua. Aliinuka haraka na kujipapasa kwa mifuko yake na kutoa simu. Alimulika chini ndipo alipomuona Majuma, msichana mdogo maskini, pale chini hawezi kufanya chochote. Aliangaza hapa na pale, aliona damu zilizotapakaa pale chini.

"Oh my God!" alishtuka kwa uoga. Moyo wake ulienda mbio. Mbio zilizoupeleka moyo katika woga na huruma kubwa mno. Alisahau yote ya nyuma wala hakutaka kujua ilikuwaje hadi likatokea hili tukio na atashughulika vipi na gharama zilizojitokeza. Haraka haraka alimulika tochi ukutani palipokuwa na nguo zake. Alichukua shati moja na kulichana chana kisha alimfunga Majuma mahali palipokuwa na jeraha.

Baada ya hapo alimbeba na kumlaza kitandani kisha alipekua haraka ule mfuko aliokuja nao, alitoa dawa fulani ya maji na kumpaka usoni. Alipofanya hivyo, alitulia kama mtu anayekumbuka kitu fulani. Sekunde tano tu alikurupuka pale chini na kwenda hadi kwenye kona ya nyumba yake ile, kona iliyojazwa vitu mbalimbali. Pekua pekua yake ilmfanya atoke na pakiti fulani ya vidonge. Alichunguza vizuri kisha alirudi haraka kumnywesha mgonjwa wake. Joshua alikuwa anafanya vitu kama mwenye alikuwa akiamrishwa maana akimaliza hiki anashika kile. Sasa alikuwa anawasha moto haraka na ilipokolea alibandika sufuria na kukoroga uji tena haraka na kumpa Majuma.Usiku sana baada ya kula na kumlisha mgonjwa chakula, alikaa kitandani na kumtazama Majuma na kujisemea.

"Pole sana. Unateseka kwa sababu yangu. Sikujua kama utapata ujauzito na kuteseka hivi. Kumbe ndio maana" alijisemea huku akimtazama Majuma kisha akaendelea.

"Nishajua sasa. Hii ni dhambi na hakiki hii dhambi ndio sababu ya yote." Joshua alisema huku analia. Majuma alikuwa anamtazama tu,

kutamka hawezi. Joshua alitokwa machozi sana, machozi yalikuwa yanadhihirisha majuto na uchungu uliopo ndani yake. Macho ya Majuma ambaye alikuwa hawezi kuongea hayakupepesuka pembeni, muda wote yalikuwa kwa Joshua. Mshangao mkubwa ulimshika Majuma kwani hakujua ni kipi hasa kimemsibu baba wa mwanae anayemsubiri. Mshangao ulipozidi alitamani kuuliza lakini ikashindikana kwani sauti haikuwa inatoka na mdomo ulikuwa mzito. Joshua aliendelea kujisemea.

"Najuta kwa ubaya wangu nilioutenda kwa msichana huyu. Nina hakika asilimia mia ni ule ubaya ndio chanzo cha yale yalionikuta. Huu ubaya ndio ulionikaanga mimi" alijisemea na kufuta machozi. Hii hali ilidumu kwa muda wa masaa mawili ndipo majira ya saa nne za usiku alipanda kitandani na kujilaza vizuri kisha alimgeukia Majuma na kusema.

"Nashindwa kujua una shida gani mpaka unashindwa kuongea. Natamani uongee ili unieleze kilichokukuta hadi nakukuta umeanguka pale chini" aliongea huku anampapasa shavuni.

"Au basi ungeongea lengo tu nisikie sauti yako, tukae tuzungumze mambo mbalimbali ya kutiana furaha ambayo pengine imeyeyuka na kupotea kwa muda mrefu" aliongea hayo kwa mahaba na upendo mzito huku akimtazama na kumpapasa Majuma shavuni.Majuma alikuwa kimya tu anasikiliza na kutazama kwa makini. Alitamani kusema neno zuri, akashindwa na kuishia kumeza mate.

"Sitaki kuongea sana, lakini sina budi kukupenda na kukulea wewe pamoja na mtoto wetu. Sina budi, labda kwa kufanya hivyo kuna afueni itajitokeza kwangu." Alizungumza jambo lililomrudisha Majuma tena katika maswali mazito alioshindwa kuyauliza kutokana na kukosa uwezo wa kuongea.
"Una shida gani wewe?" lilikuwa swali la majuma lenye maneno yalioishia mawazoni tu, hakusikika.

"Muda umeenda sana mpenzi wangu. Tulale sasa, namuomba Mungu akulinde ulale na uamke salama" alisema hivyo na kumpatia busu laini la shavuni. Majuma alipenda busu ila kuomba tena alishindwa kutokana na kukosa uwezo wa kuongea.

Ilikuwa siku nyingine asubuhi na mapema kumbe bwana Joshua alishaamka kitambo kidogo. Aliwasha moto kwenye jiko ambalo juu yake lilikuwa na sufuria yenye uji. Alikuwa anakoroga kwa ajili ya mwenzake. Majuma aliamka lakini hakuinuka kitandani, hivyo aliendelea kujilaza pale huku akimtazama mwenzake anavyoendelea kuchakarika kwa ajili yake. Kila alipomtazama mawazo kemkem yalifurukuta kichwani mwake. Mawazo juu ya mambo kadha wa kadha yaliyotokea na yanayotokea. Yapo yalioshtua moyo wake, yapo yaliomkumbusha majonzi na mengine kumjaza maswali mengi.

"Kuna nini kilimkuta hadi analalamika? Alafu mbona amebadilika ghafla, ananijali na kunipenda wakati hapo jana hakutaka hata kuniona baada ya kunipiga!" Mawazo yaliendelea kupita akilini mwake kwa nguvu iliyombeba na kumfanya aelee huku na huku hadi kufikia kiasi cha kusahau ni wapi alipo.

"Mke wangu, unawaza nini? Yani nimekuita zaidi ya mara moja na husikii?" kumbe Joshua alimuita mara kadhaa ila kwa sababu ya mawazo mengi hakusikia.

"Haya ngoja nikunyanyue unywe uji" alisema na kumsogelea karibu kisha kama mtoto anyanyuliwavyo kutoka kitandani, Majuma alinyanyuliwa na kukaa. Alikaa kwa msaada mkubwa wa ukuta. Baada ya kuhakikisha kwamba amekaa vyema alianza kumnywesha uji ule ambao ulikuwa na sukari kwa mbali sana. Hakukuwa na usumbufu katika zoezi hili maana Majuma alionyesha ushirikiano mkubwa. Dakika kama ishirini na tano hivi kila kitu kilikuwa sawa ndipo Joshua aliaga na kutoka. Kwa maelezo yake ni kwamba alikuwa anaelekea sokoni mara moja kisha hatachelewa kurudi. Majuma alimkubalia kwa kutikisa kichwa.

Tangu alipotoka saa tatu asubuhi alirejea nyumbani saa kumi na mbili jioni akiwa amechoka sana. Mkononi mwake alishika kimfuko kidogo ambacho kilikuwa na Sukuma wiki. Alirudi na kujitupa chini kisha alizama katika mawazo mazito huku mkono wake akiutwika kichwani.

"Aaah! Mmmphuuu!" Alionekana kuchoka sana, alitazama huku na huko kisha akajisemea.

"Mia moja tu!" alisema na kujikuna kichwani bado mawazo yalienda sambamba naye. Majuma aliona hali ya mwenzake na kuhisi kitu lakini aliishia kumtazama tu.

"Ooh! Pole sana mamangu, nimechelewa kurudi. Ngoja nipike haraka" alisema baada ya kushtuka. Alikurupuka pale na kama kawaida yake alikuwa chapu chapu kisha ndani ya nusu saa alimaliza kupika.

Hivi ndivyo ilivyokuwa. Ni Siku ya tano tangu waanze kuishi pamoja. Kila siku asubuhi baada ya kupiga uji kwa ajili ya mgonjwa wake hutoka na kurudi jioni. Alikuwa anatoka kutafuta chochote cha kujipatia riziki. Hali ya Majuma iliendelea kutengemaa hadi ule uzito aliokuwa akiuhisi kwenye mdomo wake ulitoweka japo kidogo hakuzungumza chochote. Mwili wake nao ulikuwa na wepesi fulani kwani alikuwa na uwezo wa kuinuka kitandani na kutembea kidogo. Maisha yao yalikuwa ya kupata na kula. Siku kinapokosekana walikuwa wanalala watatu siku hiyo, Joshua. Majuma pamoja na njaa. Joshua aliendelea kutafuta riziki, kuna siku huambulia shilingi mia moja ikizidi basi ni shilingi mia mbili tu. Mambo yalikuwa magumu, anahitaji kula, mke anahitaji kula tena isitoshe mke ni mjamzito. Mambo yalikuwa magumu.

Katika hali hiyo hiyo hatimaye zilitimia wiki mbili. Majuma alikuwa vizuri hasa katika kuongea ila kutembea bado hakuwa vizuri sana. Usiku mmoja alikuwa na mwenzake ndani. Ulikuwa ni wasaa mzuri wa kumhoji hasa yale yaliobeba dukuduku lake.

"Mume wangu, tafadhali nambie ni kipi kimekukuta. Unalalamika kila siku, sasa naomba nambie, una kipi nisichokijua?" Majuma alisema kwa sauti ya upole. Bwana Joshua alimtazama na kukaa kimya kwa dakika kadhaa kisha alivuta pumzi na kusema.

"Ni makubwa kwa kiasi chake" alisema na kuendelea.

"Najua unafahamu kuwa mimi ni kondakta wa magari yanayoenda mikoani. Si hivyo tu, pia mimi ni dereva wa magari hayo. Kuna magari ya kampuni moja yanayoshughulika na usafiri wa Nakuru kuja Kakamega nilikuwa nafanya kazi nao kama kondakta, kisha dereva mpaka siku za hivi karibuni. Nilikuwa nalipwa vizuri. Shida ilitokea baada ya kusingiziwa kwamba nimeiba pesa za kampuni hiyo, nilisingiziwa. Sasa tangu siku hiyo nilifukuzwa hata bila kufanyika uchunguzi wowote."

Alisema.

"Lakini ungeahamia kampuni nyingine, maana ni nyingi tu" Majuma alishauri.

"Nilifanya hivyo, lakini cha ajabu nilinyimwa hata ukondakta. Kwa sasa naishi tu kupiga debe, hivyo siku nyingine napata mia moja tu"

"Mmmh! Usijali mume wangu, mambo yatakuwa sawa"

"Yatakuwa sawa endapo utanisamehe maana naona ile dhambi na laana ya jambo nililokufanyia inanitafuna." Joshua aliongea kwa huzuni sana. Majuma alifuta machozi. Huzuni ikatanda na kuzaa kilio cha kwikwi ndani ya nyumba ile.

Siku mbili zilipita huku mambo yakiendelea kuwa magumu kwa Joshua. Asubuhi moja aliaga kama kawaida yake, alitoka na kuelekea kwenye mihangaiko yake. Ilikuwa ni mazoea kwa Majuma kumuona mume wake akitoka asubuhi kisha inapofika saa kumi na mbili anarudi lakini siku hiyo hadi saa mbili za usiku bado hakurudi.

"Labda atarudi, muda bado" Majuma alisema. Ilikuwa saa tatu za usiku lakini hapakutokea mtu hadi ikafika saa sita usiku na usingizi ukamchukua.

"Mke wangu" Majuma alisikia akiitwa, alikurupuka toka usingizini na kutazama huku na huku lakini hakumuona mume wake. Hiyo ilikuwa saa nane usiku.

Woga ulimshika Majuma baada ya kuamka na kumkosa aliyemuita. Upande fulani wa akili yake ulimnong'onezea kuwa ile sauti ilikuwa ya wachawi au majini. Hii fikra ilizaa woga mkubwa wakati huo upande mwingine wa akili yake ulimwambia kwamba ile sauti aliiskia kwenye ndoto tu. Licha ya wazo hili kuwa na aslimia nyingi katika uhalisia, nafsi yake haikutaka kuridhika na wala haikuwa na nguvu tena za kupambana na hali ya woga uliotawala moyo wake. Alijifunika gubigubi. Mawazo nayo hayakutaka kumuonea huruma hata kwa kiasi kidogo, yaliendelea kukiandama kichwa chake kwa hoja zisizoisha pamoja na maswali yaliokosa majibu hasa juu ya mume wake. Yuko wapi?

Unadhani alipata hata chembe ndogo la jibu? La hasha! Hakupata. Tangu alipoamka saa nane usiku hakulala tena kwani usingizi nao ulitoweka baada ya kufukuzwa na nguvu kali ya mawazo ikishirikiana na nguvu ya uoga. Sekunde, dakika hatimaye masaa yalisonga kwa

kujikokota sana, ilikuwa saa tisa. Majuma hakupata hata lepe la usingizi. Mida ya saa kumi na dakika kumi na tano hivi, ndipo kwali alianza kuhisi ushawishi wa usingizi ukitekenya macho yake. Macho yalilegea, macho yalikosa nguvu ndipo taratibu akayafumba na kulala unono. Alilala fofofo kama mtoto.

Lakini hata hakuufaidi usingizi wake aliochelewa kuupata kwani saa kumi na mbili tu, aliamka kutokana na mlio mkali wa sufuria iliyoanguka chini. Aliamka akiwa amenuna huku anasonya kwa hasira kwani hakupenda kuamka ule muda. Aliyaangaza macho yake huku na huku ambayo bado yalikuwa na usingizi mzito. Alifikicha na kupiga muayo mrefu kisha akili ilimuelekeza kuangalia chini. Hakuamini alichokiona, moyo wake ulivunjika kabisa huku kitu kigumu kama tonge au funda la maji likimkaba shingoni. Haya yote yalitokea punde alipoona unga wake uliotengwa kwa ajili ya kiamshakinywa.

"Yani mipanya ya humu ndani jamani! Sasa mimi nitakula nini ah!" aliongea na kuupeleka mkono wake wa kushoto kwenye shavu lake kwa lengo la kufuta machozi maana alishindwa kabisa kujizuia asilie.

Linapotokea jambo mbaya hupelekea akili ya mtu kukumbuka hata mabaya mengine yaliyowahi kutokea hata miaka kumi ya nyuma ili tu kumliza zaidi. Majuma alikaa chini na kuanza kulia kwani alikumbuka mambo mengi ya kuumiza moyo wake. Unadhani ni kumbukumbu ipi yenye kionjo cha furaha kwa Majuma? Alilia kilio cha kwikwi msichana wa watu. Kila kinachotokea kinamfanya aone labda jana ilikuwa afueni. "Jikaze, inuka" hii ilikuwa sauti iliyosikika kwenye nafsi yake ikimtia nguvu. Alifuta machozi na kusimama kisha aliangalia huku na huku mfano wa mtu mwenye kutafuta kitu fulani. Alichukua kikombe na kuchota maji ya kunawa uso na baada ya hapo aliingia mtaani kwa lengo la kumtafuta mwenzake au hata kuuliza kwa watu juu ya kilichomkuta mume wake.

Lakini sasa atamuuliza nani ambaye labda atakuwa anamfahamu bwana Joshua? Majuma alijipa faraja kwamba yote yanawezekana tu kwani Mungu si athumani, atampata tu wa kumuuliza. Aliendelea kutemmbea mara kadhaa akilitazama tumbo lake lililokuwa linadhibitisha kwa uwazi kwamba kuna binadamu aliyekuwa akiishi humo. Hakujua ni wapi pa kuanzia lakini aliona ni heri aingie sokoni

kwanza kisha aende maeneo ya stendi za magari. Alitembea kwa kujivuta hadi sokoni na kuanza kuuliza uliza kwa watu aliokuwa akipishana na kukutana nao.

"Brother! Brother! Kidogo tu" Majuma alisimamisha kijana mmoja aliyekuwa anapita karibu yake.

"Enh, unasemaje mama"

"Samahani! Unamjua mtu anayeitwa Joshua?" Majuma aliuliza

"Joshua yupi?" yule kijana aliuliza. Majuma aling'atang'ata kwa sababu hakuwa anajua jina la pili la Joshua. Yule kijana alicheka kisha akauliza. "Hata picha yake huna?" "Hapan..picha yake…ndi..io sina" Majuma aliongea kwa kigugumizi, aliogopa kuchekwa tena.

"Kweli wewe ni mshamba. Unamtafuta mtu kiushamba shamba tu hivyo!" yule kijana akamcheka kwa dharau na kuondoka. Majuma alivunjika moyo sana ila angefanyaje? Aliamua kuendelea na zoezi lake japo aliogopa kuuliza tena. Alizunguka maeneo ya sokoni akiwa kimya kabisa.

Ilikuwa saa tano asubuhi, Majuma aliamua kujigongoja tena kuelekea stendi ya magari. Alizunguka hapa na pale huku hofu yake ikiwa ni ile ile ya kutowauliza watu. Alizunguka sana bila mafanikio ndipo alipojiuliza kwamba atazunguka kimya kimya hivyo hadi saa ngapi? Aliamua kuuliza, liwalo na liwe.

"Kaka" aliita kwa wasiwasi mkubwa.

"Oya sister unaenda? Gari ndilo hili linatoka sasa hivi. Fanya haraka twende" yule kijana aliyeitwa na Majuma aliongea, kumbe alikuwa kondakta. Majuma alimsogelea haraka na kumhitaji wasonge pembeni kodogo.

"Samahani sana ndugu yangu"

"Haina issue sister, we ongea tu"

"Mi naomba nikuulize kitu. Sijui unamjua Joshua?" Majuma aliuliza.

"Joshua yupi? Huyu Joshua konda?" yule kijana aliuliza. Majuma alitafakari kidogo na kukubali ni yeye huyo anayemuongelelea japo hakujua kulikuwa na Joshua wangapi katika kazi hiyo.

"Ndio huyohuyo namuulizia"

"Huyo amemkimbia mke wake" yule kijana alisema jambo lililomshtua Majuma

"Yule ni rafiki yangu sana, juzi alinambia kuwa hana budi kukimbia na kwenda mbali maana maisha yake mwenyewe ni magumu alafu ameongezewa mzigo mwingine. Ameongezewa mwanamke tena mjamzito" alisema kisha alishtuka kusikia sauti ya gari.

"Dada tungeongea zaidi ila muda hatuna." Alishika mfukoni mwake na kutoa kitu.

"Hapa kuna barua aliyoiacha, naomba umpe mkewe. Kwaheri sister" aliondoka. Maskini Majuma! Aliamua kufungua hiyo barua ili ajue ni taarifa gani iiyomo, huenda kuna maagizo ameachiwa ya kumfariji kwa maisha.

*JOSHUA MATENYA,*
*S.L.P2619,*
*KAKAMEGA.*

*6/7/2021.*

*Mke wangu,*

*Najua taarifa za kupotea kwangu zimekupa wasiwasi. Ni kweli kwamba nimesalimu amri na nimekubali kushindwa katika hili. Nimeamua kuchukua uamuzi huu japo ni wa kinyama. Uko na haki ya kumwambia mtoto wangu chochote kile kuhusu mimi babake. Ila kama utafaulu na kuleta mwanetu kwa ulimwengu huu, naomba usiwe mkatili kwake kama mimi babake. Naomba umpe jina la Nyota kama ni wa kike ambaye ni marehemu mamangu, ama Matenya kama ni wa kiume ambaye ni babangu mzazi.*

*Pole sana mke wangu, kwaheri ya kuonana. Nakutakia maisha mema.*

*Mimi msaliti*

*Joshua.*

Maskini Majuma alikuwa amekimbiwa na mume wake bila kujua ni wapi amekimbilia. Ataishije peke yake! Nguvu zilimuisha njaa nayo

ilianza kumsumbua. Alijikaza kutembea kurudi nyumbani lakini hakufika mbali sana, alijikwaa na kuangukia ungo mkubwa uliokuwa na mchele wa kuuzwa. Majanga zaidi yalitokea bila kumuonea huruma licha ya yote yaliyomkuta kipindi cha nyuma na muda mfupi uliopita. Mkono wa kulia mkubwa na mgumu wa bwana Mauzo, yule muuzaji wa mchele ulimshika Majuma huku ule wa kushoto ukishusha makofi mazito usoni mwake. Majuma alipigwa makofi mazito yaliyoharibu na kuvunja vunja kabisa ile nguvu ya kuzuia kilio na machozi. Majuma alilia sana.

“Wewe ni mpumbavu! Kama unajua una mawazo kwa nini usikae nyumbani kwako tu?” Mauzo alifoka na kurusha kofi lingine lililotua kwenye uso wa Majuma.

“Nisamehe ndugu yangu, ni bahati mbaya. Nisamehe” Majuma alilalamika huku akizuia uso wake kwa mkono ili asipigwe kofi nyingine iliyokuwa imerushwa kwa nguvu. Kuzuia kwake hakukufua dafu, kofi ilinasa shavu lake.. Wapo waliokuwa wanashangilia Majuma kupigwa lakini pia walikuwepo waliiomuonea huruma.

“Kama kumpiga ushampiga vya kutosha. Muache sasa” kijana mmoja kwa jina Shariff alisema.

“Haiwezekani nimuache, ameharibu biashara yangu. Nimuache kisha faida yangu itakuwa ipi? Nafaidika nini?” Mauzo aliongea kwa hasira.

“Sasa ukimpiga faida itapatikana?” Shariff aliuliza.

"Muache ampige ili siku nyingine awe makini akitembea. Sio kutembea tembea tu kama mlevi. Afinyweee!” zilikuwa sauti za wapita njia waliosimama na kutazamabsinema hiyo. Kipigo kilichoendelea kilisababisha huruma kubwa kwa baba mmoja aliyekuwa amefika eneo hilo muda machache.

"Bwana we, kuwa na busara ya kutafuta suluhisho ndugu yangu. Sasa hata ukimpiga nini kitaendelea kwa biashara yako? Tusiongee sana, biashara yako ilikuwa inagharimu shilingi ngapi?” yule baba kwa jina Ridhaa aliuliza.

“shilingi mia saba”

“Ok,” alisema kisha alitoa waleti yake na kutoa shilingi elfu moja, alimpa yule muuzaji.

" Ile mia tatu ni ya kuuzoa huo mchele kisha weka kwenye kiroba na umpe msichana huyu" bwana Ridhaa alizungumza. Majuma hakuamini alichokiona na kukisikia siku ya leo. Katika kumbukumbu zake hii ilikuwa mara ya kwanza anaona afueni moyoni mwake maana saa nyingine zote ni simanzi na maumivu yasiyoisha.

"Baba sijui nikushukuru vipi. Mungu akubariki sana baba yangu. Hakika umenisaidia sana, naona Mungu amekutumia kuniokoa kwa hili." Majuma alisema.

"Ondoa shaka binti yangu. Wewe ni mtoto wangu, siezi ona unanyanyaswa nikakuacha. Sisi ni binadamu na tunapaswa kusaidiana." Bwana Ridhaa aliongea na kumgeukia muuzaji. "ni kilo ngapi hizo?"

"Zilikuwa kilo nane" yule muuzaji alijibu.

"Najua hawezi kubeba hizo zote kutokana na hali yake, muitie bodaboda ampeleke hadi kwake." Yalikuwa maelezo kutoka kwa bwana Ridhaa.

Majuma alifika nyumbani na kutulia huku akiwaza hili na lile. Mawazo juu ya yaliomkuta huko sokoni yalisumbua kichwa chake. Alienda kufuata nini sokoni? Kumbukumbu zake zilirudi juu ya mume wake, alikumbuka alichoambiwa na alichokisoma kuhusu kutoroka kwa mwenzake.

"Hivi ni kweli umeamua kuniacha? Joshua umeamua kunitoroka?" Majuma aliongea huku analia. Kuamini hili suala ilikuwa vigumu sana. Nguvu zilikuwa zimemuisha, alipokaa ni palepale kwani kuinuka ilikuwa shida. Njaa aliyokuwa nayo ilimpa nguvu ya kujaribu kusahau hayo. Aliinuka na kwenda kuwasha moto kwa ajili ya kupika. Alipika wali wa mchele alioumwaga sokoni.

Baada ya kula chakula chake shida ilirudi palepale. Mawazo, machozi na kilio vyote vilikuwa upande wake. Alilia hadi alipoona machozi yamekauka na yamekataa kutoka tena. Usiku uliingia, alitamani kulala lakini maumivu yaliyokuwa yanautafuna moyo na mwili wake yalimfanya akose hata lepe la usingizi. Ulikuwa usiku wa taabu na mateso akilini mwake. Alihisi kama dunia yote na uzito wake imeelemea upande wake yeye kwani mambo yalikuwa mazito na uzito wenyewe ni mara mia

ya uwezo alionao. Akahisi huenda alihukumiwa na dunia kuhusu dhambi za wanadamu wote.

# SURA YA SABA

Ilikuwa siku nyingine, kule kwa akina Rehema sasa. Mume wake alimuita na kukaa naye kisha alianza kumwambia

"Nilikuwa nakusisitiza siku zote hizi kwamba uandae siku ya kwenda kumuona rafiki yako" Mafutu alisema.

"Ni kweli mume wangu. Ila kesho nitaenda usijali." Rehema alimjibu mumewe kwa upole na sauti ya mahaba.

"Sawa. Unajua hupaswi kukaa mbali naye kiasi hicho wakati hujui anaishije." Aliendelea na kuuliza " na mbona usiende leo?"

"Leo nataka kwenda kumuona mama Esta, si unajua anaumwa." Rehema alijibu.

Mafutu alisisitiza sana. "Huko utaenda lakini kwanza pitia kwa mwenzako umuone." Rehema hakuwa na budi ila kuanza kufanya maandalizi ya kwenda kwa rafiki yake Majuma.

Majira ya asubuhi hiyohiyo alitoka nyumbani kijijini Maraba na kuanza safari ya Murumba anakoishi Majuma. Safari ilikuwa ya miguu hivyo basi alitumia takriban saa moja kufika kwa Majuma. Walisalimiana kwa furaha maana wiki kadhaa ilikuwa imepita bila wao kuonana. Baada ya kusalimiana walitagusana kuhusu hili na lile kwani mazungumzo mengi yalianza kuchukua nafasi. Walizungumza mambo mengi sana hasa baada ya Majuma kueleza yote yaliyotokea na jinsi alivyokimbiwa.

"Mmmmh! Utaweza kweli kuulea ujauzito na kumlea mtoto atakapozaliwa? Si jambo dogo, we mwenyewe ona baba wa mtoto hayupo alafu hali yenyewe ya hapa nyumbani ndio kama unavyoiona. Utaweza?" Rehema aliuliza.

"Mimi wazo langu ni wewe kutoa hiyo mimba" lilikuwa wazo la Rehema ambalo hata chembe yake ndogo haikupokelewa. Majuma alikataa katakata na kwa hali hiyo Rehema aligombana na mwenzake hadi

kufikia kutupiana maneno ya kashfa. Wazo la Majuma kumtembelea mamaye likamjia akilini, alikumbuka kuwa damu ilikuwa nzito kuliko maji.

******

Kutoka mahali anapoishi hadi sokoni ni mwendo wa dakika ishirini hivi lakini yeye alitumia dakika 50 kutokana na uchovu uliosababishwa na ujauzito alionao. Alijijikaza hivyo kwa mwendo wa kobe na hatimaye alifika. Jambo la kwanza kufanya baada ya kufika sokoni lilikuwa ni kutafuta mahali penye upepo kisha alijipweteka chini, aliupumzisha mwili kwa dakika kadhaa huku akihisi kunogewa. Ladha tamu ya pumziko lile ilimfanya ang'ang'anie pale chini bila kuinuka.

"Mmmh! Binti Majuma acha uvivu. Utakula nini?" alitamka maneno hayo yeye mwenyewe na kunyanyuka kisha alichukua ndoo yake na kuanza kuzunguka sokoni.

Zunguka yake ya muda mrefu haikuzaa matunda hata kidogo kwani sehemu zote alizoenda akiwa na uhakika wa kuwaona wanadada wa kufua, hakuwaona.

"Au leo sio siku ya kufanya kazi hii?" alijiuliza bila majibu. Alibaki pale ameduwaa na kuzubaa, akili yake haikujua kipi cha kufanya.

"Ama washafua na kuondoka?" alisema na kugeuka haraka mara baada ya kusikia sauti ya mzee aliyekuwa anafoka.

"Wewe mama utagongwa! Huoni sisi tunapita kwa kasi" aliongea mzee aliyekuwa juu ya baiskeli.

"Samahani baba" Majuma aliongea baada ya kuruka pembeni kidogo palipokuwa na kidimbwi cha maji. Alipepesuka lakini hakuanguka, japo maji machafu yalimrukia na kusababiaha aonekane mchafu. Watu walicheka. Majuma alijivuta na kuondoka mahali pale maana balaa ilianza kumfuata nyuma kwani kwake ilikuwa dalili ya mvua siku zote. Hakutaka kupepesa macho wala kushangaa shangaa sana, alienda moja kwa moja akipiga hatua hadi eneo ambalo watu wanatumia kama sehemu maalum ya kufanya kazi ya udobi. Hakika lilikuwa jambo la kheri na furaha kubwa baada ya kuwaona wanadada waliokuwa wakishughulika na kazi.

Tumaini jipya liliingia ndani mwake lakini angeanzia wapi kwenda kuungana nao? Msichana wa watu hakujua hata utaratibu uliopo mahali hapo katika kazi hiyo. Aliamua kuweka ndoo chini na kukaa juu yake huku macho yakiwa kwa hawa wenzake. Alitamani sana ila aliishia kumeza mate.

“Nitakaa hapa hadi saa ngapi?” alijisemea na kuinuka pale. Alipiga hatua za taratibu zilizojaa wasiwasi mkubwa. Alielekea karibu na dada mmoja aliyejiinamia akifanya kazi yake kwa ustadi.

“Dada shikamoo!” Majuma alitoa salamu. Yule dada alimtazama bila kuitikia.

“Samahani dadangu” Majuma aliendelea…” naweza kufua hizo nguo nyingine name nipate pesa?”

“Yani nguo nilizochukua kuzifua kwa faida yangu nikupatie wewe? Wakati sisi wenzako tunaamka mapema na kuwahi wateja wewe ulikuwa wapi?” yule dada alifoka kwa hasira. Majuma alikosa cha kujibu.

“Mijitu mingine ipo kukorofisha wenzao tu! Hebu kwanza nitokee hapa, unanitia kichefu chefu” yule dada aliongea kwa sauti kubwa hadi wale wenzake walisikia na kutoa kicheko cha umbea. “Hahaa haloooo, haloooo!"

Majuma alishangazwa sana na hili jambo maana kumuomba kazi ndio kumepelekea haya maneno yote. “Watu wengine wamekosa busara” alijiambia na kuanza kusonga pembeni. Uso wake ulishikwa na aibu sana, hakujua aondoke ama abaki. Akiondoka atakula nini siku hiyo? Hili swali tu ndio lilimnyima raha, na si kumnyima raha tu bali pia lilimfanya ashindwe kuchukua uamuzi wa moja kwa moja juu ya kuondoka. Aliweka ndoo chini na kuikalia bila kujua mbona aliketi. Je, kusubiri huruma ya hawa wanadada au kusubiri wateja? Majuma alichanganyikiwa.

Muda nao si rafiki siku zote, wenyewe unasonga bila kujali kuwa mambo kadhaa hayajatekelezwa sawa kwa dakika chache au nyingi zilizopita. Ilikuwa saa saba mchana, tumbo nalo lilianza kumkumbusha kuwa ulikuwa muda wa chamcha hata baada ya kukosa kutia kiamshakinywa mdomoni. Tumbo lilizidi kukoroma na kusababisha Majuma kujihurumia. Hakupenda mwanawe apate shida kama anavyopata yeye. Aliamua kusimama ili atembee huko na huko kwa lengo

la kwenda kuomba hata kipande kidogo cha muhindi wa kuchoma. Wakati anasimama ili kuondoka alishangaa kumuona baba mmoja akileta lundo la nguo zake.

"Jamani, mimi leo nimeishiwa yani nina mia mbili tu. Naombeni msaada tu wa kufuliwa nguo hizi!

"Aah! Hajaishiwa wala nini. Kila siku hio ndo tabia yako. Yani nguo za mia nane au mia sita wewe unalipa mia mbili? Leo hatutaki." Dada mmoja alilalamika.

"Kwa hivyo niondoke na pesa? Sio busara mabinti wangu, tusaidiane kwa hili" yule baba aliomba

"Leo hakuna cha msaada wala nini. Kama unataka kufuliwa nguo toa mia nane, ukishindwa ondoka na nguo zako, kama vipi mpe yule msichana pale" baada ya kuambiwa hayo yule baba aligeuza shingo na kumtazama yule msichana. Msichana mwenyewe alikuwa ni Majuma aliyepata faraja na matumaini makubwa sasa, alimeza mate kwa furaha.

Baba yule alipiga hatua kuelekea alipokuwa Majuma na kumtazama. Ajabu baada ya kumtazama hakumpa nguo wala kumwambia chochote zaidi ya kutema mate.

"Huyu mzee ndo afue nguo zangu? Ukiangalia ndoo yenyewe ni kama ameikota sijui wapi, yani hata akisema atafua bure, sipo tayari kwa kweli" yule baba alisema na kutema mate tena. Ile kauli ilipenya vizuri kwenye matundu ya masikio ya Majuma, na haikuishia kupenya tu bali pia iliharibu na kuvuruga vuruga mifumo yake ya usikiaji. Alihisi hakusikia vizuri lakini alivyosikia ndivyo ilivyokuwa. Nguvu zake za uvumilivu zilirarulliwa na kulipuka vibaya kutokana sauti aliyoisikia, machozi nayo yalimkosea heshima, yalianza kutengeneza mifereji usoni mwake. Mkono wake wa kushoto ulishika Kamba iliyofungwa kwenye ndoo wakati huo mkono wake wa kulia aliukunja usoni mwake na kuanza kutembea huku akijililia.

Majuma aliona dunia haina huruma kabisa kwani haikurithika na mabaya yote yaliomkuta. Mbaya zaidi, hakujua mbona siku zote ziligeuzwa machozi na majonzi bila kuwekewa wazi kosa alilolitenda. kosa lake ni lipi hadi anakumbwa na balaa kama hizo? Alitembea kwa

haraka huku nyuma akiacha vicheko vikali vyenye kumtia aibu mtu yeyote yule.

Alipofika chumbani alikuwa mwingi wa uchovu basi hakujali wala kubali atakula nini. Majuma alijitupa kitandani ambacho pia kililalama kuchoshwa kila sekunde. Alilia sana mpaka machozi yakamkauka machoni mwake, koo na kichwa vilivyokuwa vinamuuma, vyote hivi vilimjuza kwamba amelia vya kutosha basi apumzike.

"Leo ningefanya kazi ile ningepata pesa ya kununua chakula nile na mwanangu." Alisema na kushika tumbo lake kubwa kisha ghafla alikumbuka maneno ya yule mzee. Aliumia sana, maumivu yalizaa kilio kwa mara nyingine. Usiku ulikuwa mrefu baada ya kulalia mate.

Siku ziliendelea kusonga huku taabu na masaibu ya dunia yakiendelea kumwandama Majuma siku nenda siku rudi. Binti aliyekuwa kimanzi hurulaini wa peponi leo alionekana kama bikizee kwa sababu ya taabu za dunia.  Bahari ya umaskini ilikuwa imemmeza Majuma hana bee wala tee na siku zote unjejua kuwa haungami.

Kwake Maisha yalikuwa yamemwendea segemnege na kuwa mfano bora wa walalahoi pale kijijini kwani maisha yalikuwa magumu zaidi hasa kwa mwanamke mjamzito kama yeye. Licha ya unyanyapaa ambao alifanyiwa na watu, hakukata tamaa ya kuwafuata ili kuomba chochote cha kula au kuomba kazi ya kufanya.

Mungu si athumani. Baada ya zunguka zunguka Majuma alifanikiwa kupata kazi ya kuosha magari pale stendi. Hakutaka kujali ikiwa Ile Ilikuwa kazi ya kufanywa na wanaume kwani kwake ilikuwa bahati ambayo hakuiamkia bali aliitafuta kwa muda mrefu. Ilikuwa kazi inayofanywa na wanaume lakini angepata wapi nguvu ya kuchagua kazi? Alifanya kwa moyo wote huku akijipatia vipesa kadhaa japo havikutosha Ila aliona afadhali kuliko kulalia mate siku zote.

Alikumbuka riwaya moja iliyoandikwa na mwandishi wa kike kwa jina Assumpta Matei. Alimkumbuka vizuri mhusika Ridhaa humo ndani. Ridhaa alipokuwa anatoka katika msitu wa Mamba baada ya miezi sita, alijiona nafuu na hata alipomtazama mwamu wake Kaizari alijiambia "heri nusu shari kuliko shari kamili" hii ndio ilikuwa kauli ya binti huyu,

ilimtia matumaini. Majuma aliweza kujilinganisha na Ridhaa kwani wote walikuwa wamepitia mengi katika ulimwengu wa kutengwa

Siku zilisonga kwa kasi nayo hali ya Majuma ikawa tofauti. Hatimaye ulifika wakati wa kumleta mtoto kwenye uso wa dunia, dunia isiyo na huruma kwa upande wake.

"Mwanangu naona unakaribia kuja. Kama ningekuwa na uwezo ningezuia usije, ubaki huko uliko maana huku duniani ni mateso. Mama yako nateseka sana." Miezi ilifika lakini hakuwa na ndugu wala jirani atakayempeleka hospitalini. Hela aliyokuwa anapata ni kidogo na haikutosha kwa mlo mzuri wa siku hivyo hakubaki hata na akiba ndogo. Kwa hali kama hiyo wasiwasi mkubwa ulitawala kichwa chake. Atafanyaje? Hakuacha kwenda kwenye kazi yake.

"Najua siwezi pata leo uchungu. Naamini bado, kwa hivyo sina budi kwenda kuosha hata gari moja nipate pesa ya kula leo." Alisema na kujivuta hivyo hivyo hadi stendi anapooshea magari siku zote. Aliwakuta vijana wa kiume ambao tayari walishazoeana sana. Alijiunga nao kuosha magari lakini kadri muda ulivyoenda mbele ndivyo hali ilivyozidi kuwa mbaya na mwisho alihisi uchungu tumboni ghafla bin vuu alipiga unyende mkali. Vijana wale walishangazwa na tukio hili ila hawakutaka kushangaa mara mbili, walimbeba hadi kwenye gari ndogo aina ya tuktuk na kumpeleka Kakamega General Hospital. Haraka haraka aliingizwa kwenye chumba cha kujifungulia, madakdari walianza kazi yao. Baadae kidogo wale madaktari watatu walisonga pembeni na kuanza kuteta jambo. Majuma aliyekuwa anaugulia uchungu mkali alimsikia daktari mmoja akisema kwa sauti ya chini.

"Inaonekana mtoto amekaa vibaya hivyo haitawezekana kutumia njia ya kawaida. Njia iliyopo ni kumfanyia CS la sivyo tutampoteza mtoto au hata wote wawili."

Moyo wa Majuma ulimwenda mbio, siku zote alimwomba Mungu asijipate kwenye chumba cha upasuaji. Pale kitandani Majuma alitamani kunyanyuka akikimbie kitendo ambacho kingefanyika kwake muda mfupi ujao.

"Jamani daktari nawaomba msinifanyie hivyo mimi. Nitaishije na hali ile?" Majuma aliongea huku analia. Madaktari waligeuka na kumtazama. Mshangao uliotawala nyuso zao ulidhihirisha kwamba

hawakutegemea kama angeweza kusikia mazungumzo yao ya siri. Daktari aliyeonekana kama ndiye mkuu alimsogelea taratibu na kutulia kidogo huku akimtazama.

"Unalia nini dadangu?" aliuliza kwa sauti ya upole iliyojawa na adabu na ustaarabu.

"Nakuomba doctor msinifanyie hivyo, nakuomba" Majuma aliendelea kulalamika

"Tusikufanyie nini dada?" aliuliza tena na kumwacha Majuma akibabaika kujibu swali hili. Alijikaza na kujibu

"Naomba msinifanyie upasuaji. Nitaishije mimi na sina mtu wa kunisaidia maishani mwangu"

"Hauna mtu wa kukusaidia? Wale waliokuleta ni nani?" daktari aliuliza ila ghafla wazo lilimjia na kujiona hayuko sahihi kuendelea kumhoji maswali wakati hali yake si nzuri. Alitoka kwenye chumba kile, kisha wenzake walitoka pia.

Mateso makali yalikuwa yanausakama mwili wa Majuma, kila sehemu ya mwili wake ilikuwa inawaka moto kama inachomwa na msumari wa moto. Alipokumbuka alichokisema daktari, nguvu zilimuisha. Machozi yaliyomtoka yalikuwa ya mateso na maumivu yaliyochanganyika na matokeo ya maswali yaliyopita akilini mwake.

"Nani atanisaidia wakati nauguza kidonda cha upasuaji? Nani atafanya kazi kwa ajili yangu? Nitashinda nyumbani? Nitakuwa nakula nini?" alijiuliza hayo na kukumbuka kuwa hata ingekuwa sio operation bado tu angebaki nyumbani kwa siku kadhaa hadi mtoto afikishe umri wa siku fulani. Aliona ujio wa mtoto badala ya kusababisha furaha, utaungana na mengine ya dunia katika kuhakikisha kwamba analia, anateseka na kutaabika. Aliukumbuka ushauri wa rafiki yake Rehema juu ya kutoa ule ujauzito, lakini hakuthubutu hata kutamani kwamba angefanya hivyo. Machozi hayakukauka machoni pake.

Basi baada ya muda mfupi baadae madaktari waliingia wakiwa na vifaa vya upasuaji. Majuma alipowaona tu kilio kiliongezeka zaidi na kuanza kulalamika kwa sauti.

"Mungu wangu, mbona unaniacha kiasi hiki? Kwa nini hata katika hili pia unaniacha? Naenda kukatwakatwa mimi, sijui ntakufa au

nitaponea. Ila najua nisipokufa cha moto nitakiona!" Majuma alilia sana. Madaktari hawakutishwa na kilio chake, walisogea na kuandaa bomba la sindano ya usingizi ili kumchoma kabla ya kuanza kazi.

"Hivi kweli hamnionei huruma mwenzenu? Ni heri mniache tu nife kuliko mateso mnayotaka kuniongezea. Nateseka sana mimi na nitateseka zaidi mkifanya hivyo." Majuma aliendelea kulalamika huku akilia ila nani angemuonea huruma? Madaktari walikuwa kazini. Dokta mmoja mpole aliingiza mkono mfukoni na kutoa kitambaa, alifuta chozi lililokuwa linadondoka usoni pake. Baada ya yote hayo walivaa gloves na kuweka kila kitu sawa kisha walimchoma sindano ya usingizi ambapo hazikupita dakika nyingi alipatwa na usingizi mzito sana.

"Inaonekana mama huyu alikuwa hapumziki katika kipindi chote cha ujauzito wake. Hapo ndio tatizo limeanzia" doctor alizungumza. Upasuaji ulianza rasmi. Kazi hii ilifanyika kwa umakini huku ikichukua muda mrefu sana kuikamilisha. Naam! Mungu si athumani na hatawai kuwa athumani kwani madaktari walifaulu kumtoa mtoto akiwa salama. Alikuwa mtoto wa kike ambaye baada ya kufanyiwa vipimo vya kitaalamu kama yupo hai au la basi aligundulika yuko hai. Mtoto alikuwa akilia sana lakini halikuwa jambo la kushangaza wala kuogopesha kwani ni jambo la kawaida na la faraja mtoto kulia punde tu akizaliwa.

Daktari mkuu alitoka na kuwaacha wengine mle ndani. Masaa yaliendelea kusonga mbele huku mtoto akiendelea kulia hadi madaktari walibaki kushangaa. Mtoto mdogo tu nguvu za kulia muda wote anazitoa wapi? "Labda ana njaa anahitaji kunyonya" daktari mmoja alisema lakini mtoto angenyonya wapi wakati licha ya masaa mengi kupita bado mama yake hakuamka.

"Haya ni matatizo sasa. Atanyamaza vipi huyu sasa? Alafu kwa kawaida ilitakiwa nguvu ya ile dawa ya usingizi iwe imeisha. Sasa hadi wakati huu ni masaa matatu hajaamka" daktari mwingine aliongea kwa wasiwasi. Wakati wanaendelea kuumiza kichwa juu ya nini cha kufanya ghafla daktari mkuu aliingia na kuanza kuangalia angalia vitu alivyovifahamu yeye mwenyewe. Ghafla alishika kichwa na kutamka kwa nguvu.

"Mungu wangu!!!! Tumekosea, hebu njooni haraka. Tunaeza tukampotesa" daktari alisema na kuonekana kama mtu

aliyechanganyikiwa mara baada ya kuhisi wamemshona Majuma ile sehemu waliyoikata wakati huo mkasi upo ndani yake. Yani wamemshona bila kufahamu kuwa mkasi upo tumboni mwake. Vichwa vya madaktari viliwaka moto, kila mmoja hakujua ni uzembe gani aliofanya yeye au mwenzake aliyekuwepo hapo. "Hii inastaajabisha, yani sisi wote tumesahau kifaa ndani ya mwili!" daktari mmoja kwa jina Akala aliongea akidhihirisha wasiwasi alionao juu ya uhalisia wa jambo lililotokea. Akilini aliamini si bure.

"Inabidi tu tumuongezee shindano nyingine ya usingizi la sivyo wakati tunafumua nyuzi anaweza kuamka" daktari mkuu kwa jina Jason alisema. Zoezi lilianza huku wakijua kabisa hatari iliyokuwepo ya kufumua nyuzi ambazo zilishonwa muda mfupi uliopita. Haikuwa sahihi kwani usalama wa mgonjwa huwa mdogo sana lakini madaktari wangefanyaje? Walimchoma sindano nyingine na kuanza kufumua nyuzi kwa umakini mkubwa huku kila mmoja akiomba Mungu asimame katika hilo maana hatari ilikuwa waziwazi.

Mtoto aliyezaliwa alikuwa analia sana ungedhani alikuwa anajua au kuhisia kitu alichokuwa akifanyiwa mama yake. Mama ambaye hakuwa na ndugu ama jirani ambaye wangekuwa wote hapo. Kazi iliendelea huku dakika zikikatika na kutimia masaa mawili tangu kazi hio ianze. Walifanikiwa kuutoa ule mkasi uliokuwa umebaki tumboni mwa Majuma. Kufikia sasa kidonda kilikuwa kikubwa sana, damu nazo zilitoka kwa wingi. Majuma alipoteza damu nyingi.

"Tafadhali nipatie dawa angalau tukaushe hiki kidonda kidogo." Doctor Jason alisema na kutikisa kichwa mithili ya mtu mwenye masikitiko. "Alafu huyo mtoto naomba mfanye mpango wa kumsaidia. Si vizuri kulia kiasi hicho hadi sauti imempotea" Jason aliongezea.

Dawa ililetwa kwa haraka, Majuma alipakwa. Dakika ishirini mbele alianza kushonwa kwa mara nyingine.

"Hatari ipo kubwa sana kwake, hapaswi kufanya kazi ngumu au chochote kitakachohitaji kujitutumua maana hizo nyuzi tumezishona hivyo hivyo" daktari Jason alisema.

Yule mtoto alichukuliwa na daktari mmoja wa kike, alimpa malezi ya mama siku hiyo maana mama yake mzazi hakuwa ameamka siku

nzima. Ilikuwa saa mbili asubuhi siku ya Jumatano ndipo Majuma alipozinduka kutoka kwenye usingizi mzito. Alipoamka alianza kuongea mambo ya ajabu na yasiyoeleweka huku akisindikiza na matusi. Madaktari hawakushangaa kwani mara nyingi hii hali hutokea. Hata hivyo lilikuwa jambo la furaha kwa madaktari kwa mgonjwa wao kuamka. Awali ilikuwa ngumu Majuma kufahamu na kuelewa ni wapi yupo lakini alipotulia alipata kufahamu ni wapi alipo ndipo alitamka kwa sauti ya upole,

"Mtoto wangu yuko wapi?" aliuliza

"Mtoto yupo usijali" doctor Jason alijibu huku akionekana hakutaka kuweka wazi kila kitu. Majuma hakuwa mkorofi hivyo aliridhika na jibu japo jibu lenyewe halikujitosheleza. Baada ya muda kidogo aliingia yule daktari ambaye aliondoka na mtoto. Majuma alifurahi kumuona mtoto wake. Machozi ya furaha yalianza kumtoka. Kikawa mfanano na kisa cha riwaya ya chozi la heri ambapo Neema alitokwa na chozi la furaha baada ya kumpanga Mwaliko kama mtoto wake. Alijiinua kutoka pale kitandani kwa lengo la kumchukua mtoto wake ndipo alipohisi maumivu makali tumboni. Alitupa macho lile eneo lenye maumivu, mmmh! Mwili na moyo ulisisimka kwa woga kutokana na alichokiona. Aliona kidonda kikubwa. Hakuwa anajua kama alifanyiwa operesheni.

"Daktari!!!" aliita na hata kabla hajajibiwa alisema

"Niliwaambia jamani mtanitesa mkifanya hivi. Mwenzenu sina wa kunitunza sasa nitaishije na hali hii?" aliongea huku analia na kila alipokitazama kidonda chake kilio kiliongezeka maradufu.

"Mungu wangu, hatakiwi kujikakamua maana hivyo anavyolia nyuzi zitafumuka," daktari Jason aliongea. Majuma aliongeza kilio kila alipotazama kidonda kile na hasa baada ya kuona ile sehemu inavuja damu.

"Hii ni changamoto sasa" yule daktari aliyekuwa ameshika mtoto alizungumza.

"Mama nyamaza basi, nyamaza mnyonyeshe mwanao," Majuma aliambiwa lakini ilikuwa kazi bure kwani maumivu makali yaliyokuwa moyoni mwake ndio yaliyokuwa yanamliza. Aliendelea kulia na kama

ilivyo ada ya matatizo, likitokea hili humkumbusha masaibu yote yaliyomtangulia. Majuma alikosa Raha kabisa.

"Tafadhali mama mnyonyeshe mtoto, si unasikia naye analia." Daktari Jason aliongea baada ya kusikia sauti ya kinyonge kutoka kwa mtoto aliyekuwa akijikakamua kulia. Uchungu wa mwana aujuaye mzazi, hakika sauti ya mtoto ilikuwa chungu na ilijaza maumivu makali moyoni mwa Majuma baada tu ya kuisikia. Hakupenda kuona mwanae kipenzi analia mbele ya masikio yake. Kilio chake kilitoweka ghafla, alikubali kumbeba mtoto na kumnyonyesha. Alimnyonyesha kwa shida kwani kila mara mtoto alikuwa anagusa eneo lile lenye kidonda na kusababisha maumivi makali sana.

"Hebu mshikie mtoto maana tunampa mtihani mkubwa kutokana na kidonda chake." daktari Jason alisema. Daktari wa kike alisogea na kumbeba yule mtoto na kumwelekeza kwenye ziwa la mama yake. Mtoto alinyonya ungedhani aliambiwa hatanyonya tena.

Hili tukio lilizaa furaha kiasi fulani na lilimsahulisha shida mbalimbali za dunia hii, japo mara kadhaa akili yake ilichepuka na kuingiza wazo juu ya hali itakavyokuwa. Ataenda kuishi vipi na hali hii mpya iliyozuka? Atashughulika vipi na changamoto zote zitakazomkabili baada ya kutoka hapo hospitalini? Vipi kuhusu kupata mlo huko nyumbani? Loooh! Hili suala la chakula ndilo lilimmaliza nguvu za uvumilivu. Machozi yalianza tena kumtoka, alimsukuma nesi aliyekuwa amemshika mtoto na kuanza kulia huku akiwa amejishika kichwa. Alikata tamaa ya maisha kabisa.

"Daktari nilikwambia nitateseka endapo mtanifanyia oparesheni. Hivi mnavyoniona ndivyo hivi nilivyo…sina ndugu wala jirani na hata hapo jana isingekuwa vijana wale kunileta sijui ningefanya nini mimi! Ni heri mngeniacha nife kuliko hivi mlivyonifanyia, nimekuwa kama mlemavu. Nitafanyaje kazi ili kupata chakula cha mlo wa siku? Njaa itaniua mwenzenu." Majuma alilalamika sana huku kilio cha kwikwi kikimwandama.

# SURA YA NANE

Hatimaye Majuma na mwanawe waliruhusiwa kurudi nyumbani huku gharama ikifadhiliwa na binadamu mwenye utu ambaye majuma hakumjua kamwe. Gari la Dkt Jason ndilo lililomsaidia kufika nyumbani kwake.

Majuma aliutumia muda mwingi kushuka garini kwani muda huo wote alikuwa akitazama kibanda chake kilichokuwa kimeinama na kuinamiana kama mbavu za mbwa, eti nyumba. Alitazama mlango wake kuukuu uliokuwa umevunjika vunjika kwa vipande visivyohesabika. Kupitia tundu la kibanda hiki, Majuma alihesabu kila kitu kilchokuwa ndani mwa nyumba yake ya kipekee. Macho yake yalimtuma hadi paani na kulitazama lile bati lililokuwa limening'inia likisubiri upepo uje ili lihamie kwingineko. Chozi chungu lenye wingi wa hisia lilimdondoka kifuani na kuteremka polepole mpaka kwa mwanawe. Ni vipi angeishi? Angekula nini? Mwanawe je? Uchungu ulioje!

Siku zote lisilobudi hupasi mitihani ya aina yote bila kushirikisha wahusika na matarajio yao. Majuma hakuwa na nia nyingine isipokuwa kushuka na kuyaishi maisha yamtakayo wala si maisha ayatakayo yeye. Angeyataka maisha, basi hangekuwa amedhalilishwa na kusalitiwa na wanaume pamoja na dunia. Leo hii angelikuwa Daktari au Mwanasheria atetee haki ya wanyonge.

Majuma alitembea kwa uchungu mwingi hadi kwa nyumba yake. Alikilaza kimalaika chake kitandani naye kwa utaratibu akaanza shughuli za kuwasha moto aweke chakula motoni. Aliutwaa ule unga aliounununua kwa gharama ya Dkt Jason kwa maandalizi ya chamcha. Ghafla bin vuu, kitoto chake kilipiga unyende mkali uliomshtua mamaye. Huenda mtoto aliogopa mazingira ya pale yenye mateso mengi. Majuma alikichukua kitoto chake na kukipakaza kifuani pake huku macho yametua kwa sufuria mekoni bila kujiuliza kulikoni kwa mwanawe.

"Jamani mwanangu usilie." Alisema kwa upole kama ilivyo kawaida ya mama zetu wa kiafrika wanapozungumza na wanao huku wakijua kuwa wanao hawawezi kuelewa wala kusikia. Mtoto aliendelea kulia tena kwa nguvu.

"Nakupenda mwanangu, tafadhali usilie. Usilie sana mamangu." Alisema na kumtazama mwanawe aliyekuwa amevamiwa na jeshi la siafu. Moyo ulimkwenda mbio kwa kile alichokiona. Mtoto alikuwa anang'atwa na siafu ambao waliingia pale nyumbani kwa muda ambao Majuma alikuwa hospitalini. Basi kutokana na ulaini wa ngozi ya mtoto basi vidonda vilitokea kiurahisi

"Nng'aaaaaaa! Nng'aaaaaaa!" mtoto alilia sana kwa uchungu mwingi.

"Oooh! Una balaa au mkosi gani Majuma?" alijiuliza mwenyewe huku anafuta machozi. Alifanikiwa kuwatoa siafu waliokuwa wanamng'ata mtoto wake ambaye hakuacha kulia. Kilio cha mtoto kilizaa kilio kwake, kilio kilichozalisha maumivu makali kwenye kidonda kilichokosa nguvu ya kukauka kwani kila dakika kilitoneshwa. Maumivu aliyopata hayakuelezeka kabisa yani alihisi kuchanganyikiwa. Akiwa katika hali hiyo, ghafla alihisia harufu ya kitu kuungua kumbe moto ulikolea sana na kusababisha sufuria kuteketea. Nguvu ya kwenda kuipua aliikosa. Alimlaza mtoto pembeni naye bila kujijua aliangukia kitanda wakati alikuwa mwingi wa njaa na uchovu, maumivu yaliyokuwa kila sehemu yalimwandama Majuma. Kidonda kilivuja damu.

Majuma alikuwa amepitia masaibu mengi kufikia kipindi kile.Ungemuona kwa muda ule ingekuwa rahisi kuchambua maisha yake kutokana na mtazamo wake kwani, Mwili wa Majuma ulikuwa umedhoofika kwa unyonge na machungu ya ulimwengu. Urembo wake wa enzi zile ulikuwa umepotea akawa amerithi mwonekano wa bikizee kutokana na kukonda sana na kubakia fremu. Alirudi na kumtazama mwanawe aliyekuwa amelala. Kadri alivyomtazama ndivyo mawazo chungu nzima yalivyojenga ukaribu na kichwa chake.

"Au nimkimbie? Nikimtelekeza nani atajua? Mmmh!" alisita kidogo kisha aliendelea kuwaza hili na lile lakini yote hayo aliyaona hayana maana kwani si haki ya mtoto kutupwa ama kutelekezwa.

“Sitakutupa wala kukutelekeza mwanangu, kama kufa tufe wote.” alijisemea kwa sauti yake dhoofu ambayo angezungumza mbele ya watu wangehisi anawanong’onezea. Macho yake bado yalikuwa kwa mtoto wake ungedhani kuna kitu kipya alikuwa anakishangaa. Hata hivyo, tumbo lililokuwa linanguruma kwa njaa lilimsukuma mahali lilipo jiko lake. Jiko lililobeba sufuria ambayo hadi sasa ilikuwa nyeusi. Kuni nazo zilikuwa zimeisha zote.

“Aaah!” alitoa sauti yenye uchungu na mafadhaiko ndani yake, fundo kubwa la kilio lilimkaba shingo. Aliwaza na kuwazua namna ya kupata chakula kwa ajili ya siku hiyo. Kwenda kuokota kuni ingewezekana? Alijikuta analia maana kwake kulia kulikuwa suluhu.

"Liwalo na liwe!"Alijiambia Majuma kwa sauti dhaifu. Usiku ulipokaribia, alirudisha vigodoro vyake ndani na kujilaza yeye na mwanae. Alilalia mate siku hiyo. Usiku nao ukawa mrefu sana, aliteseka kwa maumivu, njaa na kuamka mara kadhaa kumnyonyesha mtoto wake. Kwake ulikuwa usiku wa mateso yasiyosahulika. Hatimaye baada ya ngoja ngoja nyingi asubuhi ilifika. Majuma alikuwa anawaza na kujiuliza ni baya lipi jipya litakalomtokea siku hiyo maana kwake kila jambo lilikuwa la machozi na majuto.

Majuma alikumbuka jinsi misukosuko na mikosi ilivyomwandama kwa kufuatana na kufanya kila kukicha kukawa afadhali jana. Aliamka na kupiga miayo iliyoashiria kuwa na njaa, aliposimama ili atembee. Alikuwa mwepesi kama karatasi kutokana na njaa iliyomshika na kumnyonya nguvu zote. Isingekuwa mkono kuwahi kushikilia ukuta, Majuma angeangukia jiwe. Angeanguka, tena angeangukia ule upande wa kidonda.

“Nitakufa aki” alijisemea na kukaa sakafuni bila kujali vumbi na uchafu uliokuwa umeenea na kutapakaa kama pipa la taka, tumbo liliwaka moto. Baada ya kufikiria alipata jawabu la kutambaa na kujikokota mpaka sokoni, si hata ngo'mbe akivunjika mguu hujikokota mpaka zizini? Aliamua kwamba alikuwa nayo nusu shari basi angeenda kwa mwendo wa kujikokota.

Majuma kabla ya kupiga hatua nyingine ya safari ya kuelekea sokoni, macho yake yalimpeleka moja kwa moja mpaka pale mlangoni.

Pale chini palikuwepo na kiroba kimoja chafu kupindukia. Kulingana na fahamu zake, Majuma hakuwa ameweka gunia hili hapa.

"Mtume Mwombezi! Imekuwaje tena!!" aliongea kwa mshtuko na mshangao mkubwa.

"Ni nini hiki?" Majuma alipata nguvu ya kuinuka pale na kusogea hadi mahali husika. Alifanya uchunguzi wa haraka kwa kutumia macho yake kisha alijiuliza

"Nani ameweka hapa na kunani humu?" Kama kuku alianza kuchakura chakura ndani ya kiroba cha kilo ishirini. Aliamua kufungua kiroba kile japo si maadali aliyofunzwa. Alifungua kwa wasiwasi mkubwa sana huku akijiandaa kwa lolote litakalo tokea. Baada ya kufungua kile kiroba, alipata kifurushi kingine ndani.

Alitoa na kugundua kwamba kilikuwa kifurushi kilichobeba mchele na pia kiliwekwa unga kilo tano.

"Mungu Wangu" aliingiwa na furaha kubwa sana baada ya kuona haya yote. Hata hivyo furaha yake kubwa ilikuwa ikighasiwa na wasiwasi uliotokana na swali kwamba, "ni nani ameweka huo mzigo hapo? Je, ni wake?" Hata hivyo haya maswali hayakumfanya asite kufanya alichotakiwa kufanya. Hakuwaza mara mbili, alijikaza kidogo na kuuvuta ndani ule mzigo.

"Mungu najua hujawai mwacha mja wako hasa yule anayekulilia na kukutumaini wewe. Wewe ndiwe unayejua ukweli kuhusu hili, hivyo naomba ukavibariki na kuvitakasa kwa ajili ya matumizi yangu. Mbariki pia mtumishi wako aliyenikumbuka kwa njia hii. Asante sana Mungu" Majuma alitamka akiwa amefunga viganja vya mikono yake.

Alitoka pale akiwa na tumaini jipya huku tabasamu iliyompotea kwa miezi kadhaa ikianza kubisha hodi kwake. Aliusikia ubaridi fulani na upepo mwanana ukipepea moyoni mwake. Siyo moyo bali hata roho na mwili vilionja ladha murwa ya ile theluthi ya furaha iliyoangukia miguuni mwake siku hiyo. Alihisi kushiba. Alimtazama mwanawe kwa furaha na kutamani hata amkumbatie lakini isingewezekana, alibaki kutabasamu tu.

"Mashallah!" Alikenua kinywa chake huku tabasamu ikimtoka kwa furaha asijue lipi la kuongeza.

Mara nyingi shetani hupenda kuona furaha ikitoweka kwa wote wenye kumtegemea Mungu, ndio maana alimua kumpa Majuma umbea fulani.

"Unachekelea haya? Wewe ni mpuuzi sana. Unaanzaje kufurahia kitu ambacho hujui kimetoka wapi na kwa nani? Hujui wala hufahamu huyu nani ameweka nini kwa hiyo nini. Itakuwaje kama amekuwekea sumu?" nafsi ya Majuma ilishtuka sana lakini hakutaka kushindwa na jaribu hilo, kwani Imani yake ilikuwa kubwa na ndio maana aliomba Mungu avitakase vile vitu. Shetani kutokana na hali kuwa hapendi kushindwa, alikuja na mbinu nyingine.

"Si una chakula, haya pika basi nikuone" Majuma alikumbuka kwamba hakuwa na kuni. Na suala la kuni hapo awali ndilo ambalo lilimtoa pale kwake kwa lengo la kwenda kununua chakula kwani kama ni unga alikuwa nao japo kidogo ila angepikaje? Kwa hili suala la kuni shetani alimdhihaki Majuma.

"Yule aliyenianzishia safari hawezi niacha njiani." alijisemea na kusimama kwa nguvu maana alijiona imara zaidi. Ule udhaifu ulipungua kwa kiasi. Majuma alimgeukia mwanae na kumbusu kisha alianza kuzungumza.

"Nina nguvu mwanangu. Acha nitoke nikaokote kuni nipike nile ili nawe upate chakula chako mama." Alisema hayo na kutoka akiwa na panga lake ambalo halikuwa jipya kwani lilikuwa limechakaa lisilo la makali. Alifunga mlango wake na kutembea haraka kuelekea kwenye pori fulani ambalo halikuwa mbali sana na pale nyumbani. Alifika kule na kuanza kukata vikuni vidogo vidogo. Majuma alikuwa makini asije athiri upya like jeraha. Ama kweli moyo hautulizwi kwa shibe ya faraja na ukitulia basi hutulia kwa muda mfupi sana kisha hali itarudi pale pale.

Majuma alitembea haraka baada ya kusikia kwi kwi kwi za mwanawe, alitupa zile kuni karibu na ua ili akakitazame kitoto chake. Kwa mara nyingine hakuamini macho yake. Ilkuwa ngumu sana kuamini macho juu ya kile kilichokuwa mbele yake.

"Asante sana Mungu wangu, umenikumbuka tena" alijikuta akizungumza maneno hayo kwa furaha isiyo kifani. Alishuka hadi chini na kupiga magoti akiendelea kutoa shukrani zake nyingi kwa Mungu.

Baada ya hapo aliusogelea ule mtungi wa gesi wa kampuni ya

MPISHI uliokuwa karibu na mlango wake, sehemu Ile Ile alipokutana na kiroba kile. Pembeni ya mtungi huu kulikuwa na kibuyu cha lita tano cha mafuta ya kupikia bila kuacha kale kiroba kalichokuwa na nyanya pamoja na samaki. Alijikaza kuvibeba vitu vile na kuviingiza ndani kisha haraka haraka aliweka maandalizi sawa na kuanza kupika. Baada ya chakula aliamua kumnyonyesha kabisa mtoto wake na kumlaza kitandani. Furaha na raha viliutawala moyo wa Majuma, huzuni ingetoka wapi? Mawazo ya nini tena? Kwa nini asifurahi? Kwa nini awaze? Labda cha kuwaza tu ni namna ya kupata maji maana yalikuwa umbali wa kiasi fulani kutoka pale anapokaa. Kingine ni juu ya huyu mtu aliyeamua kujitoa kumpa msaada wa vitu vyote hivi. Ni nani?

Usiku ulichukua zamu Majuma akiwa mwenye faraja moyo mwake. Alimwamsha mtoto wake aliyekuwa mtulivu saa zote zile. Alimwamsha na kumnyonyesha kidogo kisha alimkumbuka Mungu. Majuma aliomba kwa sauti ya chini.

"Baba nakushukuru kwa ulinzi wako ambao haujanipungukia na hautanipungukia hata sekunde. Nashukuru kwa tumaini jipya ulilozalisha ndani ya maisha yangu maana nilikata tamaa, nilivunjika moyo kiasi cha kutamani kutoweka hapa duniani, naomba unisamehe kwa hilo. Ulisikia kilio changu na hakika hukuniacha. Nakuomba ewe Jalali mwema uwe nami usiku huu na siku zote za maisha yangu kwa ajili ya sifa na utukufu wa jina lako. Amiiin" alimaliza na kujilaza pembeni ya mtoto wake. Katika maombi yake ya kila siku hakuacha kabisa kutaja neno "shukurani" kwa maana neno hili lilikuwa na uzito wa pekee kwa kila maombi yake kwa Mungu. Siku zote bila kujali unapitia jambo gani, yaani liwe baya au zuri, mshukuru Mungu. Hata vitabu vitakatifu vinasema " shukuruni Mungu kwa kila jambo"

Siku zilisonga akiwa na ahueni licha ya kukosa mtu wa kusaidiana naye. Kilichomchanganya Majuma kila siku ni yule mtu. Kwanza ni nani huyu mtu? Anatoka wapi na amlijuaje kama Majuma alihitaji msaada hasa wa vitu kama vile alivyovileta? Ni nani? Majuma hakumjua japo baada ya kuruhusu akili yake kufanya utafiti kidogo, alimhisi mtu fulani.

"Siwezi kaa bila kwenda kumshukuru" alisema asubuhi ya siku moja baada ya kujiandaa.

"Kule ni mbali sana, niende na mtoto au nimuache tu hapa nyumbani?" alijiuliza akiwa amesimama ungedhani alihojiwa na mtu. Aliwaza umbali uliopo kutoka pale hadi anapotaka kwenda na hali aliyokuwa nayo. Lakini angemuachaje mwanawe pekee yake? Aliamua kumwandaa mtoto wake na kumbeba kisha safari ilianza. Alitembea taratibu, mtoto wake akiwa mgongoni. Baada ya saa moja alifika mahali pale na kupumzika kidogo kwani alichoka si haba. Dakika nazo kama kawaida ya kukosa subira zilizidi kusonga mbele ndipo alipoamua kuinuka na kuingia ndani. Ilikuwa ni jambo la heri sana hapakuwa na foleni hivyo aliingia moja kwa moja.

"Oooh karibu sana mama"

"Asante sana" baada ya salamu mazungumzo yalianza.

"Ni muda mrefu hatujaonana, ila natumaini mambo yanaenda vizuri eh" alisema Dkt Jason.

"Yanaenda vizuri, hata hivyo bila wewe hakika sijui ningeishije" Majuma alizungumza kwa hisia kali.

"Oooh! Ondoa shaka mama, wala usijali kabisa"

"Hata sijui nikushukuru vipi. Maana msaada wako ni mkubwa kuliko hata shukurani zangu ninazotoa. Nashukuru sana kwa chakula, jiko la gesi na vingine vyote ulivyonipa" Majuma alisema na kutaka kupiga magoti. Kwa namna fulani doctor alishtuka kutokana na maneno yale.

"Hapo umeniacha sasa. Msaada wa jiko la gesi na chakula?" doctor Jason aliuliza kwa mshangao. Majuma alimuelezea daktari jinsi ilivyo hata hivyo alishangaa kuona namna daktari alivyokuwa anashangaa kusikia hayo. Hakuwa yeye aliyempa msaada.

"Kwani ni nani anayenisaidia?" alijiuliza.

Mida ya saa sita mchana alikuwa njiani kurudi nyumbani, kichwani akijiuliza maswali mengi juu ya mtu huyu asiyemjua. Hakupata kujua kabisa maana amdhaniaye ndiye kumbe siye. Alitembea taratibu sana kwani alichoka nayo njaa ikaanza kujitokeza. Majira ya saa nane mchana ndipo alifika nyumbani kwake.

"Mama yanguu!" Alisema kwa mshtuko mkubwa na kuibebesha mikono kichwani. Nguvu zilimuisha kabisa na kukaa chini, machozi nayo

yaliaanza kutiririka shavuni pake.
“Na vipi kama ningemuacha mtoto hapa?” alijiuliza na kuanza kulia kwa uchungu mkali. Alitamani kujiburuza chini na kugalagala ili kupunguza uchungu mkali ulioganda kwenye ukuta wa moyo wake. Mtoto wake aliyekuwa amembeba mgongoni alikuwa kizuizi katika utekelezaji wa alichokitamani. Alibaki tu ameshikilia kichwa huku akijikaza kulia kwa sauti lakini wapi! Sauti haikutoka sana kwani kila alipotaka kufanya hivyo tumbo lilipata maumivu kama linalochanika.

“Aaah! Jamani mimi nitaenda wapi sasa? Mbona nilionjeshwa tabasamu?” aliongea huku anafuta machozi. Kilio chake kilizaa kelele, kelele zikamwamsha mtoto mgongoni. Sasa vilio viliongezeka maradufu. Mtoto naye alifungua zamu ya kumsaidia mamaye kulia. Alikuwa analia kwa uchungu wa kile alichokiona kwa macho yake. Kilio cha mtoto kilimuongezea nguvu ya kulia zaidi. Akiwa pale pale chini ghafla alishuhudia kwa macho yake mzee mmoja aliyekuwa ameshika panga mkononi mwake akitokea upande wa kushoto.

“Na wewe ni nani? Na unafanya nini hapa?” mzee Boronga alifoka na kuonekana mwenye hasira nyingi. Majuma alikosa cha kujibu, kiliokilipoteaghafla.
“Yani binadamu sijui mna roho gani. Hata hamkumbuki fadhila licha ya mema mnayofanyiwa? Hamkumbuki makubaliano? Wapumbavu kabisa!” mzee Boronga alifoka akiwa ameachana na swali alilomuuliza Majuma, sasa alikuwa anapiga hatua hadi mahali palipokuwa na vichaka na kuanza kufyeka.Majuma hakuelewa mzee alikuwa na maana gani kusema hivyo na kwanza kabisa huyu mzee alikuwa ni nani? Hili lilizidi kumchanganya Majuma.

“Kwa hivyo huyu mzee ndiye aliyenifanyia hivi?” chozi la uchungu lilimtoka Majuma. Mzee Boronga aliendelea kulalamika.
“Binadamu hawajali chochote hasa hawa vijana wa siku hizi, si waaminifu kabisa. Yani tunapanga vizuri kwamba hakuna tatizo aje akae hapa ila awe ananipa hata sukari au chumvi lakini wapi! Hakuna chochote hata salamu ya Mungu haleti. Kwa nini nisibomoe hiki kibanda ili nilime! Kwanza amenichelewesha sana kilimo." Mzee Boronga alilalamika sana, tena kwa hasira.

Lo! Kumbe bwana Joshua alimtafuta mzee Boronga ili kuomba huruma zake. Ilikuwa baada ya kukosa mahali pa kujisitiri kile kipindi alipofukuzwa mjini Nakuru. Ilikuwa ngumu kukubalika maana mzee alikuwa na mpango wake wa kubomoa ile nyumba ambayo ni kama kibanda kwa lengo la kufanya kilimo, lakini baada ya makubaliano kwamba atakuwa anampa chakula pamoja na pesa za mahitaji madogo madogo mzee Boronga alikubali.

Siku na miezi ya awali bwana Joshua alikuwa anafanya kama walivyokubaliana kwa kumpa mzee chakula na pesa ya matumizi mengine lakini ilifika miezi kadhaa mambo yalianza kubadilika. Makubaliano yote yalianza kuvunjwa, si unga wala chumvi iliyokuwa inapelekwa kwa mzee Boronga. Mzee alishtuka ndipo alipoamua kumfuata bwana Joshua lakini kila alivyomfuata, alikimbia. Jitihada za mzee kumpata Joshua ziligonga mwamba. Kukurukakara za mzee Boronga zilichangia kwa kiasi kikubwa sana kumfanya Joshua akimbie mahali pale kando na jukumu lililoongezeka kwake, jukumu la familia. Kumkosa kabisa ndiko kuliinua hasira za mzee ndipo aliamua kufunga safari hadi mahali pale na kubomoa nyumba ile bila kujali wala kujiuliza chochote. Nyumba ilibomolewa kwa hasira, hata vitu vilivyokuwa ndani viliharibika kwa usongo hasa. Vipi kama Majuma angemuacha mtoto kwa nyumba?

Majuma aliketi pale huku mkonowe ukiwa umeshika tama asijue kipi cha kufanya. Alimtazama mwanawe kwa huruma kisha akawaza na kuwazua angekuwa mgeni wa nani yeye. Mawazo yake yalimsafirisha moja kwa moja mpaka mwanzo wa mikosi yake alipokuwa shuleni Nakuru. Mtiririko wa matukio ulibadilishana zamu ya mawazo kutoka hili mpake lile. Yote hayo yalimfanya ahisi kauli ya mamaye kumuita Mwanaharamu aliyelaaniwa iwe ya kweli. " Je, damu ni nzito kuliko maji kweli? Ikiwa jibu ni naam basi ni akina nani hao ambao walipima mizani na kupata kwamba ni nzito. Tena vipimo hivi vya kupima mizani ilipimwa lini maana mambo mengi yamebadilika."

# SURA YA TISA

"Nakushukuru ewe Jalali mwenye nyingi rehema na huruma. Asante kunijali na kunipa tumaini hasa nyakati mwanga wangu umezima, asante kuniwashia taa yako kwenye vitabu vitakatifu kuwa hutoniacha kwa shida na raha. Nipe nguvu ya leo na kesho niweze kukabiliana na milima maishani mwangu. Zaidi ya yote nitie nguvu nimalize mwendo salama. Eeeh Mungu mwema nakuomba!"

Majuma alianza kupiga hatua huku akili yake akiwa ameielekeza kwa mzazi wake, hata hivyo moyoni alihisi uoga fulani kwani hakujua ikiwa angepokelewa au angefurushwa kama punda. Alikuwa anaenda nyumbani kwa mama yake, mama yake yule yule aliyewahi kumfukuza na kumuita ibilisi, shetani. Si kwamba hakuwa anakumbuka yote hayo.

Safari ya Murumba hadi nyumbani kwao Munduma haikuwa umbali mkubwa sana, ni takribani saa moja kutembea na kufika lakini kwa hali yake yeye na mtoto mgongoni na namna alivyokuwa akihisi njaa, basi alipaona parefu sana. Hata hivyo alitamani kufika nyumbani kwa mama yake. Alijikaza kama mwanamke na mamaye mtu. Safari yake ndogo haikuwa mwisho wa mawazo na maswali mengi yaliyokuwa yanakizunguka kichwa chake kumuwanga vibaya. Mengi yalikuwa juu ya yote yaliyomkuta, nini chanzo chake? Yataisha lini? Maswali yalizaa maswali. Je, atapokelewa nyumbani au itakuwa kama ilivyokuwa siku nyingine ya nyuma alipotimuliwa kama mbwa mwizi?

Kwa kiasi fulani moyo ulisita, hofu iliingia ndani yake na kumkumbusha kwamba nguvu ya kustahimili aibu ya kufukuzwa tena haipo. Atafanyaje sasa? Aliendelea kuchapa mguu japo kwa wasiwasi. Alipiga hatua fupi fupi zenye udhaifu mwingi na mara kadhaa alikuwa

anakaa chini kupumzika. Mtoto alilia kuonyesha kwamba njaa inasumbua tumbo lake.

"Mwanangu nionee huruma mamako sijala" alisema na kumsogeza ubavuni kisha alitoa ziwa lake na kumpa anyonye. Hakukuwa na chochote. Mtoto alivuta maziwa, mama naye alikamua lakini juhudi zao hazikufua dafu. Hakukuwa na njia nyingine zaidi ya kumrudisha mgongoni na kuendelea na safari ambayo hadi sasa ni dakika 30 zimetumika lakini hata robo ya safari hawajafikia.

"Hakika si bure, ni lazima mkono wa mtu upo kwenye maisha yangu" alijiwazia.

"Nilikuwa msichana mrembo, wazazi walinipenda na kuniamini, juhudi zangu zilikuwa kubwa shuleni hata kanisani lakini ghafla tu leo hii niko hapa nahangaika pekee yangu. Si bure" Imani ya Majuma ilijaribu kuegemea upande mwingine, upande wa ushirikina na kuwaza labda kuna mtu alikuwa amemfanyia mazingara na kunyakua nyota yake. Ni nani sasa? Je, ni Fitina aliyekuwa anaishi naye huko Nakuru?

"Kama kuteseka nimeteseka vya kutosha. Na nikifukuzwa tena huku ninakoenda, basi safari yangu itakuwa kwa mganga." Mawazo ya Majuma yalibadilika ghafla. Ama ndio usemi kuwa mtegea cha nduguye hufa masikini?

Mida ya saa kumi na mbili jioni alifika kijijini Munduma akiwa hoi bin taabani. Mahali alipokuwa amefika hapakuwa mbali sana na pale nyumbani kwa mama yake kwani palikuwa panaonekana licha ya mahindi shambani yaliyokuwa yanazuia pasionekane. Mazingira hapo kijijini yalibadilika kwa kiasi kikubwa kwani kipindi alitoka kuna vitu havikuwepo na hata mashamba mengine yalikuwa hayajalimwa, yalienea nyasi tu. Majuma alikaa chini na kumsogeza mtoto ubavuni mwake kwa mara nyingine. Alimuweka sawa na kujaribu kumnyonyesha lakini kama ilivyokuwa hapo awali ndivyo ilivyokuwa sasa. Maziwa hayakutoka. Mtoto alilia kwa uchungu.

"Lu Lu Lu Nyamaza, nyamaza mtoto mzuri," alianza kumbembeleza kwa nyimbo lakini mtoto hakunyamaza kwa sababu kilichokuwa kinamliza kulihitaji tu chakula. Alikuwa na njaa, njaa ya chakula. Kilio cha mtoto kilizidi hivyo kilimsukuma Majuma kuchukua

hatua, hatua ya kuondoka pale lakini woga na hofu viliweka uzio mkubwa mbele yake. Atapita wapi?

"Au niende kwa Rehema?" alijiuliza lakini kabla hajajijibu kwa maamuzi, akili yake ilimkumbusha kwamba kuna siku waligombana na kutupiana maneno na Rehema, sasa ataenda kuongea nini huko?

"Aaaah!" Majuma alichukia. Kitu kigumu mfano wa tonge kilimkaba koo. Bado alikuwa chini akitafakari hili na lile bila kupata jibu sahihi japo orodha ya majibu yote ilikuwepo mbele yake. Baada ya kukaa chini na kutafakari, alisimama na kujipa moyo wa ujasiri.

"Liwalo na liwe!" aliyasema hayo akiwa ameshafikia uamuzi wa kwenda nyumbani kwa mama yake mzazi. Alimuweka mgongoni mtoto wake ambaye bado alikuwa analia. Alishusha pumzi ndefu na kuanza kutembea taratibu kuelekea pale nyumbani.

"Atakaponiona atafanya nini? Atasema nini?" aliwaza. Alitembea hatua kama 30 hivi, alikuwa amefika pale nyumbani. Alikuwa mbele ya mlango anasita kugonga. Baada ya kutumia dakika moja ya kujishauri, mwisho aliamua kuugonga ule mlango ambao haukufungwa ila uliegeshwa tu.

"Hodi hapa!"

"Hodi....hodi...hodi" alitoa sauti ndogo baada ya kuusulubu mlango kwa mikong'oto miwili japo laini na ya hofu. Hakukuwa na mwitikio wowote hivyo alitamani kufungua aangalie ndani ila angewezaje kufanya hivyo. Yaani ni nyumbani kwao lakini kwake ni kama kituo cha polisi. Majuma alikuwa mgeni nyumbani kwa mama yake mzazi. Aligonga tena lakini hakukuwa na tofauti na awali.

Aligeuka na kutazama kushoto kisha kulia, upande alikotokea. Uso kwa uso na mamaye aliyekuwa amebeba mzigo wa kuni kichwani. Kilichoukamata moyo wa Majuma hakikutambulika moja kwa moja hadi sasa. Je, hofu, woga, kitete vikichanganyika pamoja na ujasiri wa uongo ni nini huzaliwa? Najua hata wewe hujui. Majuma alitamani kukimbia lakini njaa iliyomshika iliifunga miguu yake kwa kifungo cha ulegevu. Alisimama tu akiwa hajui cha kufanya, alibaki tu kutoa macho na kumtazama mama yake ambaye alikuwa anapiga hatua za taratibu huku akionyesha kupigwa na butwaa. Hatua kama nne kabla ya kumfikia Majuma, mama huyu alitupa kuni alizobeba na kukimbia hadi

aliposimama Majuma.

“Majuma! Wewe ni Majuma?” aliita na kumkumbatia kwa nguvu mwanae.

“Majuma mwanangu ulikuwa unaishi wapi? Naona Mungu amenitendea muujiza mkubwa. Mungu ameamua kusikia maombi yangu. Ameamua kunifuta machozi” Bi Saradibo alisema na kumbusu mwanaye. Haya yote yalimuacha Majuma mdomo wazi. Leo hii kurudi kwake kumekuwa muujiza kwa mama yake aliyekuwa hataki kumuona?

“Siku zote nimekosa raha, nimeishi na upweke maana baba yako hayupo nawe pia haukuwepo. Nilijuta kukupoteza mwanangu. Hakika sikukupoteza wewe tu, nilipoteza amani, furaha na raha yangu, nilijuta kukukana na kukutimua mwanangu, nimeishi kujihukumu kuikana damu yangu tena kipenzi mwanangu aliyekuwa mboni ya furaha kwa familia yangu. Nimejihukumu kukusaliti mamaa, niitazame nilivyo konda kama sindano, hivi sasa kukuona kwangu kumenitia furaha na amani. "Alisema mama Majuma aliyezungumza huku akilia. Ni kweli alikonda sana. Majuma muda wote ule alikuwa amekmia na kuruhusu mtiririko wa machozi kushika usukani. Hakuweza kusema chochote kwani alipotaka kufanya hivyo kilio cha kwikwi kilimzuia. Alilia kwa kumbukumbu za machungu yote yaliyomkuta pamoja na kumuona mama yake jinsi alivyokonda. Wote walikuwa wanalia.

“Ma-ma, us-ili-e” Majuma alisema akijaribu kumtuliza mama yake wakati yeye mwenyewe machozi yalimtoka mithili ya maji bombani. Simanzi na furaha vikatawala mahali hapa hadi wakati ambao mama yake alipoamua kujinasua na kumvuta mwanae ndani ya nyumba.

Aliwasha moto haraka na kuupasha wali aliopika asubuhi. Baada ya dakika kadhaa alimwandalia Majuma kile chakula kisha alianza kupika kingine akiamini kwamba Majuma alihitaji chakula kwa wingi. Mapenzi ya mama.

Ilikuwa mida ya saa moja usiku, walikuwa wamekaa ndani huku Bi Saradibo amempakata mjukuu wake. Walikuwa wanaongea mambo kadha wa kadha hadi walipoanza kuongelelea haya yaliyowazunguka kwa miezi mingi iliyopita.

“Majuma mwanangu, naomba unambie ni yapi ambayo siyafahamu kukuhusu wewe,” mama Majuma alisema huku akimbembeleza mjukuu wake aliyekuwa anarusha rusha vimikono.

“Ni mengi sana mamangu” Majuma alianza. “hapa unaponiona mama, niko na jeraha la oparesheni ya kumpata huyu mtoto.” aliongea kwa hisia kali za huzuni. Mama yake alishtuka sana.

“Kumbe ndio maana umekonda sana mtoto wangu. Ulikuwa unakula nini sasa? Ulikuwa unaishije na hiyo hali peke yako? “ yalikuwa maswali mfululizo kutoka kwa Bi Saradibo.

“Mungu ndiye anayejua mama. Kwa kweli ni mengi hadi nashindwa ni lipi nianze nalo na lipi nimalize nalo” Majuma alisema na kutulia kidogo kisha aliendelea.

“Nitakusimulia kisa kizima toka mwanzo hadi mwisho ili uelewe vizuri na ujue chanzo cha yote haya.” Majuma alisema japo kuwa alikuwa anasita kueleza ukweli kuhusu yote aliyofanyiwa na Fitina.

Bi Saradibo hakuamini kile alichokisia, aligonga maskio na kufumbata macho yake mara kadhaa akifikiri kuwa aliyoyasikia ilikuwa ndoto mbaya.

“Yote hayo yalikukuta wewe?” mama mtu aliuliza akiwa haamini aliyoyasikia.

“Ndio mama"

“Nisamehe sana mwanangu. Naomba unisamehe kwa sababu mimi ndio chanzo cha mateso yako. Najua nisingekufukuza basi hayo yote yasingetokea”

“Usijali mama, najua hayo yote yamepita” Majuma alimjibu mamake kwa kumuondolea shaka.

“Ni kweli yamepita lakini yameacha jeraha kubwa moyoni mwangu. Najuta kwa yote niliyokufanyia mamayo mzazi” Bi Saradibo alilia sana, mtoto nae alianza kulia.

“Mnyonyeshe mtoto” Bi Saradibo alisema akiwa amempeleka mtoto kwa Majuma. Ulifuata ukimya wa dakika kadhaa kisha Majuma aliuvunja ukimya ule.

“Kwa hivyo ndivyo hali halisi mama, cha muhimu tuko pamoja tena”

“Pole sana kipenzi changu cha pekee. Katika hili sina mtu wa kumlaumu. Simlaumu Fitina wala Rehema au mume wake aliyekufukuza, lawama zote nastahili kubeba. Naomba msamaha kwako na kwa Mungu wangu kwa jambo ambalo nililifanya. Hakika ule haukuwa ubinadamu, hasira zilizaa roho ya unyama ndani yangu kisha nikasahau kuwa hasira hasara. Nisamehe ili Mungu pia anisamehe” Alisema Bi Saradibo huku amepiga magoti. Majuma alihisi vibaya sana kuona mama yake amepiga magoti huku analia.

“Mama inuka kwanza. Usifanye hivyo, mimi nilikusamehe kitambo ndio maana nikaamua kurudi nyumbani.” Majuma alisema na kujaribu kumuinua mama yake.

“Naumia moyo kila ninapokumbuka haya yote. Nina hakika Na nimeamini sasa kuwa ulitakiwa kufa kabisa. Ikiwa ningekupoteza sijui ningeishije mimi. Majuma mwanangu ulitakiwa na ilikuwa imepangwa ufe.” Majuma alishtuka sana kusikia kuwa alitakiwa kufa. Ilibaki kidogo tu ambwage mtoto chini kwa mshtuko.

“Mama mbona sikuelewi. Ningekufa kwa sababu gani? Nini kingeniua?” Majuma aliuliza huku anamtikisatikisa mtoto kwa namna ya kumbembeleza maana ule mshtuko wakati alitaka kuanguka pamoja na kelele za vilio zilifukuza usingizi wake.

“Majuma kipenzi, sijui hata nikwambie nini. Namshkuru sana Mungu maana licha ya makosa yangu, hakuacha kunisikiliza maombi yangu ya kila siku kwamba akulinde na ikiwezekana akurudishe nyumbani.” Alisema na kufuta machozi yaliyokuwa yamesambaa sehemu kubwa ya mashavu yake. Hata kabla hajatulia alikutana na maswali mengi kutoka kwa Majuma.

“Mama, kwa nini nilitakiwa kufa? Na ni nani angeniua?” Majuma aliuliza maswali hayo mfululizo lakini hakuna hata moja lililopata majibu yake.

“Kichwa kinaniuma alafu muda pia umeenda sana, hivyo naomba tulale. Tutaongea kesho inshallah!” Bi Saradibo qalisema na kusimama.

Majuma alinyanyuka na kusindikizwa hadi chumbani. Chumba chake kile kile cha siku zote ndicho alichoingia. Japo ni kile kile lakini kilikuwa na utofauti mkubwa kwani blanketi na godoro vyote vilikuwa vipya. Na vyote hivi viliwekwa na mama yake kama maandalizi kwamba siku moja mtoto wake angerudi nyumbani. Majuma alipanda kitandani na mtoto wake kisha taratibu alifunikwa blanketi na Bi Saradibo. Baada ya kufanya hivyo, alisongea taratibu na kumbusu Majuma usoni kisha kwa mjukuu wake. Aliwaaga na kwenda kulala.

Kwa mara ya kwanza Majuma aliona raha iliyokuwa imepotea, akaitafuta kwa tochi na taa akaikosa, raha ya kuwa na mzazi. Raha yenye kuzaliwa kutoka kwenye shina la upendo wa dhati kutoka kwa mama. Hakika raha hii ilikuwa mfano wa kitambaa laini cha sufi kilichokuwa kinapita kusafisha ngozi. Mwili ulisisimka! Usingizi ulikuwa mnono kwenye godoro jipya. Mwili uliona utofauti wa pekee kwani ulishazoea yale maumivu ya kujipinda kwenye vipande vipande vya nguo za vigodoro vilivyowekwa pamoja kufanya godoro la kulalia. Usiku ulikuwa murua!

Ilikuwa asubuhi ya siku nyingine, saa mbili asubuhi. Bado Majuma alikuwa katikati ya usingizi mzito uliokuwa unamfanya aelee huku na huku, huku akiota ndoto saafi akiwa kwenye bustani ya kuvutia mithili ya bustani ya Eden.

“Mwacheni apumzike” Bi Saradibo alijisemea. Ungekuwepo ungedhani kuna mtu kando yake anaongea naye kumbe alikuwa pekee yake wakati anabandika sufuria ya maji jikoni. Maji kwa ajili ya mwanae Majuma kwenda kuoga. Alipomaliza aliyafunika vizuri kwenye ndoo na kuchemsha chai ndipo saa mbili na nusu hivi alienda kumwamsha Majuma. Ungedhani ni mtu na boss wake. Baadaye walikaa pale nje wakiota jua japo lilikuwa na mionzi hafifu. Soga mbalimbali ziliendelea kurindima katikati yao na kufanya mazungumzo yao yanoge. Katika pandashuka za mazungumzo yao, hatimaye Majuma alikumbuka jambo. “Nilitakiwa kufa, kivipi?” alijiuliza mawazoni mwake. Haikuwa kazi nyepesi kupata jibu la hili swali. Suluhisho ni kuuliza na si kujiuliza.

“Mama!”

“Ndio mamangu, toa usemi” mama Majuma aliitikia huku akitoa tabasamu akidhani ni mwendelezo wa soga zao zenye kufurahisha. Majuma alisita kidogo lakini akajikaza tu kuuliza.

“Jana usiku ulizungumza jambo lililoniacha njia panda. Nilitakiwa kufa, kivipi yani?”

“Oooh! Karibu nisahau, naomba ujiweke sawa kesho twende kanisani. Nguo si..” mama Majuma alitaka kuuliza swali lakini aliishia njiani. Aliinuka na kuingia ndani haraka. Huko alifanya upekuzi akitafuta alichokuwa anakifahamu mwenyewe. Huku nje Majuma alikuwa anawaza.

“Kwa nini mama anakwepa kuniambia ukweli wa hili jambo?” aliwaza na muda mfupi baadae sauti ilisikika kutoka ndani.

“Majuma! Njoo..."

Majuma aliingia na kuonyeshwa nguo zake za zamani, mmmh! Nyingi zilikuwa ndogo kwake.

“Mmmh! Ushakuwa mama siku hizi. Nitakupa zangu uvae.” Alisema na kuingia chumbani kwake. Alipekua sana na kutoka na nguo zake nyingi ambazo alimpa Majuma.

"Kesho twende kanisani sasa” Bi Saradibo alisema huku ankitabasamu.

“Sawa, lakini mama natamani nikalione kaburi la baba”

“Usijali, tutaenda kuliona ila cha muhimu twende kanisani kwanza kesho.”

“Sawa mama! Nimekuelewa lakini mbona hutaki kunijibu swali langu mama, kwa nini?” Majuma alilalamika.

“Usiwe na pupa mwanangu. Nahofia kuongeza au kupunguza chumvi maana mimi sio mpishi, mpishi yupo hivyo kesho utayafahamu.”

Kesho yake ilikuwa jumapili, safari ya kwenda kanisani ilianza. Baada ya dakika 30 walifika kanisani. Ibada ilikuwa inaendeshwa na mchungaji Miamba, iliendelea kwa mahubiri yenye nguvu.

“Nakusisitiza leo omba toba. Omba sana toba kwa ajili ya mababu zako, omba sana toba kwa ajili ya bibi zako. Omba toba kwa ajili ya vizazi

vyote vilivyopita." Mchungaji Miamba aliyasema hayo akiwaacha waumini wake wakipiga makofi mengi. Baada ya kujipanguza jasho na kuendelea.

"Kwa nini nasema hivyo? Nina sababu ya kusema hivyo. Narudia tena nina sababu ya kusema hivyo. Leo hii kuna watu wengi wanabebeshwa mzigo usiokuwa wao. Watu wengi wanateseka kwa sababu ya maagano mabaya iliyowekwa na mababu na mabibi enzi hizo. Naomba nikufahamishe kwamba, agano lisipovunjwa hudumu na huishi vizazi hadi vizazi, uzao hadi uzao. Ni muhimu kuvunja maagano yote. Kuvunja ni hatua ya pili, hatua ya kwanza ni ipi?"

"Kuomba tobaaaaaa" kanisa lilijibu kwa sauti. Sauti za vinanda zilitamalaki kanisa nzima. Mchungaji alitulia kidogo kisha akaendelea.

"Roho wa Bwana anasema, kuna msichana mmoja yupo hapa anasumbuliwa na maagano ya kichawi yaliyofanywa na babu zake enzi hizo. Katika familia yao hakutakiwa kusoma wala kufanikiwa hata mtu mmoja. Na akitokea mtu wa kutaka kufanikiwa au kusoma na kufika mbali, basi mikosi humzukia ghafla na chaguo la mwisho la mtu huyu ni kifo kwa sababu anaenda kinyume na maagano" mchungaju Miamba alisema na kuendelea.

"Sasa nasema leo ni mwisho wa mateso yake katika Jina kuu la Yesu aliye hai. Amelia sana ila sasa ndio mwisho" aliposema hivyo ghafla kilisikika kilio cha mtu mwenye kuripuka mapepo. Kilisikika kutoka nyuma ya kanisa.

"Mleteni mbele huyo mama" mchungaji alisema. Yule dada alibebwa msobe msobe hadi mbele. Vijana ambao ni watumishi wa kanisa hilo walisaidiana kumbeba Majuma na kumfikisha mbele kwa mchungaji."Mwekeni hapo hapo" mchungaji alisema kisha aliwageukia waumini.

"Huyu ndiye msichana ambaye anateseka kwa sababu ya maagano ambayo yeye hakuingia na wala hajui kama kulikuwa na maagano hayo. Maagano huishi, omba toba" alisema hayo nakupiga hatua kuelekea kwa Majuma. Mchungaji alikunja magoti yake nakuchuchumaa kisha alianza kumtazama Majuma mfano wa mtu mpelelezi au mchunguzi wa kitu fulani. Alimtazama sana hadi chozi la uchungu lilimtoka machoni pake.

"Ee Mungu wangu! Hili chozi halitafutika kamwe endapo hautamponya mja wako. Wewe ni Mungu mwenye nguvu ipitayo nguvu zote za dunia na ulimwengu. Bwana nakuomba mponye binti huyu, vunja maagano na minyororo yote iliyomfunga" alisema hayo baada ya kupiga magoti.

Baada ya hapo alimgusa na kusimama, kitendo cha kumgusa kilimfanya Majuma aanze kulia na kutoa sauti za ajabu ikiwemo sauti nzito ya mtu ikilalami.

Pepo: Usinitoe, hii ndio nyumba yangu. Hata hivyo sijakamilisha kazi yangu.

Mchungaji: We ni nani?

Pepo :Naitwa shabiusi, nimetokea mjini Belzabuti.

Mchungaji: Kazi gani ambayo hujamaliza?

Pepo: Kumuua huyu binti na kuinywa damu yake.

Mchungaji: Kwa nini mnataka kumuua?

Pepo: Ameenda kinyume na mkataba wetu, sisi ni walinzi wa mkataba.

Mchungaji: Oooooh sasa sikiliza nikwambie, kwa sasa hamna nafasi tena.

Pepo: (kwa hasira) Siondoki, mpaka ninywe damu yake.

MMchungaji: Sasa nikama hunijui mimi pastor Miamba...

Mchungaji Miamba alisema hivyo na kuanza kukemea. Baada ya dakika chache Majuma alitulia na kusimama. Alikuwa vizuri na wala hakuwa anapiga kelele, kitu cha pekee ni kwamba bado akili zake hazikuwa zimemkaa sawasawa, alikuwa anashangaa.

"Wala msihofu, huyu amepona kabisa. Msongezeni akae hapo mbele" mchungaji alisema kisha alitoa sauti kubwa.

"Siachi na sitowacha kuwasisitiza kuomba toba. Wengi wenu hapa mnateseka kwa mambo kama haya. Mnateseka kwa umaskini, magonjwa yasiyoisha pamoja na mikosi kwa sababu ya maagano. Mwambie jirani yako simama tuombe toba."

******

“Mama kwa kweli najihisi tofauti sana tangu nilipoombewa,” Majuma alisema siku moja wakiwa nyumbani na mama yake.

“Ni kweli kwa sababu ulikuwa kifungoni. Nimefurahi sana kusikia hivyo. Sasa cha kufanya ni kupanga siku ili utoe ushuhuda kanisani. Tena sio ushuhuda tu na sadaka ya shukurani, nitaitoa mimi mwenyewe” mama Majuma alizungumza kwa furaha.

Basi kama ilivyopangwa siku ya Jumapili ilifika nao walikuwa kanisani. Ibada ilianza na kuendelea hadi ilipofika saa ya ushuhuda. Nafasi hiyo ilipotolewa, Majuma hakusita kwenda mbele akiwa na mtoto wake mgongoni. Alitoa salamu kwa waumini wenzake kisha alianza.

“Kuna siku mchungaji alizungumzia maagano. Nataka niwaambie kuwa kila alichokisema ni cha ukweli kwa sababu nimekutana nayo mimi mwenyewe.” Waumini walikuwa kimya kusikiliza.

“Nina ushuhuda ambao nitautoa lakini kabla sijaendelea naomba nitoe sadaka yangu ya shukurani.” Alitoa bahasha na kumkabidhi mchungaji kisha aliendelea kusimulia yote aliyokutana nayo. Alianzia mbali sana ili kila mtu aelewe. Kila mtu alikuwa kimya kusikiliza kwa makini. Wakati Majuma anaendelea kusimulia historia yake, wimbo unaoitwa *Ekwueme* ulikuwa ukisikika kwa mbali na kuongeza hisia kwa msimuliaji na wasikilizaji.

Katika masimulizi yake yote hakufanikiwa kufika nusu ya yaliyomtokea hasa yale mazito kwa sababu alikuwa analia sana na kanisa nzima lilitawaliwa na simanzi. Kila mtu alikuwa anafuta machozi. Wimbo huu uliendelea.

“Nashindwa hata kuendelea maana yaliyonikuta yanaumiza moyo wangu kila ninapoyakumbuka” Majuma alisema huku analia. Hata hivyo alijikaza na kuendelea kusimulia. Alisimulia shida ya upasuaji, jinsi alivyopata shida kuishi peke yake hasa baada ya upasuaji. Hata hakumaliza simulizi yake iliyobeba ushuhuda mkali,

“Naomba niishie hapo, hata hivyo namshukuru Mungu amenitazama” kanisa zima lililipuka kwa makofi.

“Hakika Mungu ni mkuu sana. Kuna wakati waweza kupitia magumu hadi ukaona labda Mungu amekuacha. Nikupongeze sana msichana wangu kwa sababu hukumwacha Mungu wako. Ni simulizi ya

machozi sana, nimeona hata akina baba wametoa machozi." Mchungaji alisema kisha akamgeukiaMajuma.

"Huyu ndiye mtoto wako?"

"Ndio, ni mtoto wangu baba mchungaji" Majuma alijibu.

"Anaitwa nani?"

"Bado sijampa jina"

"Anhaa! Basi leo hii atabatizwa. Atabatizwa kwa jina litakalomfanya awe baraka kwa familia yenu" mchungaji Miamba alisema. Alimuombea mtoto kisha alisema,

"Ninaitakasa nafsi yako, roho na mwili wako kufanana na jina la kiungu. Kuanzia leo wewe ni Nyota" mtoto aliitwa Nyota, kumbuka alikuwa wa kike.

Basi hayo yote yalipomalisika watu walitoka nje kwa ajili ya safari ya kurudi nyumbani, Majuma na mamake walikuwa pale nje pia.

"Oooh! Kumbe siku hizi yuko huku. Lakini anakaa wapi? Acha niwafuatilie hadi nijue mahali wanapokaa," ilikuwa sauti ya mtu aliyekuwa amemfuatilia Majuma tangu alipomuona kanisani. Alisema na kuwafuta kimya kimya. Safari ya kurudi nyumbani ilianza bila kujua kwamba walikuwa wanafuatiliwa kwa mbali na mtu. Hawakuwa na hili wala lile ama kweli jambo usilolijua ni sawa na usiku wa giza.

Kama kawaida ni mwendo wa nusu saa kutoka kanisani hadi nyumbani. Ndivyo ilivyokuwa, ni dakika thelathini tu ndizo zilitumika. Yule mwanaume aliyekuwa anawafuatilia taratibu alisimama umbali wa mita chache akichunguza kila hatua yao hadi walipoingia ndani ya nyumba.

"Oooh! Kumbe mnakaa hapo" Alisema kisha aligeuka na kuondoka kama mtu mwenye haraka.

"Hatimaye nimepajua sasa, nimehangaika sana kumtafuta. Hapa sasa cha muhimu ni kutengeneza mazingira sawa." Alizungumza maneno hayo yule mtu akiwa anatembea njiani.

"Waooooh! Nyota mjukuu wangu. Jina nzuri sana" Bi Saradibo alisema baada ya kukaa chini na mjukuu wake.

"Mama tunapika nini?"

"Pika tu ugali wewe ule, mimi bado niko sawa. Mboga naamini bado iko."

"Ndio mama ipo ile ilibaki kidogo"

"Lakini naamini itakutosha"

"Ndio"

"Haya, pika ule uje umnyonyeshe mtoto. Alafu kuna mazungumzo nataka tuongee." Bi Saradibo alisema.

Majuma aliingia jikoni na kupika ugali wa kumtosha kisha baada ya kula alifatisha ratiba nyingine hasa kumnyonyesha mtoto. Baada ya hapo sasa Bi Saradibo alianza kuzungumza.

"Kwa kweli binadamu tuna mapungufu sana. Ndio maana yupo Mungu wa kumwomba hasa unapotokea wakati ambao wewe upo nyuma ya mapungufu yako." Yalikuwa maneno ya Bi Saradibo.

"Ni kweli mama" Majuma alijibu huku yuko makini sana kumsikiza mamake.

"Enhh! Sasa mapungufu hayo ya kibidamu ndio huwa yananifanya niumie wakati mwingine nikisikia rafiki yako Fitina anaendelea tu na masomo, hana shida." Majuma aliguna baada ya kusikia maneno ya mamake. Mama aliendelea.

"Sina maana kwamba sipendi asome, hapana. Ila moyo wangu unaumia kwa sababu yeye yupo huko Kampala anasoma alafu wewe upo tu mtaani unateseka. Inaniuma sana kwa sababu naamini hata wewe ungekuwa chuo ukisoma." Maneno ya mama mtu na namna alivyokuwa akiyatamka yalidhihirisha maumivu makali yaliyokuwa yanautafuna moyo wake. Angependa sana mtoto wake wa pekee asome.

"Hakuna namna mama, ishakuwa tayari" Majuma aliongea kumtuliza mamake kisha akaendelea. "Hata mimi mwenyewe inaniumiza sana, lakini nitafanyaje?"

"Basi tu, tumwachie Mungu." Bi Saradibo alisema huku mkono wake wa kulia ukiwa kwenye shavu. Majuma alinyanyuka na kuwaacha Nyota na nyanyake pale nje. Aliingia chumbani kwake na kujilaza kitandani. Haikuwa kazi rahisi kusahau yote yaliyomsibu, labda atasahau lakini itagharimu kiasi kikubwa cha muda. Alikumbuka juhudi zake

katika masomo hadi wazazi wake walikuwa wamewamini na kumpenda sana. Alikuwa na ndoto mbali mbali lakini ndio zimeshapotea. Mbaya zaidi mtu aliyefanya yeye kuharibikiwa na maisha aliendelea na masomo na kwa sasa yuko chuo kikuu cha Makerere Uganda.

Zilipita siku tatu tangu siku ile. Ilikuwa siku ya Alhamisi. Bi Saradibo alikuwa amekwenda shambani kukagua mazao yake. Majuma alibaki na Nyota nyumbani kwa sababu hali yake haingemruhusu kufanya kazi ngumu. Mamake alifanya kazi hadi majira ya saa kumi jioni. Baada ya hapo aliongoza njia kurudi nyumbani. Kichwani alikuwa na furushi lenye vitu vingi mahindi kwa ajili ya kwenda kuchoma. Alitembea taratibu na kwa uchovu sana hadi alipofanikiwa kufika nyumbani. Hakutaka hata kuingia ndani, alitua mzigo wake kisha alijitupa chini kwa ajili ya kupumzika. baada ya dakika chache aliita.

“Majuma! Majuma! We mama Nyota!” aliita lakini hapakuwa na sauti yoyote kumwitikia wito wake. Alipatwa na wasiwasi, alisimama na kuelekea ndani ya nyumba huku akiendelea kuita.

“Mama Nyota!” bado hakujibiwa. Aliingia hadi chumbani kwa Majuma, ajabu ni kwamba Nyota alikuwa kitandani amelala mamaye hakuonekana.

“Mama yake ameenda wapi sasa?” alijiuliza bila kupata jibu. Maamuzi yaliyopita ndani yake ni kusubiri labda atarudi baadae. Usiku mkali uliingia, Majuma hakurudi. Wasiwasi mkubwa kwamba mtoto wake amepotea uliingia ndani yake.

# SURA YA KUMI

Machozi yalianza kumlenga machoni pake baada ya hayo mawazo kuchanganyika na sauti ya mtoto Nyota aliyekuwa analia, akihitaji kunyonya.

"Nimempoteza tena." Mama Majuma hakupika chochote cha kula usiku huo, alipika tu uji kwa ajili ya mtoto japo alikuwa hajafikia umri wa kula chochote. Alihitaji maziwa tu. Mawazo yalikitawala kichwa chake usiku wote, aliwaza hili na lile. Usingizi ulimpitia kushoto!

Yarabi! Mama Majuma hakuwa anajua kwamba mchana wa siku hiyo Majuma alitembelewa na wageni. Wageni asiowajua wala kuwafahamu. Walimsalimu na kisha wakajimbulisha kwamba wanatoka katika Taasisi Ya Agakhan hivyo wamekuja hapa kwa ajili ya kufahamu maendeleo yake. Pia kuongea naye zaidi kuhusu namna ya kufanya wakati mtu ana jeraha la oparesheni. Majuma alishangaa sana kwa yote hayo. Wamejuaje kama yeye ana hayo matatizo?

"Sasa tunakuomba tusongee hadi kwenye gari letu lile pale ili tuongee zaidi…kuwa na amani" mmoja kati ya wale watatu alisema. Majuma alisita lakini baada ya kushawishiwa sana alikubali. Walisongea hadi kwenye lile gari na kuingia ndani. Mazungumzo yalianza lakini kabla hata hawajaongea maneno mengi, gari liliwashwa na vioo vilifungwa kisha mafuta yaliganyagwa, gari liliondoka pale.

Majuma alifumbwa mdomo hata kelele alishindwa kupiga, hata hivyo hakuwa anafahamu ni wapi gari lile lilikuwa linaenda. Alichoshuhudia tu ni kitu kimoja baada ya vioo kushushwa. Alishuhudia jumba kubwa na zuri mbele yake na ndiko alikokuwa akipelekwa. Geti

lilifunguliwa, milango ilifunguliwa na kuingizwa hadi ndani kabisa ya jumba lile.

"Mweke hapohapo" kijana mmoja alisema. Majuma aliachiliwa na kuanguka chini. Wale vijana watatu walitoka na kufunga mlango. Hofu kubwa ilitanda moyoni mwake, hakujua yuko wapi na yupo hapo kwa ajili gani. Ukimya ulikuwa mkubwa sana mahali pale lakini ghafla alisikia mtu akikohoa, na kukohoa kwake kulisikika kama mtu aliyefanya hivyo huku mkononi akiwa na kipaza sauti. Majuma alitazama huku na huku bila mafanikio. Moyo ulidunda.

"Dada karibu sana" sauti tu ndio iliyosikika, yani mzungumzaji alikuwa na kipaza sauti. Alinyamaza kidogo kisha aliendelea.

"Natumai unaendelea vizuri hadi sasa. Ni furaha yangu kubwa sana kama matumaini yangu unaendana na uhalisia wenyewe."

"Na…ni…wewe?" Majuma aliuliza lakini aliishia kutoa kigugumizi tu. Woga ulimtawala kila kona.

"Huna haja ya kuogopa. Unaogopa nini? Kufa? Kama kufa ningekuwa nishakuua tangu zamani." Ile sauti ilisikika. Hofu iliendelea kutanda ndani ya Majuma. Hakujua ni kwa nini angeweza kuuwawa zamani.

"Najua unatamani sana kunijua, nami sina shida na hilo. Mimi ni yule niliyekuwa nakupa msaada wa vitu mbalimbali." Sauti ile ilisikika na kumwacha Majuma katika vuta nikuvute ndani ya nafsi yake. "Alinijuaje? Alinijulia wapi?" Majuma alijiuliza na kutamani kufahamu zaidi hasa kumjua kwa sura huyo mtu.

Kweli kama ilivyokuwa tamaa yake Majuma, yule mtu alianza kupiga hatua kuelekea alipokuwa. Moyo ulimdunda. Muda mfupi tu, yule mtu alifika lakini Majuma hakufanikiwa kumtambua yule mtu kwani usoni mwake alivalia barakoa.

"Najua unanifahamu lakini sitaki unifahamu kwa utambuzi wa macho" aliongea na kutoa sauti ya kicheko kidogo. Kwa kuwa sasa hakuwa anaongea kwa kutumia kipaza sauti, sauti yake ilisikika vyema na kwa Majuma aliwahi isikia mahali.

“Kuwa na amani na usiogope chochote kile” yule mtu aliongea na kuanza kutoka nje. Majuma alimgeukia.

“Nitaondoka saa ngapi?” aliuliza lakini hakujibiwa. Majuma aliachwa pale ndani hadi masaa ya usiku. Na ilipotimia saa mbili usiku ule mlango ulifunguliwa kisha aliingia yule mtu aliyekuwepo awali. Alikuwa na barakoa yake vilevile ila alipofika mahali Majuma alikuwa, alianza kuivua taratibu. Macho ya Majuma yalimtoka ndii, alikuwa tayari kumuona huyu mtu. Ajabu ile mask ilivyovuliwa tu, na taa zikazimwa.

“Utanijua tu. Ipo siku” alisema na kutoa amri kwa kidole kisha dakika chache watu walianza kuingia wakiwa wamebeba vitu tofauti tofauti. Majuma hakujua ni vitu gani kwa sababu kulikuwa na giza.

“Kabla ya kuendelea na mengine, ningependa ufahamu kwamba nimekufuatilia kwa ndani zaidi, napafahamu ulipokuwa unakaa, najua shida zako. Na ndio maana sikuona shaka kukusaidia.” Yule mtu aliongea.

“Nashukuru” Majuma aliongea kisha yule mtu aliendelea.

“Leo nataka ufahamu hatima yangu pia. Sitaki uendelee kuteseka. Kwa hivyo, jipange na ujiandae tuishi pamoja ili nikusaidie tukiwa pamoja pia nisaidie ndugu zako. Yani nataka niishi na wewe kama mke na mume, na hii ndio sababu ya kuleta hapa ili ujue.” Alisita kidogo.

“Hey! Songeni hapa” alitoa amri kwa wale watu waliomzunguka. Haraka bila kupoteza wakati walisongea.

“Kuna vitu gani hapo?” aliuliza

“Mkuu vipo viroba viwili vya unga pamoja na mchele” kijana mmoja alijibu

“Ni hivyo tu?” aliuliza tena

“Hapana kuna mtungi wa gesi pamoja na nguo za mtoto” mwingine alijibu.

“Okay men.... Hakikisha amefika salama pamoja na hivyo vitu vyake vyote.” Aliamuru.

Majuma kusikia hivyo alipata amani kubwa moyoni mwake na shauku ya kumfahamu huyu mtu mwenye roho nzuri kiasi hiki.

"Yatafakari niliyokwambia. Pia ukiwa tayari siku moja nielezee ni nini kilitokea maishani mwako" yule mtu alisema. Majuma alibebwa kwenye gari pamoja na vile vitu vyote kisha safari ya kurudi nyumbani ilianza. Ilikuwa saa tatu kasoro usiku. Majira ya saa tatu na dakika zisizopungua thelathini alifikishwa nyumbani kwao na kusaidiwa vile vitu hadi mlangoni. Baada ya hapo wale watu waligeuka na kuondoka. Aliamua kupiga hatua na kuusongea mlango. Alisita kwanza baada ya kujiuliza ni mambo gani ataulizwa na mama yake na atamjibu nini. Lakini kwa sababu hakuwa sehemu mbaya kufanya ubaya, hakuona sababu ya kuogopa. Sauti ya mtoto Nyota aliyekuwa analia ndani iliamsha nguvu ya kuinua mkono na kugonga mlango.

"Hodii!" aligonga na kuita mara kadhaa hadi muda ambao mama yake alitoka kumfungulia.

"Wewe mama Nyota, ulikuwa wapi? Unaondoka na kutuacha tena bila taarifa!" yalikuwa maneno ya mwanzo na punde baada ya kufungua mlango.

"Mama, usihofu, mimi niko salama. Acha tuongee kesho maana nimechoka na nina usingizi. Niruhusu tu mama" Majuma alimwongelesha mamake kwa upole.

"Kazi ni unitia mawazo tu. Muda kama huu mimi huwa nishalala lakini ona, usingizi sina" Bi Saradibo alilalamika.

"Samahani mama, kesho tutaongea vizuri tafadhali" Majuma alimsihi mamake.

"Haya na hivi ni vitu gani?" Bi Saradibo aliuliza

"Ni mtungi wa gesi na kiroba cha unga na mchele" Majuma alijibu na kujaribu kuinua kile kiroba.

*******

Siku nyingine majira ya asubuhi walikaa na kuzungumza kuhusu hili lililojiri hapo jana. Ilibidi Majuma aeleze yote ii kumtoa wasiwasi mama yake.

"Hata mwenyewe nilikuwa na wasiwasi mkubwa lakini baada ya muda nilikuwa sawa tu." Majuma alisema

“Ah! Hata kama ipo hivyo lakini kupata mashaka ni jambo lisiloepukika. Kwa hivyo hata hivi vitu umevipata huko?” mama mtu aliuliza.

“Ndio, na hajaanza leo, alianza tangu nikiwa Murumba” Majuma alijibu na kuficha kabisa habari ya kwamba hakumfahamu mtu yule.

“Nashukuru sana Mungu ambariki yule baba.” Yalikuwa maneno ya Bi Saradibo ambaye bado hakuwa sawa kwa asilimia mia moja. Wakati huo huo pia haikuwa mwisho wa mvurugano wa mawazo kichwani mwa Majuma, yule mtu ni nani? Na kweli amedhamiria kumuoa kweli? Kiujumla ni maswali mengi yalipita kichwani mwake. Aliamua kuyapuuza maana majibu ya maswali hayo hayakuwa rahisi kuyapata.

Maisha yaliendelea kusonga huku kila baada ya wiki kiroba cha mchele kikawa kinaletwa nyumbani kwao. Njia iliyokuwa inatumika kuleta viroba hivyo hamna aliyejua kwani vilikuwa vinawekwa ndani majira ya usiku na Majuma angevikuta asubuhi pale nje.

"Fanya mpango sasa nimuone huyu kijana yangu anayetushibisha” yalikuwa b maneno ya mama mtu.

“Usijali mama, utamuona tu japo yeye mwenyewe anasema huu sio wakati mwafaka kwake kujiweka wazi” Majuma aliamua kudanganya maana hakuwa na namna nyingine ya kusema.

“Ni vyema aje nimshukuru maana anatulea, ona ulivyonawiri mwanangu” Bi saradibo alisema.

Ni kweli kabisa Majuma alikuwa anapendeza kwani nuru ilikuwa imerudi usoni mwake, ile sura ya kizee iliyokuwa imebadili uso wake ilipotea. Tabasamu mwanana iliupamba uso wa Majuma. Siku fulani ya Jumatatu kama kawaida majuma huwa wa kwanza kuamka, basi alitoka nje na moja kwa moja macho yake yalitua kwenye begi lililokuwa mbele yake. Lililkuwa begi la nguo zake na za mtoto. Alipochunguza vizuri alikutana na rununu, alipowasha tu ujumbe uliingia.

“Naamini umefurahia, mwambie mama naye kuna mzigo wake wa nguo. Pia kwa muda mfupi kuanzia sasa utanifahamu kwa sababu tayari nimeandaa kila kitu kwa ajili ya kuishi nawe” Majuma alishangaa kuangukiwa na nyota ya jaha. Majuma alilala kwa huzuni akaamkia dunia tofauti ya furaha. Ama kweli akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Majuma

hakuwahi taka kupoteza bahati hii ya mtende naye akaapa kutolipa ubaya kwa wema. Alifurahi sana kwa upande mwingine baada ya kukubaliwa na baadhi ya wanadamu.

Ni miaka miwili imepita sasa. Mtoto Nyota alikuwa mkubwa pia hivyo ni miaka miwili bila Majuma kufanikiwa kumuona huyu mtu ambaye alijitokeza na kumpenda Majuma bila kujali utofauti wa matabaka.

"Ni muda sasa sijakuona na bado hutaki nikuone," Majuma alisema. Matunzo aliyokuwa anayapata yalifanya urembo wake wa zamani urudi upya licha ya kuwa na mtoto. Alisema hayo siku moja walipokuwa wanazungumza kupitia kwenye rununu.

"Haya sasa jiandae kesho tuonane. Vijana wangu watakuja kukuchukua saa tano asubuhi" ile ilikuwa sauti ya yule mwanaume. "Ni kweli? Maana kipindi cha nyuma ulinambia tuko karibu kuonana lakini ni miaka miwili sasa" Majuma alidadisi. "Basi naomba uniamini mpenzi wangu, kesho tutaonana"

"Sasa naomba usiivunje imani yangu tena" Majuma alijibu.

Baada ya mazungumzo hayo ambayo hayakuwa marefu sana, walitakiana usiku mwema. Kila mmoja alilala ila hamu iliyokuwa ndani ya moyo wa Majuma ilimfanya achelewe kulala. Hamu ya kumuona mwenzake ilimpanda. Masaa ya usiku yalikimbizana na hatimaye asubuhi ya siku nyingine ilizaliwa. Kama ilivyokuwa ahadi basi majira ya saa tano na dakika chache gari nyeusi aina ya BMW liliegeshwa karibu na nyumbani kwa akina Majuma. Majuma alikuwa tayari ameshajiandaa, hivyo aliaga pale nyumbani na kuelekea mahali palipokuwa na lile gari.

Safari ilianza kwa kasi. Majuma alitamani afike haraka kwani aliona anachelewa. Baada ya angalia angalia zake hatimaye walifika eneo lile lile ambalo aliletwa mwanzo. Alipelekwa hadi ndani kwa heshima kubwa kisha wale vijana walitoka nje. Sebuleni hapakuwa na mtu mwingine hivyo palikuwa kimya kabisa. Ule ukimya ulimpa nafasi ya kusikia kwa ufasaha zaidi hatua za mtu aliyekuwa anatembea kuja pale. Moyo wa Majuma ulidunda na kuongeza mapigo, aliyaandaa macho yake kumuona mtu yule. Sekunde tano hatimaye macho ya Majuma yalitua kwenye kiatu kilichokuwa mbele yake, kiatu cheusi tititi kama usiku

usisokuwa na mbalamwezi kilichokuwa kinang'ara kwa kiwi. Macho yake yalipopanda hadi usoni, alikutana na uso mweupe. Alaah! Majuma alijaribu kuweka jambo fulani sawa akilini mwake kisha kwa mbali alikumbuka kwamba aliwahi kumuona huyu mtu mahali. Ni wapi? Hakuwa na uhakika.

"Karibu sana mpenzi. Hakika umependeza hadi nimepata mkanganyiko katika utambulizi." Yule mtu alisema na kuketi kwenye kochi. Marashi murua yenye uturi wa muwaridi yalikolea na kusambaa kila sehemu ya chumba hicho.

"Nashukuru sana" Majuma alisema na kutoa tabasamu fupi. Mawazo yake yalikuwa na kazi moja, "Nilimuona wapi?"

Salamu zilifuata, kila mmoja alimsabahi mwenzake. Baada ya hapo mazungumzo yalianza na bila kupoteza wakati, yule bwana alianza kuzungumza.

"Najua uko na mengi ambayo unataka kujua lakini naomba nijitambulishe kwako kwa kueleza haya. Usichoke kunisikiliza tafadhali." Alikohoa kidogo na kuendelea.

"Mimi ni wa pekee niliyebaki katika familia yetu baada ya kumpoteza kaka yangu Mwele kwa ugonjwa wa moyo ambao kama familia ingekuwa na pesa angetibiwa na kupona. Nimekulia katika familia ya kimaskini sana, chakula kilikuwa cha shida hasa baada ya baba mzazi kutukimbia. Mama mzazi alinisomesha kwa shida sana, alifanya kazi ngumu na kwa muda mwingi ili apate pesa ya kunipeleka shule. Si haba niliendelea na shule na nikafanikiwa kufika kidato cha kwanza kwa msaada wa mama. Lakini kutokana na hali ya kufanya kazi ngumu na kwa muda mwingi, alipata matatizo sugu ya kifua yaliyochangia kuipa dunia mkono wa buriani. Niliishiwa nguvu sana maana sikuwa na mtetezi. Hata hivyo nakumbuka wasia wake kabla hajafariki kwamba sitakiwi kulia kwa kile kitakachotokea bali nisimame imara ili nipambane nifikie malengo. Kubwa zaidi, alilonambia ni kwamba nitakuwa namuenzi endapo nitakuwa mtu wa kusaidia binadamu wenzangu wenye shida. Ni kama alitambua kengele ya mauti ilikuwa mlangoni pake." Alitulia kidogo baada ya kumuona Majuma akilia. Alimbembeleza kisha alisema;

“Nilipata mfadhili baada ya juhudi zangu shuleni. Alinisaidia nikasoma hadi chuo ambako nilikuwa nasomea udaktari. Namshukuru Mungu nilipomaliza nilipata kazi huku Kakamega. Haya yote yamechangizwa na kujitoa mhanga kwa shujaa wangu kipenzi, marehemu mama. Mimi nimekaa hapa sana na sio kukaa tu bali huwa napendelea kuzunguka hasa wikendi. Nakumbuka ilikuwa wikendi moja nilikuwa nazunguka, nilifanikiwa kumuona msichana mdogo ambaye kwa muonekano tu alitambulikana ni mwenye mateso. Alinikumbusha namna mama yangu alivyokuwa akiteseka na kuhangaika hapa na pale. Nilipata shauku kumfuatilia na nilifahamu hadi mahali alipoishi. Kwa kweli kila kitu chake kilinitia simanzi kubwa. Nilikosa namna ya kumsaidia ila nafsi ilinisuta sana. Niliwaza iwapo nitampa msaada wa moja kwa moja angeupokea? Angeniamini kweli? Baada ya kujiuliza hivyo nilikaa bila kufanya chochote hadi wakati nilipokutana naye hospitalini ambako alikuja kwa ajili ya kujifungua mtoto ila kwa bahati mbaya alitakiwa kufanyiwa upasuaji kwa sababu mtoto wake tumboni alikuwa amekaa vibaya.” Majuma alishtuka kusikia hivyo. “Huyu msichana ni wewe” yule mtu alisema na kufuta machozi usoni mwake.

Majuma alipata picha halisi ya mtu huyu sasa, kumbe alimuona hospitalini. Huyu ni Dkt Sanda. Dkt ambaye hata ile siku ya upasuaji wa Majuma alilengwalengwa na machozi.

“Sijui niseme nini” Majuma alisema na kupiga magoti huku akilia. Moyo wake ambao ulikumbwa na mengi hakika ulitoneshwa yale majeraha machungu. Hata hivyo hakuacha kutoa shukrani kwa dokta Sanda.

“Sina la kusema zaidi ya neno nashukuru sana” Majuma alisema.

“Ondoa shaka, napenda ufurahi, najua hata kipenzi changu huko peponi anafurahi kwa sababu ya hili.” Dkt Sanda alisema

“Nashukuru sana, ila nina ombi moja kwako” Majuma alisema.

“Omba chochote nami niko tayari kukifanya hata sasa hivi” Sanda alisema akiwa anamaanisha anachokisema.

“Kweli?” Majuma aliuliza.

“Sitegemei kama kufikia sasa bado huniamini. Usiwe na hofu kwangu” Dkt Sanda alijibu

"Mamangu anataka kujua, tafadhali njoo nami twende nyumbani." Ndilo ombi langu"

"Anhaa lakini..." Sanda alimeza maneno

"...jamani mpenzi wangu, kumbuka umeniahidi utafanya chochote nitakachokiomba" Majuma alizungumza Majuma.

"Sawa, hakuna namna" alijibu.

Saa nane mchana walikuwa ndani ya gari wakielekea nyumbani kwa Bi Saradibo. Safari iliendelea hadi saa nane na dakika hamsini walipowasili nyumbani. Ilikuwa furaha kubwa sana kwa Bi Saradibo kumuona daktari Sanda ambaye hakuacha kujitambulisha nakueleza mengi yafananayo na yale aliyomsimulia Majuma na mengine mengi. Katika mazungumzo hayo, Sanda alijikuta akiongelelea suala lile la kuhitaji kuishi na Majuma kama mke na mume. Kwa kweli mama mtu hakuwa na kinyongo juu ya hili.

"Mimi sina tatizo na hilo, cha muhimu mmekubaliana. Katika ndoa ni upendo na kuheshimiana" Bi Saradibo alishauri.

Siku zilizonga, mipango ya ndoa ilianza kufanyika huku msimamizi wa masuala yanayohusu pesa yakifanywa na Dkt Sanda. Hili jambo halikuwashangaza watu tu bali hata Majuma na Bi Saradibo hawakuacha kushangaa.

Maisha yalikuwa mazuri ndani ya kasri la Sanda. Siku moja Dkt Sanda akiwa chumbani na aila yake.

"Umri wa mama umeenda sana hivyo hapaswi kukaa peke yake. Tufanye mpango ahamie hapa" doctor Sanda aliyasema hayo wakiwa wamekaa sebuleni.

"Ni kweli ila sina uhakika kama atakubali. Huyo mama kumtoa kwa kaburi la mzee wake si jambo rahisi." Majuma alisema huku akijua kulikuwepo na mtihani mgumu.

# SURA YA KUMI NA MOJA

Miaka iliendelea kusonga, furaha na imani vilitawala maisha yao. Majuma hakuacha kumshukuru Mungu kila siku maana alimtendea makuu. Nyota kwa wakati huo alikuwa na umri wa miaka mitano kwani mwonekano wa urembo wake ulikuwa wazi kama maneno ya ngiri kwani alikuwa shilingi kwa ya pili na mamaye Majuma.

"Hatutakiwi kuongeza mtoto, tumlee huyu aliyepo" yalikuwa maneno ya kila mara ya doctor Sanda akimsisitiza mke wake, Majuma. Nyota aliendelea kukua huku akilelewa katika maadili makubwa na heshima kubwa sana. Kila alichokihitaji alipewa lengo likiwa ni kumjazia furaha ambayo mama yake na huyu baba yake waliikosa kipindi cha nyuma. Ujanja wa mtoto Nyota ndio uliochochea mioyo ya wazazi hawa kufikiria kumpeleka shule. Nyota alisajiliwa kuanza shule. Asubuhi alipelekwa kwa gari, jioni vilevile na baba yake aliyekuwa anatoka kazini. Nyumba ilichangamka kutokana na uwepo wa Nyota. Miaka ilisonga hatimaye alikuwa gredi ya pili. Siku moja simu ya Sanda iliita, ilikuwa namba geni.

"Haloo! Ni bwana Nick mkuu wa shule ya Nalonja Academy" ilikuwa sauti ya mkuu.

"Ahaa, habari mkuu" Sanda alimsalimu. Na baada ya salamu Nick alizungumza.

"Jambo lililonifanya nikupigie simu ni juu ya huyu mtoto wako Nyota. Hakika anashangaza sana, mtoto anayajua hata mambo hajafunzwa. Kiufupi ana akili zisizo za kawaida." Dick alisema. Dkt Sanda alishangazwa na taarifa hizi japo kwa namna fulani alikuwa anaona mwenendo wa Nyota.

"Sasa naona tumrushe gredi yani aende tu gredi ya tatu au hata nne." Hayo yalikuwa maneno ya bwana Dick mkuu wa shule.

Mtoto Nyota alikuwa mwerevu kama jina lake kwani aling'aa kwa kila Jambo. Kwa upande mwingine alipendeza na kupendwa na watu wengi maana alikuwa na mvuto wa kipekee ambao ungeenea kwa haraka kama uturi wa muwaridi unavyoenewa kwa kasi. Kutokana na tazama tazama za wazazi wa nyota, alikuwa anapenda michezo ya kutangaza pamoja na maswala ya siasa. Huu kwake haukuwa mwisho kwani nyota njema huonekana asubuhi. Alipofika gredi ya tano alipewa nafasi ya kuwatangazia wageni waliokuwa wamekuja shuleni ili kufadhili watoto mayatima. Alisimama na kuelekea jukwani.

*"Hatari! Hatari! Hatari bin hatari! Ukisikia jina hatari, taadhari kabla ya hatari!*
*Kata abadani katan kukutana na jina hatari! Corona!*
*Corona kisha jaa jaa ulimwenguni, linabisha bisha kama bishi la ubwabwa,*
*Linatesatesa kama mama wa kambo mpango wa kando kando,*
*Linakita na kupenya mizizi kama mti wa cacta, linatetema na kutetemesha ardhi nikitete mtete.*
*Linawapa watu matukule na majugajuga kisha linawaangamiza huku wanapayapaya.*
*Mukhtasar wake tu!*

Vile vile katika gredi ya tano alihudumu kama head girl. Aliitumikia vizuri nafasi hii na hakika kila aliyemuona alimpenda sana. Roho ya uongozi haikumuacha, alikuwa kiongozi wa wanafunzi hata wakati wa kidato cha tano na cha sita. Aliwaongoza wenzake kwa hekima na busara.

"Huyu mwanafunzi atafika mbali sana" yalikuwa maneno yaliyotamkwa mara kwa mara katika vinywa vya waliomshuhudia hasa walimu wake. Ushawishi wa mwalimu wake wa michezo na burudani uliongeza nguvu ya kutaka kusomea uandishi wa habari. Ulipofika wakati wa kwenda chuo, alichagua hii kozi. Bi Saradibo wakati huo alikuwa amekula chumvi kwani uzee ulikuwa umepokea mara nyingi angetembea kwa msaada wa mkongojo.

“Mungu naomba usiichukue roho yangu hadi nitakaposhuhudia matunda ya mjukuu wangu. Nyoosha njia ya mafanikio yake.” Yalikuwa maombi ya Bi Saradibo. Wazazi hawakuacha kumuombea kwani maombi yalikuwa na nguvu sana. Jambo lililokuwa gumu kwa wengine, Nyota alilifanya huku akitabasamu kwani kwake lilikuwa kama kupiga meno mswaki.

Kazi ya utangazaji alianza akiwa mwishoni mwa mwaka wa tatu wa masomo yake. Vyumba mbali mbali vya utangazaji vilipenda sana kufanya kazi naye kwani sauti yake ilidhihirisha kipaji. Muda ulifika ambapob alirudi nyumbani Kakamega, aliporudi watu nao hawakumuacha kumuuliza maswali na mapendekezo chungu nzima.

“Gombea ubunge, unafaa sana.” Nyota alibaki kushangaa. Mama yake naye alijawa na furaha kwa sababu ya mazuri yote yaliyojiri kwa mwanae.

“Baba, nitaweza kweli?” Nyota aliuliza.

“Hakuna mtu aliyewahi kuwa na uhakika wa uwezo juu ya kitu ambacho hajawahi kufanya. Hao wabunge na mawaziri unaowaona hawakuwahi kujua. Najua pesa unazo lakini mimi babako nitalipia mwenyewe. Nenda uchukue fomu ya ubunge.” Dkt Sanda alimaliza kuzungumza.

“Hutakiwi kuwa na hofu, tena isitoshe wananchi wenyewe ndio walipendekeza hili. Usiogope mamangu.” Majuma alisema.

“Sawa nimewaelewa sana wazazi wangu, lakini naomba msiache kuniombea maana maombi yenu ni chachu kubwa ya mafanikio kwangu.” Nyota alikubali kugombea ubunge. Baada ya kuchukua fomu alifuata taratibu zote hadi wakati wa kampeni zake ambazo zilijaza watu waliokuwa wanamshangilia hadi anakosa nafasi ya kuongea. Mungu si athumani, alifanikiwa kushinda katika matokeo ya uchaguzi huo. Aliingia bungeni, hoja zake bungeni zilikuwa na mshiko pamoja na ushawishi wa hali ya juu. Ni hoja hizi hizi zilizofanya ateuliwe kuwa waziri wa burudani, Sanaa na michezo. Maendeleo ya michezo na sekta mbalimbali kama barabara na maji halikuwa jambo la kuuliza. Nyota alikuwa mwanamke mchapakazi kwelikweli. Jina lake lilikuwa ngumzo katika vyombo vya habari, mara Nyota Joshua ni mchapakazi, Nyota Joshua ni

kiongozi shupavu mwenye msimamo. Hizi taarifa zilisambaa nchi kwani aliye na macho haambiwi tazama.

"Nawashukuru sana wazazi wangu maana nyinyi ndio mlioamsha mafanikio ya jambo hili." Nyota aliwaambia wazazi wake siku moja wakiwa pale nyumbani.

"Usijali mama, cha muhimu ni kuendelea kumuomba Mungu aendelee kufungua milango ya furaha maishani mwako na kuifunga ile ya vilio na huzuni ambayo ilikuwa upande wetu sisi wazazi wako" yalikuwa maneno ya Majuma ambaye bila kubwabwaja maneno ni kwamba alimkirimia mwanae baraka zote.

Ndoa ya Nyota na Hassan ilikuwa ya kupendeza sana kwani kwao hawakukosa furaha "Mungu naomba usiichukue roho yangu hadi nitakaposhuhudia matunda ya mjukuu wangu" Kwa mara nyingine yalikuwa maneno ya bibi yake akiwa amelala chumbani, umri wake ulikuwa umeenda sana.

Nyota na bibiye walikuwa marafiki wakubwa sana, mara nyingi akiwa hapo nyumbani, hutumia muda wake kupiga soga na bibi yake kipenzi japo uwezo wa kuongea wa bibi huyu ulianza kupotea. Hakuwacha kumuombea baraka kwa kumshika kichwa mjukuu wake hadi wakati ambao mwenyewe aliridhika

"Mjukuu wangu fuata njia ile ile ya malezi ya wazazi wako. Waheshimu na uwapende wananchi wako unaowaongoza pia usisahau kusamehe. Najua kuna mengine mengi sitashuhudia kwa macho ila roho yangu itaiona haya. Mungu akupe mema makubwa hadi ushangae"

"Amina bibi yangu" Nyota alijibu. Bibi alipomaliza hayo alijikakamua na kukaa kitako kisha akamshukuru Mungu na kusema,

"Ee Mungu nimeshuhudia mengi ya mjukuu wangu, sasa unaweza nipumzisha" yalikuwa maneno ya Bi Saradibo usiku moja kabla ya roho yake kumtoka. Ilikuwa simanzi kwa Nyota lakini haidhuru kwani aliwahi kuambiwa,
"Nikifa usilie bali furahi kwani itakuwa furaha yangu pia. Ukilia utaniumiza. Huko niendako naenda kukuombea zaidi."

*******

Miaka miwili ilipita kazi za serikali zikiendelea. Kila utendaji wake wa kazi uliinua daraja la uaminifu kwa wale anaowaongoza na kwa wale walio juu yake. Na kama ilivyo ada uchaguzi hufanyika kila baada ya miaka mitano, wakati ulipofika nafsi yake ilimtuma achukue fomu ya urais japo alisita kidogo. Mume wake Hassan alimtia moyo kwamba yote yawezekana endapo ataamua na kushirikisha Mwenyezi Mungu. Nyota alichukua fomu ya urais na siku ya kuchukua fomu hii alikuwa pamoja na mgombea mwenzake wa kiume pamoja na familia yake. Alipopewa nafasi kuzungumza alitoa salamu kisha akasema,

“Ndugu zangu nawashukuru sana kwa yote. Lakini nitakuwa mbaya sana wa shukurani na fadhila endapo sitamshukuru Mungu pamoja na viumbe vya dhamana sana kwangu. Mama naomba simama uje mbele pamoja na baba.

”Mama Nyota alikuja mbele na kupewa nafasi ya kuongea. Mama Nyota ambaye ndiye Majuma hakuacha kueleza yale mazito yaliyomkuta na kumalizia jambo hili, “Nilifikia hatua ya kutaka kufanya dhambi kutoa ujauzito. Sijui leo mngemuona wapi huyu mgombea wenu” alisema na kutabasamu watu nao walichombeza kicheko kidogo.

Baada ya mengi Nyota alichukua tena kinasa sauti, “Pia namshukuru sana baba kwa kunitunza na kunilea vyema” Dkt Sanda ambaye naye umri ulisonga alipewa nafasi kuzungumza naye alizungumza ya kwake kisha Nyota aliendelea kusema.

“Jamani hayo mlioyasikia ndiyo yaliyomkuta mama yangu ambaye mimi namuita shujaa kwa sababu hakukimbia vita, alipambana nayo mwanzo hadi mwisho. Hakufikiria kutoa ujauzito ambao ni mimi wala hakufikiria kunitupa ama kunitelekeza licha ya hali ngumu katika afya yake na maisha kiujumla. Jamani mama anajua uchungu wa mtoto, hata awe wazimu, hawezi kumtupa mwanae. Na iwapo utampata mwanamke amemtupa mtoto, basi huyu sio mwanamke ni binadamu mwenye jinsia ya kike tu. Asante mama kwa mapenzi yako." Alisema na kumkumbatia mama yake. Hili tukio lilikuwa linaruka mubashala kupitia televisheni mbalimbali pamoja na redio.

Sasa kumbe hii siku bwana Joshua alikuwa ndani ya banda fulani la TV akiangalia hili tukio. Hakufahamu kama yule ni mwanae lakini yale aliyoyasikia yalimfanya aamini kwamba hakika yule ni mwanae wa damu hasa baada ya kumuona Majuma pia baada ya kusikia jina la pili la yule mgombea, Nyota Joshua.

"Yule ni mwanangu, mwanangu anagombea urais" alisema na kujipika kifua. Alijisifu kwa sauti yake ya kukwaruza. Sauti ilikwaruza kwani licha ya uzee, alikuwa anakunywa sana pombe pamoja na kuvuta sigara.

"Msichana wangu anagombea urais alafu mimi nipo hapa nateseka na mapombe huku Kawangware. Lazima niende nimuone, ile ni damu yangu" alisema siku moja baada ya kuona mambo yamemfika shingoni. Hakujua aende Nairobi eneo gani ili kuwapata watu anaowahitaji. Aliona ni vyema afanye kuomba omba hadi alipopata nafasi ya kwenda Kakamega. Baada ya kuuliza uliza alipelekwa hadi nyumbani kwa wazazi wa Nyota. Baada ya kubisha hodi, alikaribishwa na kuanza kujieleza.

"Mimi ni bwana Joshua, samahani sana wazazi wenzangu nimekuja kumuona mwanangu."

"Mwanao yupi tena?" Majuma aliuliza baada ya kumtambua bwana huyu. Hali pale ndani haikuwa nzuri, Majuma alikasirika sana na hakutaka kumuona kabisa mzee huyu maana kumwona kulimsababishia akumbuke machungu aliyoyapitia. Ulikuwa ni ugomvi mkubwa. Aliyekuwa akizuia baya lisitokee alikuwa Dkt Sanda ambaye upo wakati naye alikuwa akizidiwa nguvu. Ilikuwa ahueni muda fulani ambao mlango uligongwa na kuingia Nyota na mume wake waliokuwa wamekuja kusalimu Majuma babake Sanda.

"Mama kuna nini tena?" Nyota alishangaa ilibidi aelezewe yanayoendelea hapa. Alishtuka zaidi kusikia hivyo.

"Kama huyu ndiyo baba mzazi alikuwa wapi kipindi chote?" Nyota alihoji.

"Alinitelekeza pekee yangu," mama Nyota alidakia. Hakika hii habari ilimuumiza sana Nyota na alichukia sana. Ila ghafla kumbukumbu zake zilirudi nyuma na kukumbuka wasia wa bibi yake juu ya kusamehe. Aliamua kusamehe na kujitahidi kumuweka sawa mama yake. Ilikuwa

kazi ngumu kuelewa lakini mwisho alikubali kusamehe pia. Bwana Joshua alisamehewa.

Baada ya muda kidogo mlango ulibishwa tena, kabla haujafunguliwa, yule mgongaji kwa Fujo huku akihema kwa nguvu. Aliingia na kwenda kujitupa chini ya miguu ya Majuma.

“Majuma rafiki yangu nisamehe. Nisamehe sana mwenzako nateseka na laana.” Yule mtu alisema kwa uchungu.

“Huyu ni nani tena mama?” Nyota aliuliza.

Huyu alikuwa ni Fitina. Baada ya kusababishia Majuma matatizo alianza kuishi pekee yake huku akijihisi huru zaidi kiasi cha kuingiza wanaume pale kwake. Aliingiza wanaume wa kila aina; si wafupi kama mbilikimo, si wanene kama nguruwe, si warefu ja mlingoti, si matajiri, si maskini, si weupe pepepe, si weusi kama makaa hadi mwenye nyumba alipoamua kumfukuza kwa kugeuza chumba chake danguro. Alipofukuzwa aliendá kuishi kwa mwanaume mmoja huko mtaani huku akiendelea na masomo ya kidato cha sita. Baada ya kumaliza aliingia chuoni na akafanikiwa kupata ndoa. Kwa bahati mbaya ndoa hii haikudumu kutoka na kukosa mtoto. Fitina alikuwa ameavya mimba nyingi wakati akiwa chuoni.

Baada ya ndoa kuvunjika alifukuzwa na bila kuogopa chochote aliamua kuwa kahaba wa kutupwa naye akacheza mchezo wa nipe nikupe. Alipenda sana kunywa pombe jambo lililomsababishia ugonjwa wa saratani. Ugonjwa wa ukimwi nao ulimtafuna na kumuacha mifupa na kichwa pekee. Hakika Fitina alitia huruma. Majuma alimuhurumia rafiki yake hivyo alimsamehe na kwa ushirikiano na mume wake pamoja na Mheshimiwa Nyota walifanya mpango kuwapeleka kwenye matibabu. Fitina alipelekwa hospitalini wakati huo bwana Joshua alipelekwa kwenye shirika maalum kwa ajili ya wale walioathirika na vitu mfano wa dawa za kulevya.

Baada ya muda, ganga ganga za madaktari hazikuzaa matunda. Uwele wa ukimwi hata baada ya funzo ya kukosa amani na mtoto kwake hayakumpa fursa ya kuishi tena. Afya yake ilizidi kunyong'onyea na kudhoofika sana, Fitina akazidi kukonda na kukondeana siku nenda siku rudi. Madaktari na manesi wenye tajiriba mbali mbali walileta kwa

uongozi wa Dkt Sanda angalau kutia marafiki wa karibu tumaini ya kuishi, mshumaa wa tumaini uliwashwa lakini ulianza kuteketea kila baada ya sekunde.

Siku moja ya ajabu baada ya yote, habari za kusikitisha zilitetemesha nchi nzima baada ya tarifa kueneshwa katika vyombo vya utangazaji; Si majarida, si televisheni, si redio, si fesibuku, si twita, si wazapu. Fitina alipatikana amefariki baada ya mwili wake kukosa nguvu ya kukabiliana na aina fulani ya tembe. Sivyo tu, Joshua naye siku ile Ile alipatikana karibu na mto huku akiwa amerejesha kope zake tayari kwa Muumba, siku zote maisha ni mshumaa usokuwa mkesha naama mshahara wa dhambi ni mauti.

Baada ya uchaguzi jina Nyota lilipitishwa katika mchujo ule ndani ya chama chake. Nyota lilivyo jina lake sasa akang'aa zaidi ya wengine. Ilikuwa jambo aula na la kushangaza kuwapiku wagombezi wake zaidi ya wanaume wanane bila kutia jasho walivyofanya wao. Ama kweli Chanda chema huvikwa pete. Jina Rais liling'aa kila pande ya nchi hasa tamko mwanamke Rais likawa la kwanza kuingia vinywa vya watu. Uchungu wa Majuma uligeuka sherehe yenye vitamu na vinono. Majuma kwake aliridhika kwani Chozi lake lilikuwa limebadilika na kuwa furaha yenye tabasamu.

"Mungu si mtu. Mungu siku zote hamwachi mwanawe." Alijiambia Majuma huku ameketi ikulu ya mwanawe.

Hapo kijana mmoja kwa jina Emmanuel alisimama na kumpa pongezi kwaa shairi lake Salim Shekh.

*"Nakusabahi salamu, zangu zipokee mama,*
*Na nyingi hamu na ghamu, na mengi ya kuyasema,*
*Niazime leo zamu, mwanawanchi nikisema,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako*

*Nchi yenye wendawazimu, haisogei dawama,*
*Ukweli kwenu ni sumu, unafiki umezama,*
*Kutaka kumwaga damu, kisa ni kibaki chama,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako.*

*Nyuso zenu binadamu, matendo yao wanyama,*
*Katiba kutoheshimu, ni viapo kujichoma,*
*Amani mwaikirimu, silaa ziko kwa nyuma,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako.*

*Mama kiti kiko kwako, Amani kushikamana,*
*Lisikufike anguko, wapinzani kukiona,*
*Madaraka si chereko, nayo kodi 'songamana,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako.*

*Amani ili iweko, haki utu ni 'peana,*
*usawa vyama paweko, siyo kupendeleana,*
*Sheria isiwe fuko, mabaya kufichiana,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako.*

*'pendo wa kweli pambiko, jipambe nalo kwa sana,*
*Katiba ni hitajiko, ile mapya tuja ona,*
*Uthubutu wa tamko, kamati zimejazana,*
*Una nafasi kutenda, liwe baya zuri kazi kwako."*

Hili lilikuwa shairi la himizo kwa Mheshimiwa Nyota. Rais, nafasi unayo mkononi.

*****MWISHO******